

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 17 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kabla ya kuanza, naomba kwanza kabisa nitoe salamu za rambirambi kwa wananchi wa Njombe na Mafinga ambao juzi walipata ajali kubwa sana. Bahati mbaya sana nilisikia ajali hiyo wakati nikiwa Botswana. Wamepoteza maisha ya watu wengi sana pamoja na Mkurugenzi wetu wa Mipango Miji amepoteza mke wake na watoto wawili na amekwenda kuzika Bukoba, jana ndiyo walipita hapa. Niwaombe wawe wavumilivu katika kipindi hiki, hiyo ni kazi ya Mungu haina makosa.

Baada ya hayo, namwita Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami naomba niungane nawe kuwapa pole waliopoteza maisha na Mwenyezi Mungu awape nafasi ya kuvumilia yaliyojitokeza.

Na. 209

**Mtandao wa Barabara za Lami, Changarawe  
na Udongo Wilayani Hai**

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

(a) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ina mtandao wa barabara za lami, changarawe na udongo za kilomita ngapi?

- (b) Je, Serikali imetoa kiasi gani kwa ujenzi wa barabara hizi kwenye mtandao wa barabara kwa miaka kumi iliyopita na kati ya fedha zilizotolewa, ni kiasi gani kimetumika kwa ajili ya ukodishaji wa mitambo ya ujenzi?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kutoa mitambo ya ujenzi kwa Halmashauri za Wilaya kwa utaratibu maalum ili kupunguza kiwango cha fedha kinachotolewa kwa kazi ya ujenzi na ukarabati kila mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niungane na wewe kuwapa pole hao ambao umetupa taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 412 na zimeainishwa katika mchanganuo ufuatao:-
- (i) Kilomita 23.05 ni barabara za lami sawa na asilimia 5.6;
  - (ii) Kilomita 197.1 ni barabara za changarawe sawa na asilimia 47.8; na
  - (iii) Kilomita 197.85 ni barabara za udongo sawa na asilimia 46.6.
- (b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kuanzia mwaka 2005 hadi 2015, Serikali imekwishatoa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai jumla ya shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hizo. Baada ya Serikali kusitisha matumizi ya wataalam wa Halmashauri katika utekelezaji wa miradi ya barabara yaani *force account* kazi zimekuwa zikifanywa na mkandarasi.

Wazabuni wanapoandaa viwango vya malipo ya kazi hujumuisha gharama za mitambo vifaa, uendeshaji wa ofisi, faida pamoja na nguvu kazi. Hivyo Halmashauri hazitakiwi kuwalipa Wakandarasi fedha za ukodishaji wa mitambo, bali huwalipa Wakandarasi fedha stahiki kwa kuzingatia vipimo vya kazi wanazozifanya.

(c) Mheshimiwa Spika, ushauri wa Halmashauri kuwa na mitambo ya ujenzi wa barabara ni wa msingi, hata hivyo utekelezaji wake unafanywa na Halmashauri zenyewe kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa. Mfano, zipo Halmashauri ambazo zimeweza kununua mitambo ya aina hiyo zikiwemo Mbinga za Masasi hasa baada ya kupata kibali kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Hai inaweza kuweka kipaumbele na kuainisha chanzo za fedha zitakazotumika kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kuwasilisha maombi hayo kwa Waziri mwenye dhamana ili kupata kibali cha kununua mitambo hiyo.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mbassa swali la nyongeza!

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu ya Naibu Waziri yaliyotolewa. Kwa kuwa shughuli za ujenzi wa barabara katika Halmashauri zetu zinagharimu fedha nyingi sana na matengenezo yanayofanyika muda mwingi hayazingatii thamani ya fedha au *value for money*. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muhimu wa kuwaagiza Madiwani pindi hizi kandarasi zinapotolewa ili nao washirikishwe waweze kusimamia vizuri shughuli hizi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa gharama hizi zinakuwa ni nyingi sana Waziri mwenye dhamana haoni sasa kuna haja ya kutoa wito au kuziandikia Halmashauri kwamba ziweke vipaumbele kwa ajili ya kununua mitambo hii ambayo kimsingi katika Halmashauri zetu nyingi hatuna na ndiyo maana gharama hizi zinakuwa kubwa? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza, hili ambalo anazungumzia Madiwani kushirikishwa. Kule kinachofanyika katika Halmashauri zetu, kuna kitu kinaitwa Kamati ya Zabuni yaani zabuni yenyewe inakuwa na Bodi yake pale na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika huwa anamteua mmoja wa wale Wakuu wa Idara ambao wana manunuzi madogo kuliko idara zingine zozote. Yeye ndiye anakuwa Mwenyekiti wake, mle ndani wanaingia *Ma-engineer, Procurement Managers* na watu wengine wanaingia pale wanafanya maamuzi pale.

Mheshimiwa Spika, wakishafanya maamuzi kwa Sheria iliyopitishwa hapa Bungeni, wanakwenda kwenye Kamati ya Fedha kuiarifu kwamba sisi tunamwona. Wanamchukua mtu anaitwa *the lowest evaluated bidder* ndiye anayepewa kazi ile. Akishapewa kazi ile, wanaondoka moja kwa moja wanakwenda kwenye Kamati na ile Halmashauri itakapokutana katika *Full*

*Council*, watapea taarifa kwamba walishapitisha huu utaratibu ambao nauzungumzia hapa. Kwa hiyo, kwa namna au nyingine Halmashauri inahusishwa kwa utaratibu huo nilioueleza.

Mheshimiwa Spika, la pili, hili analisema la kuruhusu Halmashauri zinunue mitambo nimeeleza. Nikasema Mbinga wameshafanya hivyo, Masasi wamefanya hivyo na ziko Halmashauri zingine ambazo zinaendelea kufanya hivyo. Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambayo inazungumzwa hapa unaposema unakwenda kununua *grader* moja ni shilingi milioni 550 na hiyo unazungumza *caterpillar. Roller* pale shilingi milioni 550, *excavator* milioni 550, jumla bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai mwaka huu tulionao ina bilioni moja na milioni 31 ambazo zimetengwa kwa ajili ya Halmashauri, *so far* tumeshawapelekea milioni 800. Kiwango kinachoruhusiwa kuchukuliwa kwenye *Road Fund* ni *two percent only* na *two percent* ya hizo hela nilizotaja hapo ni shilingi milioni 20, ndizo ambazo zitafanya. Nataka kuonesha kama jambo hili linawezekana, hakuna mtu anayebisha. Njombe pale mkisema ninyi mko tayari kununua na hela yenu mtaipata hapa mtaruhusiwa, haina tatizo.

**SPIKA:** Sisi tumenunua, tulikopa na deni tumemaliza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sawa kabisa na wao kama wanaweza wakakopa, watakopa lakini lazima wapate kibali cha Waziri mwenye dhamana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Machali swali lingine la nyongeza!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja dogo la nyongeza. Suala la ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali hapa nchini zile ambazo zinahudumiwa na *TANROAD* lakini pia hata hizi ambazo ziko chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ni mambo ambayo yanaigharimu Serikali pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia Wakandarasi umeonekana kuigharimu Serikali pesa nyingi, lakini pia upo utaratibu ambao zamani ulikuwa ukutumika huu wa *force account* ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameueleza. Naomba kupata kauli ya Serikali ni kwa nini Serikali isiimarishe Idara ya Uhandisi ili kuhakikisha tunatumia utaratibu wa *force account* ambayo ni njia nyepesi na ambayo inaiwezesha Serikali kuokoa pesa nyingi, badala ya kutumia Wakandarasi, pengine tunaweza kujikuta tumetengeneza barabara nyingi kwa muda mfupi kuliko utaratibu wa sasa ambao Serikali inaonekana inajielekeza sana kwenye kutumia Wakandarasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hata wewe mwenyewe umetuambia kwamba ninyi Njombe mmenunua *graders* na wamefanya hivyo. Kuzungumza habari ya *force account* hapa ni vizuri tukawekana sawa tukajua tunazungumza nini. *Force account* ina sheria yake ambayo imewekwa pale. *In fact it's only two percent* ya *Road Fund* niliyozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, unaposema hivi maana yake ni nini, ni kwamba habari ya *procurement* na hii nyingine tuliyoeleza ya wazabuni ina-*fallout*, unakwenda pale katika Halmashauri unamtumia mtu anayeitwa Mhandisi wa Halmashauri. Mhandisi wa Halmashauri atakachofanya pale ni kwamba yeye atakwenda kutafuta ma-*grader*, *excavator* na vitu vingine. Asimamie yeye mwenyewe pale ambapo kabisa kabisa haiko katika Sheria kama tunavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba ina-*allow* tu, wako watu walio pembezoni huko, tusitaje maeneo ya watu lakini wako pembeni kiasi ambacho ukitangaza kwamba unataka mzabuni hakuna mtu anayejitokeza. Hapo ndipo tunapozungumza kitu kinachoitwa *force account*. Pili, wanazungumza habari ya *single sourcing* kwamba unaweza ukampata Mkandarasi mmoja tu kwa sababu wengine hawakujitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika hili analisema hapa, ukipeleka pale maana sasa una-*introduce* ile habari ya kule tulikotoka. Maana yake ni kwamba, hata *pump* ikipasuka pale inatakiwa iende ikatengenezwe kwa milioni 15, Kamati ya Fedha lazima ikae kwanza na Kamati ya Fedha inakutana mara moja tu katika mwezi. Maana yake utaingiza urasimu pale, wataanza vurugu, tunataka haki zetu, tunaonewa na vitu vingine vya namna hiyo. Naiona *point* yake kwa sababu inatokana na uhalisia anaouona kule. Hapa tuzungumze namna ya kuboresha utaratibu tulionao, lakini Sheria ya Manunuzi ilivyo sasa hivi hairuhusu hii, inaruhusu *only two percent*.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, kwa niaba yake Mheshimiwa Machali!

Na. 210

### Huduma za Kijamii Mpanda

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. SAID A. ARFI)** aliuliza:-

- (a) Je, kutokuwepo kwa huduma za msingi za kijamii kama vile barabara na maji kwa wananchi waliopisha upanuzi na ujenzi wa viwanja vya ndege Mpanda ni msingi wa utawala bora?
- (b) Je, ni hatua gani zimefikiwa za kuondoa kero hiyo baada ya Tume kufika na kuzungumza na wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 Serikali ilitwaa baadhi ya maeneo ili kuwezesha shughuli za ujenzi za uwanja wa ndege katika Mji wa Mpanda. Ili kutekeleza azma hiyo Serikali ilitoa baadhi ya maeneo ya wananchi ili kuwa na eneo la kutosha kwa ajili ya kazi hiyo. Upanuzi huu ulihusisha maeneo ambayo hayakuwa maalum kwa ajili ya makazi ya watu kuishi yaani *informal settlement*. Wananchi waliohamishiwa eneo la jirani ambalo linajulikana kama *Airtel* katika Kata ya Nsemulwa na kupewa viwanja vilivyopimwa na Halmashauri walikwenda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa eneo la upanuzi wa uwanja wa ndege ulifanyika kwa kuzingatia Sheria ya utoaji ardhi yaani *the Land Acquisition Act 1967*, kifungu kidogo cha (3) na cha 11(i) pamoja na Sura ya 113(3)(i) na (g) cha Sheria ya Ardhi namba nne (4) ya mwaka 1999 ambapo uthamini wa ardhi na mali zisizohamishika ulifanyika kwa fidia na zililipwa kwa wakazi waliopitiwa na zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri ambayo ni Mamlaka ya Mpango Miji ya Mpanda Mjini ilifanya maandalizi ya mpango wa kina namba 39MPND/30/022010/3 ulioidhinishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tarehe 23 Septemba, 2011. Mpango huu uliainisha maeneo ya barabara, huduma za kuabudu, huduma za afya, maeneo ya soko pamoja na maeneo ya makazi.

- (b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa kero kwa wananchi waliondoka katika maeneo yao kupisha ujenzi wa viwanja vya ndege, ni kweli Mkuu wa Wilaya ya Mpanda aliunda Kamati ya kusimamia na kuhakikisha haki inatendeka ili kila mwananchi aweze kulipwa fidia anayostahili. Kazi ya ulipaji fidia kwa wananchi hao imekamilika.

Hatua zingine zilizochukuliwa na Serikali ni ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 1.5 kwa gharama ya shilingi milioni 30 katika eneo la *Airtel* liliko katika Kata ya Nsemulwa na ujenzi wa mradi wa maji wa Ikorongo ambao una vituo viwili vya kuchotea maji na tayari wananchi wanapata huduma za maji safi na salama kupitia mradi huo Serikali itaendelea kuimarisha huduma za jamii ikiwa ni pamoja na kuongeza huduma zingine katika maeneo hayo kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Machali, maswali ya nyongeza!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kazi ya ulipaji fidia kwa wananchi hao imekamilika, lakini inaonekana baadhi ya wananchi hawa hawajalipwa. Sasa naomba kauli Serikali ni lini wananchi hawa ambao bado hawajalipwa nao watalipwa kama ambavyo baadhi wamekwishakulipwa?

Mheshimiwa Spika, pia huduma hizi zingine za msingi za kijamii ambazo wananchi wanazihitaji kupitia Mbunge wao ameeleza katika maswali yake ya msingi, inaonekana bado ni hafifu pamoja na kwamba kuna vituo ambavyo vimejengwa pale. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inapanua wigo wa kusogeza huduma hizi karibu zaidi na wananchi? Kwa sababu suala la vituo viwili na *population* ya eneo hilo inaonekana kwamba havitoshi. Ndiyo maana Mbunge wao anasisitiza hapa, je, Serikali itapanua huduma hizi kama za maji, umeme na miundombinu mingine kama barabara ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma kikamilifu?

**SPIKA:** Ahsante, lakini hotuba imekuwa ndefu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme jambo moja ili tuweke picha hapa. Nimezungumza na Mkurugenzi Suleiman Lukanga asubuhi hii na nitakupa namba zake za simu ili u-test kama ninachosema ni kweli. Haya maswali yote anayouliza Mheshimiwa Machali nami nimemuuliza. Ninachotaka kusema hapa kwa zoezi la watu waliotoka katika ule uwanja wa ndege wakaenda eneo la *Airtel* pale kwa *records* walizonazo wanasema kwamba, walilipwa kila kitu.

Mheshimiwa Spika, wamekwenda katika eneo moja linaitwa Nsemulwa ambapo kuna shule ya msingi ya Nsemulwa. Katika eneo hilo ndipo ambapo kuna matatizo watu wengi walipoona watu wamehamishwa wakakimbilia katika eneo lile, watu wapatao mia nane wakabana pale. Walipobana katika eneo lile, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, huduma inayopatikana pale iko chini kidogo ukilinganisha na idadi ya watu waliokwenda pale.

Mheshimiwa Spika, nimemwagiza Mkurugenzi Mtendaji kwanza lazima ahakikishe watu wanaokaa pale wanastahili kupata hizo huduma na hii inajibu swali la pili analouliza kuhusu maji na vitu vingine. Hii habari inayozungumzwa hapa ni *once upon a time* kulikuwa na tatizo hilo likatatuliwa kwa kiwango hicho nilichokisema cha watu wapatao 411, likawa limefanyika na wamemaliza. Sasa wamehamia wengine eneo limepanuka na idadi ya watu inavyoongezeka pale maana yake na huduma nazo zitatakiwa pale.

Mheshimiwa Spika, *look at my eyes* pamoja na Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza, mimi nitasimamia kuhakikisha kwamba eneo hilo litashughulikiwa. La pili ambao wameniambia pia watalifanya hapa wale unaosema hawakufidiwa, hawa watakuwa *considered* katika viwanja 800 ambavyo vimepimwa pale kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo na hili nalo kumwagiza kwamba, pamoja na kusema watu waliohama kutoka uwanja wa ndege wameshafidiwa wote, lakini bado kuna watu wengine. Hapa maana yake ni hii ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, waliopewa hela na wao watakwenda kuomba viwanja na watapitia taratibu zile za kulipia kama watu wengine ili wananchi walioko kule wasije wakafikiri kwamba viwanja vitagawanywa bure pale. Wale waliopata hela wamekwenda na wao wakaenda kuomba viwanja kama watu wengine ambao Mheshimiwa Mbunge anasema kuwa hawakupata fidia, watakuwa labda hawakwenda kuomba, lakini nitakwenda kupitia kwa undani zaidi ili niweze kujua undani wa jambo hili analosema Mheshimiwa Machali.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Moses kasema kirefu na mjibu swali naye kajibu kirefu. Itabidi tuendelee na Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu. Mheshimiwa Fakharia Khamis atauliza swali hilo!



Na. 211

**Mikoa Iliyofanikiwa Kutokana na Mradi  
wa TASAF II**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Mradi wa *TASAF II* ulikuwa umejikita katika miradi ya jamii na kwa kiasi fulani mradi huo ulifanikiwa katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania:-

- (a) Je, ni mikoa mingapi kwa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar imefanikiwa kutokana na mradi huo?
- (b) Je, Serikali inatuambia nini kwa ile Mikoa ambayo haikufanikiwa miradi yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mradi wa *TASAF* awamu ya pili ulitekelezwa kwa kipindi cha miaka minane kuanzia mwaka 2005 hadi 2013, mradi huu ulitekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar katika kipindi hicho Mikoa na Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar ilifikiwa.

Jumla ya miradi 12,347 ya sekta mbalimbali ilitekelezwa katika ngazi mbalimbali za jamii yenye thamani ya shilingi bilioni 430. Kwa kiasi kikubwa mikoa mingi ilifanikiwa isipokuwa kuna miradi michache haikukamilika wananchi walishiriki kikamilifu katika miradi hiyo kwa kufanya kile walichotakiwa ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano na kupanga shughuli za miradi kujitolea nguvu kazi na vifaa pale ilipobidi na kuzingatia maelekezo wakati wa utekelezaji.

- (b) Mheshimiwa Spika, kiujumla hakuna mkoa ambao haukufanikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi ilitekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar japokuwa haikwenda katika kila kijiji au shehia. Miradi ambayo haikukamilika iliorodheshwa na kuingizwa kwenye mipango ya Halmashauri kwa ukamilishaji.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Fakharia swali la nyongeza!

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri na kumpongeza kwa jawabu lake zuri alilolitoa kwa kuufahamisha umma kwamba *TASAF* imefanikiwa na namwambia hongera na Mungu ampe mafanikio na shughuli zake zingine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nina majibu mawili madogo...

**SPIKA:** Hapana, labda una maswali.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Aah! Nina maswali mawili madogo. La kwanza ni kwamba, wamechukua kigezo gani hata wakaona Mikoa hiyo imefikiwa na mafanikio, Wizara ilifanya kigezo gani nilitaka nielewe.

Mheshimiwa Spika, pili, kama mikoa hiyo imepata mafanikio, je, Wizara ilitoa tuzo gani au elimu gani kwa kuipongeza mikoa hiyo kwa mafanikio iliyoyafikia? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu kwa kifupi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, vigezo ambavyo vimechukuliwa kuona mafanikio. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Fakharia kwa sababu ni mmoja wa Wabunge wengi ambao kwa kweli wamekuwa wakiipongeza Serikali kwa miradi ya *TASAF* ambayo iliwapa wananchi mafanikio.

Mheshimiwa Spika, sasa vigezo vilivyotumika, miradi hii ilikuwa ya aina nyingi, lakini cha kwanza ni kukamilisha na kufikisha huduma ambayo ilikuwa inaletwa na miradi hiyo. Kwa mfano, maji, mafanikio yake ni kuona kwamba wananchi wanachota maji na kama ni mradi wa barabara, mafanikio yake ni kuona kwamba, barabara imejengwa na inatumika na miradi mingine mingi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nilivyosema mikoa yote imefanikiwa isipokuwa kuna miradi michache haikukamilika, kazi yetu sisi ilikuwa ni kupeleka habari njema kwa wale ambao wako nyuma kuiga mifano ya mikoa ile ambayo imefanya vizuri zaidi. Kwa sababu bado tunaendelea na *TASAF* bado tutaendelea kutoa elimu hiyo na nina hakika *TASAF* itaendelea kuwanufaisha wananchi na hasa awamu hii ya nne ambayo ni kuondokana na umaskini kwa Kaya zilizo maskini sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Limbu, swali lingine la nyongeza!

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Naipongeza sana Serikali kwa kuja na Mpango huu wa *TASAF* na Wilaya ya Magu imefaidika sana na miradi mingi

ikiwepo barabara ya kwenda Nobola mpaka Mahaha kule na mambo mengine mengi. Awamu hii inayoendelea sasa kaya maskini zimelengwa ili kuondoa umaskini na kupambana na tatizo kwamba uchumi unakua lakini umaskini haupungui au unapungua kwa kasi ndogo.

Mheshimiwa Spika, kila familia maskini ilipewa kwa takwimu nilizonazo ilipewa takribani sh. 160,000. Nakubaliana na wazo hilo kwamba, ni wazo zuri, lakini Waziri haoni kwamba kama wangeweza kuwapatia familia maskini sh. 100,000 halafu sh. 60,000 wakawawezesha kupanda miti ya matunda kama maembe ya kisasa ambayo yanazalishwa pale SUA na maeneo mengine ili baada ya miaka mitatu waweze kupata sh. 100,000 kwa muda wa miaka 15 mfululizo? Je, Serikali haiwezi kubuni sasa katika awamu inayokuja kufanya utaratibu wa kuwawezesha hawa maskini waweze kuwa na miradi itakayowaingizia kipato cha uhakika muda mrefu?

**SPIKA:** Ahsante, swali zuri sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza kwa kufuatilia miradi hii ya *TASAF* na hata kujua takwimu za hela zilizopelekwa katika kaya na nakubaliana na yeye kwamba kuwapa fedha kwa ajili ya kujikimu na kwa ajili ya kupeleka watoto shule na kuwapeleka hospitali haitoshelezi, inatakiwa wawe na miradi ambayo hatimaye wataachana na umaskini. Pia nakubaliana naye kwamba, tuwe na miradi ambayo ni endelevu ili waendeleo kuwa na vipato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachukua ushauri wake na haitakuwa ni maembe kila mahali kwa sababu kuna maeneo ambayo maembe huwa hayakui, kwa hiyo, pale ambapo maembe yanawezekana tutafanya hivyo, pale ambapo machungwa yanawezekana, tutafanya hivyo. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

**SPIKA:** Haya tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar anauliza swali hilo, kwa niaba yake, Mheshimiwa Jaddy Simai!

Na. 212

### Wahindi Wanaofanya Kazi Kwenye Night Clubs

**MHE. JADDY SIMAI JADDY (K.n.y. MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR)** aliuliza:-

Hivi karibuni imeripotiwa katika vyombo vya habari kwamba wamekamatwa baadhi ya watu wenye asili ya Kihindi wakifanya kazi kwenye club za starehe za usiku (*Night Club*) na kazi zisizokuwa na heshima

- (a) Je, ni nani aliyewapa watu hao kibali cha kufanya kazi hizo na kimetolewa kwa misingi gani?
- (b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika waliowaleta watu hao nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni wamekamatwa wasichana 21 wenye asili ya Nepal na India kwenye club za starehe za usiku Jijini Dar es Salaam. Vibali vilivyotolewa kwao na Serikali kupitia Uhamiaji na Baraza la Sanaa (BASATA) kwa misingi kwamba, kazi za halali za wasanii wa ngoma za asili za utamaduni wa India na Nepal. Hata hivyo, kwa bahati mbaya badala ya kufanya shughuli hizo walikiuka masharti ya vibali na kufanya kazi ambazo zilikuwa ni kinyume na masharti ya vibali vyao na kinyume na maadili yetu ambapo baada ya kubainika hivyo wasichana hao walirejeshwa makwao.
- (b) Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa kwa wahusika waliowaleta wageni hao ni pamoja na:-

- (i) Kuwashtaki Mahakamani kwa makosa ya kiuhamiaji na yale yaliyoangukia katika biashara haramu za usafirishaji wa binadamu;
- (ii) Kufuta vibali vya ukaazi vya raia wanne wa India wenye Kampuni ya *Dhamak Entertainment Limited* ambayo ndani yake ilikuwa ikiendesha klab mbili za starehe za usiku zinazojulikana kwa majina ya *Hunters Night Club* iliyopo Kinondoni na *Continental Night Club* iliyopo Mnara wa Saa Jijini Dar es Salaam. Wahusika hao ndiyo waliowaleta wageni hao na kuwafanyisha kazi hizo za aibu;

- (iii) Kuwafukuza na kuwazuia kuingia tena nchini kutokana na makosa waliyoyatenda; na
- (iv) Kutaifisha baadhi ya mali zao zilizotumika katika biashara hiyo haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaddy, maswali ya nyongeza!

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kazi hii inashamiri siyo tu Tanzania, bali duniani kote, je, kwa upande wake Serikali yetu ina mkakati gani wa kulikomesha kabisa suala hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, si amewaachia nyie nafasi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, ingawa biashara hii ni kongwe sana, lakini upanukaji wake kwa sasa hivi duniani inatisha. Kama Serikali ni lazima tuwe na mikakati ambayo itasaidia kulinda heshima za watoto, lakini pia na wazee wetu, tunayo mikakati mikuu kama mitatu. Kwanza ni kuhakikisha kwamba, kupitia Idara ya Uhamiaji na vyombo vingine vya usalama, kupitia katika maeneo mbalimbali siyo tuya *Night Clubs* lakini maeneo ya biashara ambayo yanaweza kuvutia mambo kama haya.

La pili, tumeunda Kikosi Kazi ambacho kinahusika na suala la mwenendo wa usafirishaji wa binadamu na utumikishaji wao katika mambo ambayo ni ya udhalilishaji.

Tatu, tunashirikiana na vyombo vingine kama Polisi wa Kimataifa na pia taasisi zingine za nchi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunapata taarifa ili kuweza kudhibiti nchi yetu isiwe eneo baya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlata, swali lingine la nyongeza!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini naomba nimuulize kwamba kwa sababu kitendo hiki kwanza kinadhalilisha hata kazi za sanaa kwa watu kuingia nchini kwa kutumia kigezo cha sanaa, kwa maana hiyo hata Ubalizi wa nchi hiyo uliopo hapa Tanzania unahusika na wale walioko kule wanahusika lakini Uhamiaji pia wanahusika. Je, ni hatua zipi sasa ambazo zimechukuliwa kwa vipengele vyote

kuanzia uhamiaji, Ubalozi wa Nepal na Maafisa walioko kule ambao waliwaruhusu kuja hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, siyo mara zote kwamba kosa analolifanya motto, mama au baba analifahamu na kwa sababu jambo hili lilifika Mahakamani na Mahakama ikawatia hatiani ambao walihusika. Kwa hiyo, naomba kutoa taarifa na kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pengine kuna kasoro ndogo, lakini siyo kwamba wanahusika kwa maana ya kushiriki katika hili, vinginevyo Mahakama ingewaona nao kuwatia hatiani.

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana baada ya mapumziko marefu uliyokuwa nayo. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, anachozungumzia ni suala la wanawake ambao walikamatwa katika madisco na swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omari linatokana na baada ya kwenda kwenye *club* hizo. Sasa naomba kujua, kurudishwa kwao ni sawasawa na watu ambao wanakuja nchini kwetu kuchunguza na kufanya uhasama au kushambulia, lipi ni bora na nini sababu yao kurejeshwa hawa?

**SPIKA:** Kurejeshwa kwao, si wametuletea taabu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, vyombo vya sheria au kusimamia sheria wanachokifanya ni kuwadhibiti wacosaji na wacosaji wako wengi na aina za makosa ziko nyingi. Tatizo siyo kwenda *club* ya usiku au vinginevyo, lakini ukishafika *club* na nini, ndiyo matatizo ambayo tunayafuatilia. Kwa sababu hawa wametoka nchi za kigeni na *infact* tunavyowaona hawa ambao wamerejeshwa siyo kwamba wao ni wacosaji, wametendewa makosa kusafirishwa na kudhalilishwa. Kwa hiyo, hawa kwetu sisi tunaita ni wahanga na hawa tumewarejesha kwa sababu wamedhalilishwa na wamelaghaiwa ili wafanye hicho walichokifanya.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wao nchini ulifanywa na chombo cha Kimaitaifa kinachohusiana na *Immigration* au Uhamiaji (*IOM*) kwa sababu hili kosa la kuwasafirisha watu na kuwatumikisha visivyo ni kosa la Kimataifa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, siyo hiyo nongwa basi mnataka mwendeele tu. Sasa namwita Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura!

## Fidia kwa Kupisha Mradi wa Bandari Kavu – Butungu

**MHE. SEBREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Je, ni katika Bajeti ya mwaka gani wananchi wa eneo la Butungu katika Manispaa ya Kigoma Ujiji watalipwa fidia ili kupisha mradi wa Bandari Kavu katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Tathimini ya utwaaji wa eneo la Katosho lililopo katika Manispaa ya Kigoma Ujiji lenye ukubwa wa hekta 69 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari Kavu lilikamilika mwaka wa 2013. Tathimini ilibaini kwamba jumla ya shilingi bilioni 12.043 zinahitajika kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wakazi 1,228 watakaopisha eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilianza kulipa fidia kwa wakazi wa eneo hili mwezi Aprili mwaka huu, hadi kufikia tarehe 15 Juni, mwaka 2015, jumla ya wakazi 1135 wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni 10.1. Fidia kwa wakazi 93 waliobaki watalipwa wakati wowote baada ya wao kukamilisha taratibu za kibenki.

**MHE. SEBREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu kutoka kwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo ya nyongeza, kwa kuwa taratibu za uthamini na ulipaji kwa ajili ya maeneo ya ardhi ambayo yamekuwa yakipisha miradi taratibu nasheria zinajulikana. Miongoni mwa taratibu na sheria ni pamoja na kutoa *notice* ya siku 21, kuweka majina na kuonesha kiwango cha kila mhusika atakacholipwa, lakini kwa kuwa sheria hii imekuwa ikikiukwa na kusababisha watu wengi kulipwa fidia chini ya kiwango, mtu analipwa milioni mbili na milioni mbili hiyo hawezi hata kupata kiwanja kipya. Je, Serikali sasa iko tayari au Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda katika eneo husika kuona upungufu uliojitokeza na hatua madhubuti kuweza kuchukuliwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Waziri anaweza kutuambia muda mahususi ama tarehe mahususi ya watu waliobakia kulipwa fidia zao na ziwe ni fidia toshelezi na stahiki na zisiwe ni fidia zenye dhuluma? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli taratibu na sheria inayosimamia mambo ya fidia inafahamika na ni wajibu wa pande zote kuhakikisha kwamba sheria hiyo imefuatwa kama ilivyo. Sisi katika ulipaji wa fidia eneo la Katosho Sheria ilizingatiwa kwa maana ya kwamba, taratibu zote za uthamini kwa kuhusishwa wananchi wenyewe, viongozi wao wa mitaa, Halmashauri husika, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa na Mdamini Mkuu wa Serikali zilifuatwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo ni kwamba, wakati mwingine wananchi hawaridhiki kwamba malipo yale kama yalivyoainishwa katika majedwali yale ya fidia hayatoshi. Kwa hivyo, sheria pia imesema utaratibu wa kufuata endapo mwananchi atakuwa anaona kwamba fidia aliyothaminiwa haifanani na hicho alichokuwa akitarajia yeye, lakini kwa suala la Kigoma utaratibu wote ulifuatwa.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu muda mahususi lini, wananchi hawa watalipwa fidia yao, wale 93 waliobaki. Ni kwamba wao wenyewe ndiyo wamechelewesha ulipwaji wao, kwa sababu wanachotakiwa ni baada ya kufungua zile akaunti zao, wapitie kwa Viongozi wa Vijiji vyao waende Mkoani pale, wakathibitishwe kwamba zile akaunti ndizo za kwao kweli na uongozi wa Mkoa *immediately* uta-transfer hiyo *information* kule Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na fedha zipo, hata leo wakikamilisha hizo taratibu watalipwa fedha zao. Nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Sungura kwenda kuona tatizo hilo watakapokuwa tayari.

**SPIKA:** Aah! Watu hata hapa Bungeni hawapo, halafu mnaanza kwenda huko, hiyo si kweli.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Mallole ataulizwa swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Badwel!

Na. 214

**Kuwatumia Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya  
Dodoma Kuboresha Elimu**

**MHE. OMARY A. BADWEL (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE)** aliuliza:-

Kuwepo kwa Vyuo Vikuu vya St. John's na UDOM kumesababisha ongezeko la watu katika Manispaa ya Dodoma:-

Je, Serikali inawatumiaje wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo hivyo kuboresha elimu kwa kuwapanga kufundisha kwenye shule zilizoko pembezoni mwa mji wakati wa mazoezi yao ya BTP ili kupunguza kero ya upungufu wa Walimu katika shule nyingi za Dodoma Mjini?



**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazoezi ya kufundisha (*Teaching Practice*) huwa yanafanywa kwa kuzingatia Mwongozo wa Mazoezi ya Kufundisha (*TP Guidelines*) ambapo kila chuo huwapanga wanafunzi wanaosoma program za Ualimu katika shule mbalimbali kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kufundisha.

Mheshimiwa Spika, mahali pa kwenda kufanya mazoezi ya kufundisha ni suala la utashi wa wanafunzi. Kabla ya kupangiwa, wanafunzi hutakiwa kuchagua mikoa mitatu na shule tatu ambazo wangependa kwenda kufanya mazoezi ya kufundisha. Mkoa hupangiwa Walimu-wanafunzi wa kwenda kufanya mazoezi ya kufundisha iwapo watafikia 20 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Mwongozo wa Mazoezi ya Kufundisha, Vyuo Vikuu vya St. John's na Dodoma vimekuwa vikiwapangia Walimu-wanafunzi kufanya mazoezi ya kufundisha katika shule za Halmashauri zilizopo Mkoani Dodoma ikiwa ni pamoja na Manispaa ya Dodoma. Kwa mfano, mwaka 2012, Chuo Kikuu cha St. Johns kiliwapangia wanafunzi 325 na mwaka 2013 walipangwa wanafunzi 249. Aidha, Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mwaka 2013 kiliwapangia wanachuo 114 katika shule mbalimbali mkoani Dodoma kufanya mazoezi ya kufundisha. Kwa takwimu hizi, ni wazi kuwa Vyuo Vikuu tajwa vimeweza kupunguza kwa muda changamoto ya upungufu wa Walimu katika shule husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Badwel, maswali ya nyongeza!

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa hivi vyuo vyote alivyovitaja Mheshimiwa Waziri vipo Dodoma na inaonekana Walimu hawa wanafunzi wamekuwa wakifanya mafunzo katika hizi shule ambazo zipo Manispaa, lakini Mkoa wa Dodoma una Wilaya zingine pia katika Halmashauri zetu mbalimbali. Je, Wizara ina ushauri gani kuhusu Walimu hawa wanaopangiwa ili waweze pia kupangiwa katika Wilaya zingine za Mkoa wa Dodoma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, shida kubwa inayoonekana sasa ni Walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari na kwa ujumla nchi nzima. Je, Serikali ina mpango gani kabambe kuhakikisha kuwa hawa Walimu wa sayansi wanapatikana katika miaka hii miwili ama mitatu inayokuja?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu kupangia Walimu-wanafunzi hawa kufanya mazoezi katika Halmashauri zingine ndani ya Mkoa wa Dodoma, hivyo ndivyo inavyofanywa na nikitoa mfano wa mwaka 2010/2011, Dodoma Manispaa, Kongwa, Mpwapwa na Kondoa zilipangiwa Walimu na Chuo Kikuu cha Dodoma, hali kadhalika St. Johns ya Dodoma ilipanga Walimu katika shule za Halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Dodoma, siyo tu Manispaa ya Dodoma. Hii ikiwemo Gairo Sekondari, Hazina, Itega, Kizota na Kongwa Sekondari. Kwa hiyo, ni Halmashauri tofauti tofauti katika Mkoa wa Dodoma siyo tu Manispaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la upungufu wa Walimu wa sayansi...

**SPIKA:** Bahi hakuna, hawakwenda!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, sina uhakika kwa sababu orodha hii ni ndefu na sijaiona Bahi hapa.

Tutawashawishi vyuo waangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba, kwa vyuo hivi vilivyopo Dodoma, basi vinajitahidi kutenda haki kwa kuwatengea shule za kufundisha Walimu-wanafunzi katika Halmashauri zote na niziombe Halmashauri nazo ziweke mazingira yenye kuvutia kwa wanafunzi hawa ili wachague Halmashauri hizo kwenda kufundishia.

Mheshimiwa Spika, namba mbili upungufu wa Walimu wa sayansi. Tunafanya juhudi kubwa sana. Hapa kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma tumeanzisha program maalum ya sayansi na ualimu ama Walimu katika masomo ya sayansi. Tulikusudia tuwe na wanafunzi elfu tano na kidogo, lakini waliofika ni elfu mbili na kidogo. Mwaka ujao wa masomo tunatarajia kuongeza idadi hiyo ili tuwe na Walimu wengi zaidi hapa katika Chuo Kikuu cha Dodoma, lakini pia tumeanzisha program kama hizo katika Vyuo vingine vya Ualimu tofauti na Chuo Kikuu cha Dodoma.

**SPIKA:** Ahsante. Muda uliotumika katika swali hilo ni mwingi sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, kwa niaba yake Mheshimiwa Mshama.

Na. 115

## Majengo ya FDC Kutumiwa kwa Chuo cha Ufundi

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA (K.n.y. MHE. SELEMANI S. JAFO)** aliuliza:-

Chuo cha FDC Kisarawe kina majengo ya kutosha ya kuwezesha kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Ufundi VETA:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuboresha Chuo cha FDC Kisarawe ili kiweze kufanywa Chuo cha Ufundi VETA ili vijana wengi wa Kisarawe waweze kupatiwa mafunzo mbalimbali ya stadi za kazi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali ya kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kutumia Vyuo vya VETA, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na Vyuo binafsi vya ufundi stadi. Hii inatokana na utafiti juu ya mahitaji ya soko la ajira ambao umeonesha uhitaji mkubwa wa Mafunzo ya Ufundi Stadi. Ndiyo maana katika mafunzo yanayotolewa kuna mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVETDP) unaotekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2013/2014. Moja ya malengo ya mpango huu ni kupanua na kuboresha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo kuvijengea uwezo vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe ili viweze kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kiwango cha Vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kilianza kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi mwaka 2014 katika fani za ufundi magari, umeme wa majumbani, ujenzi, uhomeleaji na uunganishaji vyuma, ushonaji na matengenezo ya kompyuta kwa kutumia rasilimali watu na vitendea kazi vilivyopo.

Hivyo, si nia ya Serikali kubadili matumizi ya majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kuwa ya VETA bali ni kuongeza aina ya mafunzo yanayotolewa yaende sambamba na utoaji wa mafunzo ya elimu ya wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mshama, maswali ya nyongeza!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali la msingi la Mheshimiwa Jafo, ni kwamba yeye angependa au anatamani kile chuo kibadilike kiwe cha VETA, kwa nini? Kikiwa kamili Chuo cha VETA kuna faida nyingi sana ambazo zinapatikana kwa sababu kinakuwa chini yake. Hivyo miongozo yote inapotolewa na zile faida za kuwa chini ya VETA zinapatikana moja kwa moja kuliko wakiwa chini ya FDC. Hivyo nadhani angependa kusikia kwamba mnabadilisha na mkibadilisha kunakuwa tayari kama kuna tatizo anakuja moja kwa moja kwenye mlolongo wa VETA. Je, lini kitabadilishwa ili kiweze kuwa na ustadi wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hiki chuo kipo sawasawa na Chuo chetu cha Gera, pale ni Gera ni chuo ambacho kilikuwa kimejengwa kwa thamani sana, majengo ni mazuri yameanza sasa kuharibika na kipo chini ya FDC. Matokeo yake ili wapate huduma ya VETA, VETA wanasema ninyi hamko kwetu, mpo chini ya Maendeleo ya Jamii na matokeo yake kinazidi kuporomoka.

Naibu Waziri wa Elimu alivyotembelea alitaka kiwe chini ya VETA. Naomba kama inawezekana itusaidie kiwe chini ya VETA ili elimu ya haki, usawa na yenye uwezo iliyo bora iweze kupatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri na wewe jibu kwa kifupi tafadhali, maana yake inaonekana, nachukua aliyeuliza swali na wewe tu basi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe, kama vile Vyuo vingine vya Maendeleo ya Wananchi katika mikoa mingine, Serikali haina mpango wa kuvibadilisha vyuo hivi kuwa vyuo vya VETA kamili. VETA itaendelea kujenga vyuo ambavyo vitasimamiwa na Mamlaka ya VETA, lakini pia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuongeza idadi ya Taasisi ya elimu ya ufundi stadi katika nchi yetu. Huo ndio msimamo ya Serikali na hivyo ndivyo tutakavyofanya kwa sasa na kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, swali la kile Chuo cha Gera, Kagera kama nimekisikia vizuri, vyuo vyote 55 vya Maendeleo ya Wananchi ama FDC, vyote tutavijengea uwezo viweze kutoa mafunzo ya ufundi stadi. Tumeanza na 25, awamu ya pili itakuja vyuo 16 na awamu ya mwisho ya tatu itakuwa vyuo 14, ili vyote viwe vinatoa mafunzo ya ufundi stadi yanayofanana na yale yanayotolewa na VETA.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Masauni!

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sera ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wanajenga vyuo vya VETA kila Wilaya. Je, mpaka sasa ni kwa kiwango gani Serikali imefanikisha malengo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nia na madhumuni ya Serikali ni kujenga Chuo cha VETA kwa kila Wilaya, niseme kwamba mpaka hivi sasa hatujaweza kufanya hivyo kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu ya matatizo kadhaa ya upatikanaji wa fedha. Tumekamilisha Chuo cha Makete lakini katika mpango wa mwaka huu wa fedha, tuna vyuo vitano ambavyo vipo katika taratibu mbalimbali za ujenzi, lakini tuna vyuo vinne vya Mkoa, Mkoa wa Geita, Simiyu, Rukwa pamoja na Njombe ambavyo vimeshatengewa pesa zaidi ya bilioni sita katika mwaka huu wa fedha, kwa ajili ya ujenzi. Tutaendelea katika kasi hiyo hiyo ya kuhakikisha kwamba nia hiyo tunaitekeleza kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Ezekiel Maige!

Na. 216

### **Kujenga Chuo cha VETA- Msalala**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kujenga Vyuo vya VETA kwa kila Wilaya na Msalala walishaahidiwa na Mheshimiwa Rais kuwa watajengewa Chuo cha VETA katika eneo la Bugarama na eneo hilo lilishatengwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo iliyotolewa mwaka 2010?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Wilaya, Serikali ilipanga kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi kwa awamu. Kigezo kikubwa ni kuanza kujenga Chuo katika Wilaya ambazo hazina kabisa Chuo chochote cha Ufundi Stadi cha Serikali, Taasisi au Binafsi. Wilaya ya Kahama ina Chuo cha Ufundi cha Mtakatifu Francis kinachomilikiwa na Taasisi ya dini kilichopo Isaka na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanva.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ni mojawapo ya Halmashauri zilizopo katika Wilaya ya Kahama ambayo ilianzishwa mwaka 2013. Wakati Halmashauri hiyo inaanzishwa, Serikali ilishateua Wilaya 43 zisizo na Chuo chochote cha Ufundi Stadi ili zijengeve Vyuo vya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imetenga eneo la ekari 10 katika Kata ya Bugarama kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya. Hata hivyo, eneo lililotengwa halikidhi hitaji kwa ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya kama ilivyoelekezwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) yaani ekari 75 au hekta 30. Nashauri eneo hilo liongezwe, Serikali itajenga chuo hicho baada ya ujenzi wa Vyuo vya Wilaya vilivyoko kwenye awamu ya kwanza na ya pili kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige, maswali ya nyongeza!

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kwanza nitoe masikitiko yangu kwamba, inawezekana mawasiliano yaliyopo ndani ya Serikali si kamilifu sana, kwa sababu Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni mwaka 2010, maombi mahususi ambayo wananchi wa Msalala walimwasilishia ni suala la kujengewa Chuo cha Ufundi, kutokana na mazingira ya uwepo wa mgodi hasa mgodi wa Bulyankhulu, unaovutia vijana wengi kuwepo lakini hawawezi kupata kazi zozote kwa sababu ya ukosefu wa elimu na Mheshimiwa Rais akakubali. Kwa hiyo, hili ni ombi mahususi la Rais ambalo lipo katika ahadi zake na si miongoni mwa zile VETA za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa sababu hitaji la Chuo cha Ufundi VETA kwenye eneo la Bugarama ni mahususi kutokana na mazingira yaliyopo na kwa kushirikisha wadau mwekezaji wa mgodi wa *Acacia* Bulyankhulu yupo tayari kujenga chuo hicho, endapo Serikali itakubaliana naye kujenga chuo hicho kutokana na mrabaha ambao mgodi ungeweza kulipa Serikalini. Je, Serikali ipo tayari kumwandikia au kumruhusu ajenge hicho chuo ili katika malipo ya mrabaha aje akate gharama alizotumia kujenga chuo hicho, ili chuo kiweze kujengwa na fedha kutoka Serikalini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa chuo pekee kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ni hiki chuo cha Taasisi ya dini cha Kanisa Katoliki cha Mtakatifu Francis cha Isaka na kwa sababu chuo hiki ni cha sekta binafsi na gharama zake ni kubwa na wanafunzi wengi wa kawaida wanashindwa kupata fursa kutokana na gharama hizo. Je, Serikali ipo tayari kutoa ruzuku ya ada kwa wanafunzi wanaokwenda kudahiliwa kwenye chuo hicho ili waweze kumudu gharama za kusoma pale na kupata wanafunzi wengi wanaosoma mafunzo haya?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu utayari wa Bulyankhulu *Gold Mines* kushirikiana na wananchi wa Msalala kujenga chuo cha mafunzo ya ufundi stadi. Serikali inakaribisha nia hiyo kwa mikono miwili na tupo tayari sana kushirikiana na Mbunge kwa juhudi zake kubwa za kuwashawishi, kwa sababu sidhani alifanya hivyo ofa tu, bila Mbunge huyu kuwashawishi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nipo tayari kushirikiana na Mbunge kwa kazi yake hii na nimwombe Mbunge ashirikiane na Halmashauri ili Halmashauri ituwasilishie maombi maalum ya ujenzi huu na nimhakikishie kwamba tutashiriki kwa kila namna kuweza kulitekeleza jambo hilo, isipokuwa azingatie kwamba eneo lile nalo inabidi liongezwe kwa sababu maelekezo ya VETA ni mahsus kwamba wawe na angalau hekta 30.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu ruzuku ya ada kwa wale wanafunzi ambao wanasoma St. Francis, bahati mbaya hatuna uwezo huo kwa sasa, tungependa kufanya hivyo kwa Vyuo vyote vile visivyokuwa vya Serikali. Jumla yake vipo 670 vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi visivyokuwa vya Serikali na tungependa kuwasaidia wale ambao wanakwenda kule, kwa sasa uwezo huo hatuna, lakini tutaangalia kadri uwezo unavyopanda, namna ambavyo tunaweza kuvi-support ama vyuo vyenyewe ama wanafunzi ambao watakuwa wanajiandikisha humo.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendeleo na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, kwa niaba yake Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 217

### **Kampeni ya Nyota ya Kijani**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE)** aliuliza:-

Miaka ya nyuma Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliendesha kampeni iliyojulikana kama Nyota ya Kijani ambayo ilielimisha jamii juu ya suala zima la mpango wa uzazi, kudhibiti ongezeko kubwa la watu lakini kampeni hizo hazisikiki tena:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kampeni hizo ili kulinda afya ya wanawake na watoto na kudhibiti ongezeko la watu kiholela?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miaka ya nyuma Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliendesha kampeni ya nyota ya kijani ambayo ilielimisha jamii juu ya suala zima la mpango wa uzazi, kudhibiti ongezeko la watu. Kampeni haijasimama kwani bado inaendelea katika sehemu mbalimbali nchini kote.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau wa uzazi wa mpango, walizindua upya kampeni ya nyota ya kijani katika Mikoa ifuatayo:-

Mwanzo ilikuwa tarehe 20 Mei, 2014 ambako mimi mwenyewe nilizindua kampeni hiyo. Shinyanga ilikuwa tarehe 21 Januari, Simiyu tarehe 21 mwezi Mei, Geita ilikuwa tarehe 2 Juni na Mara tarehe 9 Juni, mwaka jana. Kwa sasa wadau wa uzazi wa mpango wanaendelea na kampeni ya uhamasishaji wa nyota ya kijani kwa kutumia redio na *television*. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa uzazi wa mpango iko kwenye mpango wa kuzindua upya nyota ya kijani mwezi Agosti mwaka huu katika Mikoa ya Katavi, Singida na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, uhamasishaji wa kampeni ya nyota ya kijani, unaendelea nchini kote na katika maeneo ya vijijini mbinu mbalimbali za kuhamasisha jamii zinatumiwa ikiwemo redio, *television*, vipeperushi, vijarida, mabango pamoja na *road shows*.

Mheshimiwa Spika, aidha, elimu ya afya kuhusu uzazi wa mpango imeendelea kutolewa na watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma. Pia watoa huduma huwatembelea wananchi katika jamii ambako watoa huduma za mkoba pamoja na kutoa elimu ya uzazi wa mpango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, maswali ya nyongeza!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa tafiti mbalimbali zilizofanywa inaonekana bado elimu ya uzazi wa mpango haijajieleweka ipasavyo na bado kuna ongezeko kubwa la uzazi usiokuwa na mpango na unachangia sana kuwepo kwa watoto wengi wa mitaani. Jambo hili pia linahusiana kwa karibu na imani pamoja na mambo ya kimila. Sasa Serikali imeshirikiana vya kutosha na Viongozi wa Dini na mila zetu ili kuhakikisha jambo hili linafanikiwa ipasavyo? Hilo swali la kwanza.



Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunapozungumzia Wizara hii ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, lakini tumeona *focus* kubwa ipo katika upande wa afya na ndiyo maana unakuta kuna chombo cha Madaktari na chombo cha Manesi, lakini kwa upande wa Ustawi wa Jamii imeachwa sana hata ukija bajeti ni ndogo na wao wameandaa sera, lakini je, ni lini Serikali mtaleta sheria ili kiwepo chombo kina-*deal* na Ustawi wa Jamii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza kwamba Serikali imeshirikisha vipi vyombo mbalimbali ikiwemo vya dini na mashirika mengine pamoja na jamii hususani kujielekeza katika mila. Ni kweli suala hili la uzazi wa mpango siyo la Wizara ya Afya pekee bali hushirikisha Wizara zingine kama eneo mtambuka. Mashirika ya dini pamoja na jamii kupitia mila, zoezi hili linaendelea katika nchi nzima kama ambavyo tumeanza rasmi kuhamasisha upya yaani ku-*revamp* katika *family planning* kulingana na mkutano uliokaa London kuhusu *Family Planning 2020*, suala hili limejumuisha maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwamba suala zima la ustawi wa jamii kuhusu sera; maandalizi ya awali yameshakamilika juu ya Sera ya Ustawi wa Jamii na tunaandaa iende katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na baada ya hapo *IMTC* waweze kukamilisha utaratibu huo na hatimaye sera hii iweze kutoka. Rasimu imeshakamilika bado kuwasilishwa katika vyombo husika.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Sara Msafiri atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Abdulsalaam Amer!

Na. 218

### Uzalishaji wa Sukari Nchini

**MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER (K.n.y. MHE. SARA M. ALLY)** aliuliza:-

Viwanda vya sukari hapa nchini vimeshindwa kuzalisha sukari ya kutosha hivyo kusababisha uhaba mkubwa sana kwa watumiaji wa bidhaa hiyo muhimu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuagiza sukari ya kutosha kutoka nje?

(b) Je, ni vigezo gani vinatumika kumruhusu mfanyabiashara kuagiza sukari kutoka nje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi huzingatia kiwango cha uzalishaji wa ndani wa sukari na mahitaji halisi ya sukari kwa wakati husika. Kwa sasa mahitaji ya sukari nchini ni wastani wa tani 5,090,000 ambapo tani 420,000 ni kwa matumizi ya nyumbani na wastani wa tani 170,000 ni kwa matumizi ya viwandani.

Mheshimiwa Spika uzalishaji wa sukari nchini kwa mwaka ni wastani wa tani laki tatu ambazo ni kwa matumizi ya nyumbani na hivyo Serikali kulazimika kuagiza kiasi cha wastani wa tani 290,000 kila mwaka ili kufidia pengo la uzalishaji. Kati ya kiasi hicho tani 120,000 ni kwa matumizi ya nyumbani na wastani wa tani 170,000 ni kwa matumizi ya viwandani. Aidha, kwa kuzingatia uzalishaji na mahitaji ya sukari nchini, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango ya upatikanaji wa sukari ya kutosha kwa wananchi kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi umeainishwa katika Kanuni za Sukari za mwaka 2010 (*The Sugar Regulations 2010*), kwa mujibu wa kanuni hizo, Bodi ya Sukari ndiyo yenye dhamana ya kutoa leseni ya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi. Kanuni hizo zimeanzisha Kamati ya Ushauri ya Ufundi ya Uagizaji Sukari (*The Technical Advisory Committee on the Sugar Importation*) ambayo ina jukumu la kushauri Bodi ya Sukari juu ya kiasi, punguzo la kodi na muda wa uagizaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, kanuni hizo zimeainisha vigezo ambavyo wafanyabiashara wanatakiwa kutimiza ili waruhusiwe kuagiza sukari kutoka nje ya nchi. Vigezo hivyo ni pamoja na wafanyabiashara kusajiliwa na Bodi ya Sukari, uthibitisho wa uhalali wa kampuni kwa kuwa na leseni ya biashara, namba ya mlipa kodi (*TIN*) na usajili wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*), uthibitisho wa uwezo wa kusambaza sukari nchini, uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutoka taasisi za fedha na uthibitisho mwingine kadri Bodi itakavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, uagizaji wa sukari kwa Nchi zote Wanachama wa Jumuiya ni lazima uidhinishwe na Baraza la Mawaziri wa Nchi za Afrika Mashariki (*Council of Ministers*).

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulsalaam, maswali ya nyongeza!

**MHE. ABDALSALAAM SELEMANI AMER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Wakulima wa Miwa wa nje (*out growers*) kila mwaka wanalalamika miwa yao inalalia kwa sababu haivunwi na viwanda husika. Mfano, Kiwanda cha Kilombero (K1 na K2). Sasa je, ni lini Serikali itaweza kuvishauri au kuviambia viwanda hivyo viongeze mitambo ya kuzalisha sukari ili miwa yote ya watu wa nje iweze kuvunwa kwa wakulima wa bonde la Luhembe na Kilombero, Wilaya ya Kilosa na Wilaya ya Kilombero ili kupunguza wazo la kudumu kwamba kila mwaka tuna upungufu wa tano 290,000. Naomba Serikali iwashauri kwa sababu ina hisa katika kampuni zile ili waweze kuongeza viwanda vya kuzalisha sukari na wakulima wavuniwe miwa yao yote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hawa wakulima wa miwa wanachangia zaidi ya asilimia hamsini ya miwa ambayo inauzwa viwandani. Je, ni lini Serikali itaweza kuwasaidia au kuwakopesha wakulima hawa wadogo waweze kupata mitambo yao ya kutoa sukari ili ipunguze upungufu wa sukari nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimtoe Mheshimiwa wasiwasi kwamba ni kweli tuna kitu kinaitwa pengo la uzalishaji wa sukari kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya msingi. Pia tumegundua kwamba viwanda vyote hivi viwe vya kule Kagera, Kilombero kama alivyosema yeye mwenyewe tumekuwa na tatizo la miwa ya wakulima wa nje (*out growers*) kupata soko kwa viwanda vile. Sasa tumechukua hatua, Bodi ya Sukari imeshamaliza kufanya upembuzi yakinifu ili tuweze kuanzisha viwanda vya kati pamoja na viwanda vidogo vya uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo muda mrefu sana viwanda hivyo vitakwenda kujengwa na miwa ya wakulima kama yeye alivyosema na kama ambavyo Wizara tunatambua miwa hiyo itapata soko la kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maana ya suala la kuwakopesha wakulima, hili tumekuwa tunasisitiza wakati wote kwamba wakulima hawa na tunajua wana umoja wao, lakini wawe na kitu kama umoja au SACCOS vile, vitu ambavyo vinaweza vikawafanya wakopesheke wao kwa pamoja kuliko wakienda mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunayo Benki ya *TIB* na wale ambao wameitumia kwa ajili ya kukopa katika uwekezaji wamepata mikopo hii. Kwa hiyo, nina hakika hata wakulima wa miwa hawa *out growers* wanaweza kabisa kukopa kupitia *TIB* na benki nyingine ili

wapate mitambo kwa ajili ya kuwawezesha pia kujenga viwanda vyao vya sukari wao wenyewe.

**SPIKA:** Haya jamani tunatamani kuendelea wee, lakini muda umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwatambue baadhi ya wageni tulionao. Tunao wageni wa Mheshimiwa Festus Limbu ambao ni wanafunzi 46 na Walimu wane na wazazi 10 kutoka shule ya Sekondari Kitumba. Naomba hawa jamaa zetu wanafunzi, Walimu na wazazi wasimame kama wamo humu ndani. Ahsante sana. Wazazi, Walimu na watoto tunawatakia masomo mema ahsante sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Highness Kiwia kutoka Chuo cha Mipango Ilemela. Naomba na hawa wasimame kama wapo, karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu tunao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo; kuna wanafunzi 30 na Walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Mughanga, Singida. Naomba hawa wasimame kama wapo humu ndani, nadhani wamekosa nafasi kwa sasa.

Vile vile tunao wanafunzi 192 na Walimu 26 kutoka shule mbalimbali za Msingi katika Jiji la Arusha ambao ni Shule ya Msingi Elerai wasimame, ahsante sana. Shule ya Msinga Burka wasimame, ahsante sana. Kuna Shule ya Msingi ya Azimio wasimame kama wapo mahali, ahsante sana. Kuna Shule ya Msingi ya Unga *Limited* wasimame hapo walipo, ahsante sana. Kuna shule ya Msingi ya Baraa nao wasimame, ahsante sana. Tuna Shule ya Msingi ya Sokoni One, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Hawa wanafunzi karibu wote wanatoka Arusha na Walimu wao tunawashukuru sana kwa kuwaleta wanafunzi. Sisi tupo siku za mwisho mwisho, lakini ninyi endeleeni kusoma kwa bidii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wanafunzi 30 na Walimu Wawili kutoka shule ya Mtakatifu Terezya ya Morogoro wasimame kama wamo, nafikiri wamekosa nafasi watapata nafasi baadaye. Wale waandaaji mnaweza pia kuwaingiza kwenye *Speakers Lounge* sina wageni leo.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengineyo ni kwamba Katibu Mkuu wa APNAC, Tanzania Mheshimiwa Vita Kawawa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati Kuu ya APNAC Tanzania kuwa leo tarehe 17 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati Kuu ya APNAC katika ukumbi Na. 227 ghorofa ya pili. APNAC mnajua ni Chama cha Wabunge cha kupambana na rushwa kwa hiyo Kamati Kuu yake inakaa leo.

Waheshimiwa Wabunge, nami natangaza Wenyeviti, Kamati ya Uongozi ya Bunge tutakutana saa saba. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

na

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

(Majadiliano yanaendelea)

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mwongozo wangu, Mwongozo wako tena!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Sorry Madam, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), lakini pia nitarejea Kanuni ndogo ya 64(1). Kufuatia majibu ya Waziri wa Afya kwenye swali alilouliza Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye swali la afya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo huu kwa sababu majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri na akataja London *Summit* ni uwongo na kinyume kabisa...

**SPIKA:** Mwongozo wangu eleza sasa unachotaka kuniambia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Natambua kabisa afya ya uzazi wa mpango ni muhimu kwenye nchi yetu na ukizingatia miundombinu ya afya kwa maana ya *dispensary* na vifaa vingine vyote, ingesaidia sana kama Serikali inge-*invest* kwenye hii idara ya afya ya uzazi wa mpango. Iliazimiwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Kikwete alisema atahakikisha ameboresha afya ya uzazi wa mpango kwa asilimia 60 ambapo walisema watatenga bilioni 20 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea tangu isemwe haijawahi kutengwa hata bilioni nne, leo Waziri anajibu hapo anasema kwamba wanakwenda kutekeleza hilo Azimio la 2020, ni vipi Serikali inaweza ikatuambia hapa, inashindwa kutenga 20 bilioni kwa ajili ya afya ya uzazi wa mpango ambapo

najua kabisa inge-*invest* kwenye afya ya uzazi wa mpango ingesaidia kwenye kutatua wananchi wengi sisi wanawake tunapata mimba, miundombinu ya uzazi ni mibovu, inapelekea vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Spika, anavyojibu anajibu ndivyo sivyo, naomba kabisa Wizara ituambie kwa mfano mwaka huu wa fedha imetenga kiasi gani kwenye hiyo idara ya uzazi wa mpango na maazimio ni 20 bilioni kwa kila bajeti ya mwaka tunaokwenda.

**SPIKA:** Kwanza Mwongozo siyo *clear*. Naomba mkae chini nikisimama. Ninachokisema hapa Mwongozo wenyewe siyo *clear* na hapa umefanya majadiliano yanaingia kwa Waziri wa Fedha mnajadili hapa, basi *noted*. Serikali ni moja.

Mheshimiwa Ester siyo uchanganye hapa mambo!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, sitaki kuchanganya na namheshimu sana wajina wangu na analolisema ni sahihi, lakini uzazi wa mpango katika swali nililoulizia mimi ni tofauti na anachokisema yeye. Uzazi wa mpango ambao kwa hii operesheni ambayo tunaisema ni kuhusiana na watu kutozaa ovyo. Haihusiani na miundombinu, suala la miundombinu hata mimi nakubaliana naye. Swali nililoliuliza hapa ni kutoa elimu kwa wananchi kuzaa kwa mpango (kutozaa watoto wengi) ndiyo swali langu lilikuwa linahusu hivyo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wajina amechanganya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hebu kaeni chini wote na mwendelee na kazi. Mheshimiwa Esther Matiko, tulia. Tatizo la watoto hawa huwa hawasikii! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, haya aliyosema Mheshimiwa Esther Matiko tunazungumza bajeti, lakini suala la uzazi wa mpango ni suala la wananchi wote na suala la sera na suala la kufa na kupona. Kwa hiyo, tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana jana ni kwamba, mtaongea kwa dakika kumi na tano. Sasa nianze na Mheshimiwa Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Kasembe, Mheshimiwa Badwel, Mheshimiwa Kangi Lugola, halafu atafuatia Mheshimiwa Hamad Ali Hamad. Tuanze na hawa kwanza. Mheshimiwa Maige!

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kama mchangiaji wa kwanza leo kuchangia Bajeti ya Serikali. Naomba nianze mchango wangu kwa kuipongeza sana Serikali kwa ujumla wake, kwa juhudi kubwa ambayo imefanyika katika kipindi cha miaka tuseme

kumi sasa ya Awamu hii ya Nne katika kuongeza makusanyo ya Serikali. Kuongezeka kwa makusanyo haya kumeiwezesha Serikali kutekeleza Miradi mingi ya Kimaendeleo na kutoa huduma nyingi za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Jimbo langu la Msalala, tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kwenye sekta karibia zote za kijamii. Ukiangalia kwa mfano suala la upatikanaji wa umeme, idadi ya vijiji ambavyo havikuwa na umeme mwaka 2005 na idadi ya vijiji ambavyo leo hii ukifika utashangaa. Yote hii ni kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali. Mimi kama Mbunge na kama Wabunge wote ambavyo tumekuwa tukifanya, kazi yetu ni kuiomba Serikali iweze kutoa fedha. Isingewezekana Miradi hii kufanyika kama Serikali ingekuwa haikusanyi fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napongeza sana hatua kubwa iliyofanyika katika Miradi ya Umeme kwenye Jimbo langu, ambako tunategemea hadi kufika Septemba mwaka huu, kama Wakandarasi watatekeleza kwa mujibu wa mikataba yao, basi katika Kata 24 za Jimbo la Msalala, tutakuwa tumebakisha Kata sita tu ambazo ambazo kwa namna moja ama nyingine, hazijaguswa na mtandao wa umeme kutoka kwenye wastani wa Kata nne zilizokuwepo mwaka 2005. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imefanyika kazi kubwa vilevile kwa upande wa elimu. Katika Kata zote za Jimbo la Msalala zimebaki Kata mbili ambazo ni mpya zilizoanzishwa mwaka 2008, ambazo bado hazijakamilisha kuwa na Sekondari, lakini Kata nyingine zote zina Sekondari.

Kwa kiasi kikubwa miundombinu kwenye shule hizo ipo ya kutosha, japo upungufu hauwezi kukosekana. Imewezekana kufanyika hivyo kwa sababu Serikali imekuwa ikikusanya fedha. Kuna Miradi mingine inayoendelea hata hivi sasa kwa mfano Miradi ya Barabara na Maji, niombe tu Serikali kwa kadiri inavyowezekana inavyoendelea kukusanya, basi fedha zitolewe mapema ili Miradi hii iweze kukamilika na wananchi waweze kupata huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ambazo Serikali imefanya, bado kuna maeneo ambayo nafikiri inaweza ikafaa yakatazamwa kwa ajili ya kuboresha. Kwanza, wigo wa kodi bado siyo mkubwa sana. Nimesikia kwa mfano, mwaka huu kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri, angalau kodi zimeongezwa kwenye mafuta, kama eneo mojawapo ambalo linategemewa kwa kiasi kikubwa na kama walivyochangia baadhi ya Wabunge, sioni kama kuna tatizo kubwa kwenye eneo hili kama usimamizi utakuwa mzuri kudhibiti *spiral effect* ya ongezeko la bei inayoweza kutokea kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta kutokana na ushuru unaoongezwa. Hata hivyo, naamini bado kuna maeneo mengine ambayo yanaweza yakatazamwa. Yako maeneo

ambayo yanaweza yakawezeshwa yakasimama yenyewe na mengine yanaweza yakasaidiwa yakakusanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa maeneo mawili. Kwanza, eneo la utalii. Kumekuwepo mapendekezo miaka ya nyuma kwamba, *TTB* au Bodi ya Utalii, inaweza kabisa ikabadilishiwa Sheria yake kwa kuiunganisha na Idara ya Utalii kwenye Wizara na kuunda Mamlaka ya Utalii ambayo itakuwa inakusanya fedha kutoka kwenye sekta na kujendesha yenyewe kama zilivyo sekta nyingine; kwa mfano, *TCRA* pamoja na mamlaka nyingine za kiusimamizi. Nchi nyingine wanafanya hivyo na mafanikio ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi *TTB* inategemea kupata fedha kutoka Serikalini, haikusanyi chochote. Sheria waliyonayo ni ya kuwawezesha tu kutangaza utalii basi. Ingeweza kuboreshwa Sheria ile, hata kama ukiweka tozo ya asilimia moja tu kwenye mapato yanayotoka kwenye Sekta ya Utalii ambayo kwa sasa yanakaribia dola za kimarekani bilioni moja na kitu, maana yake ni kwamba, ukiweka tozo ya asilimia moja, unaweza ukawa unakusanya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni mia moja kama na hamsini au mia moja na zaidi, ambazo zinaweza zikasaidia sana kutangaza utalii na kwa maana hiyo, ikapunguza hitaji la Serikali kuchangia Bajeti ya *TTB*. Jambo hili linawezekana, tunafikiri likitazamwa kwa sura hiyo tunaweza tukapunguza mzigo wa fedha kutoka Wizara ya Fedha kupeleka *TTB*, Taasisi ambayo inaweza ikajitegemea kutokana na makusanyo yanayopatikana huko.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la madini. Bado kazi ambayo imefanyika kwenye eneo hili ni kubwa, lakini bado tunaweza tukafanya kazi kubwa zaidi. Utoroshaji wa madini bado upo mkubwa hasa kwenye sekta ambazo zinafanyiwa utafiti. Kwa mfano, kwenye maeneo ambayo wanafanya utafiti wa uchimbaji, si uchimbaji rasmi, maeneo mengi yaliyotolewa leseni za uchimbaji hasa kwa wachimbaji wakubwa, udhibiti wa madini yanayopatikana kwenye maeneo hayo bado siyo mkubwa na kwa maana hiyo, utoroshaji bado unakuwepo. Vilevile sekta yenyewe bado mchango wake siyo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na majadiliano kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, kuongeza mrabaha kutoka asilimia tatu kwenye madini ya dhahabu hadi asilimia nne. Ziko kampuni ambazo zimekwishakubali, lakini ziko kampuni kwa mfano *ACACIA*, wamekuwa wakikaidi kupandisha ushuru huo, jambo ambalo sioni hasa ni kwa nini wanakuwa wanasita. Naamini Serikali ikikaza buti kwenye eneo hilo, tunaweza tukaongeza makusanyo zaidi na kupunguza athari kwenye maeneo mengine ambayo yana athari kwa Wananchi.



Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo kubwa ambazo zimefanyika, nataka niombe sana na niishauri Serikali kwamba, nidhamu ya matumizi bado ni changamoto kubwa sana. Ukiangalia kwenye bajeti yenyewe, Bajeti ya Serikali, iko Miradi ambayo tumeiahidi na iko kwenye Ilani na iko kwenye Bajeti ya Serikali, lakini haipewi fedha. Badala yake tunakuwa na Miradi mingine ambayo naamini ingeweza isifanyike kwa sababu kwanza haipo kwenye Ilani, haipo kwenye Mpango na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka jana, Bajeti ya Wizara ya Maji tulikubaliana tutakuwa na bilioni nane kwa ajili ya kupeleka maji kwenye Miji Midogo ya Kagongwa na Isaka. Mpaka hivi tunavyozungumza, fedha zilizotolewa hazifiki milioni 400 na hakuna kazi yoyote ya maana iliyofanyika na mwaka unakwisha. Ukiangalia umuhimu wa Miradi kama hii ambayo tumeiahidi na inagusa wananchi moja kwa moja, unaweza ukaona pengine ingefaa sana baadhi ya Miradi ambayo tumeiibua sasa hivi ingeweza isifanyike.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mifano ya Miradi kadhaa ambayo tumeianza na haijakamilika. Tuna Mradi mkubwa wa Vitambulisho vya Taifa ambao unaendelea kwa kusuasua. Ulianza kidogo na baadaye ukawa umepotea kimyakimya. Athari yake ni kwamba, Mradi huo umechukua kiasi fulani cha fedha na haujakamilika. Baadaye tumekuja tena na mpango huu wa kuwaandikisha wapiga kura upya kabisa. Ingewezekana tungeweza ku-update daftari lililopo kwa kutumia vitambulisho vya zamani na ku-update wale ambao hawana vitambulisho ingekuwa rahisi.

Sasa tumekuja na mpango mpya kabisa ambao unatumia mabilioni ya shilingi, kwa haraka haraka sasa hivi uandikishaji unaoendelea katika Mkoa wangu wa Shinyanga kwa mfano, hizi siku saba zinazotolewa hazitoshi na kuna Wananchi wengi tutakaowaacha bila kuwaandikisha kwa sababu tu, tumeanza mpango huu ghafla bila maandalizi mazuri. Kwa maoni yangu, tungeweka nguvu kwenye Vitambulisho vya Taifa, vingeweza kabisa kusaidia, pamoja na vitambulisho vya kupigia kura ambavyo vilikuwepo zamani vikatumika pamoja na Vitambulisho vya Taifa kuweza kupunguza mahitaji ya kifedha kwenye eneo ambalo lingeweza kuwa *postponed* angalau *temporarily*.

Mheshimiwa Spika, ninaamini tukiongeza udhibiti katika matumizi ya Serikali, itatusaidia sana pia kuweza kupata matokeo. Bahati nzuri Naibu Waziri wa Maji yuko hapa, ni rafiki yangu sana na Naibu Waziri wa Kilimo na ninaomba wanisikilize vizuri; kuna Miradi ambayo kwenye vitabu vyao wametoa taarifa kwamba, imetekelezwa, lakini utekelezaji wake ni masikitiko makubwa. Kwenye Miradi kwa mfano ya Maji, katika Miradi ya *BRN* iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, tulikuwa na Miradi ya vijiji vitano na kwenye orodha imetekelezwa vijiji vinne; Kijiji cha Segese, Kijiji cha Burige, Kijiji cha Kagongwa na Kijiji cha Chela.

Mheshimiwa Spika, ukifika katika Miradi hii ambayo yote kwa ujumla wake kila mmoja umetumia si chini ya shilingi milioni 500, Mradi wa Burige hivi tunavyoongea haufanyi kazi, sababu ndogo tu, usimamizi. Mkandarasi kaweka mabomba ambayo hayana ubora, yanapasuka kila wakati, hayawezi kuhimili *pressure* ya maji yanayotoka kwenye bomba la Ziwa Viktoria ambako ndiyo tumeunganisha Mradi huu. Matokeo yake Mradi haufanyi kazi, milioni zaidi ya 700 zimetumika na Mradi hautekelezwi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema eneo hili ni la muhimu na naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla, waweze kutazama. Mradi wa Burigi haufanyi kazi kwa sababu mabomba siyo bora. Mradi wa Kagongwa haufanyi kazi kwa sababu chanzo hakina maji na tulishauri kwamba, kwa sababu utafiti ulionesha kwenye kile chanzo maji yaliyokuwepo ni kidogo, kipatikane chanzo kingine ili kuunganisha na chanzo ambacho kinatumika hivi sasa. Wataalamu hawakutusikia wanasema sisi ndiyo Wataalamu ninyi ni Wanasiasa, matokeo yake zaidi ya milioni 430 zimetumika na maji hakuna hivi tunavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kijiji cha Chela nako hivyo hivyo, tulitegemea kingechimbwa kisima kipya, badala yake hawakuchimba wakaenda kwenye chemchemi ambayo imekuwa ikitumika na wananchi! Maji hayatoshi, Mradi umefungwa, fedha zaidi ya shilingi milioni 500 zimetumika pale Chela, wananchi hawapati maji. Kwa hiyo, kuna usimamizi hafifu sana wa Miradi inayotekelezwa kwa fedha kidogo tunazozitenga.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Zambzi, rafiki yangu, nimekuwa nikimweleza sana kuhusu Mradi wa Umwagiliaji wa Kahanga. Tulitenga shilingi milioni 850 na Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Chela tulitenga zaidi ya milioni 600 na Wakandarasi wakapewa mikataba na wakafanya kazi. Nimekuwa nikisema, ukifika Kahanga hata hii leo thamani ya kazi iliyofanyika haifiki shilingi milioni 150 na wale vibarua hawajalipwa wanadai zaidi ya shilingi milioni 30, imekuwa ni kero ya kisiasa, lakini unaambiwa Mradi umetekelezwa na kwenye Vitabu vya Serikali unaoneshwa kwamba umetekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali, fedha kidogo tunazozikusanya izisimamie vizuri. Kipekee pia niwaombe Viongozi wa Wizara hizi; Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Kilimo, nipate majibu, najua ni Bajeti Kuu ya Serikali, Mawaziri wa Sekta watapata nafasi ya kuzungumza. Ninaomba Waziri wa Kilimo na Umwagiliaji, anieleze Mradi wa Kahanga *fate* yake ni nini? Milioni mia nane na kitu, hazijatumika vizuri, ni ufasidi umetokea pale, sijaona hatua zilizochukuliwa dhidi ya wale ambao naamini wametumika katika ku-*squander* fedha ambazo zilitengwa.

Mheshimiwa Spika, nimetaja Mradi mwingine, Mradi wa Chela, ambao nao ni Skimu ya Umwagiliaji kwa upande huo huo wa Wizara ya Umwagiliaji; nao fedha zimetengwa, hakuna kazi iliyofanyika. Hata ukifika Chela leo hii hakuna mtu anayefanya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba Viongozi wa Wizara hizi waweze kutusaidia kwa maana ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na nimeshapigiwa kengele ya kwanza, nimalizie ombi moja; kuna Mradi wa Umeme ambao unaendelea karibu unakamilika wa kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Segese. Kuna vijiji ambavyo vimepitiwa na umeme, lakini havijaunganishiwa; Kijiji cha Nyikoboko, Kijiji cha Segese tunaita Segese Namba Moja, nyaya zimepita pale. Niliongea na Naibu Waziri, bahati mbaya simwoni hapa, lakini nilimweleza akasema jambo hili ni dogo, kwa sababu Sera ya Serikali ni kuhakikisha sehemu zote ambazo umeme umepita au nyaya zimepita, wananchi wa maeneo hayo wanapata umeme. Naomba sana Serikali itusaidie katika kuhakikisha kabla Mradi huu haujafungwa na Mkandarasi kuondoka *site*, basi hizo sehemu ambazo zimeachwa ziweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, limekuwepo pia tatizo la Taasisi za Umma kutokuunganishiwa umeme. Katika hizi njia za umeme ambazo zinajengwa kwa Mpango wa REA na hata huu Mradi wa kupeleka umeme Bukombe, ambao ndiyo umepita kwenye eneo langu la Segese, kuna Shule za Sekondari, kwa mfano Shule ya Sekondari ya Lunguya, Shule ya Sekondari ya Nyikoboko, ambazo zinapaswa ziunganishiwe umeme pamoja na zahanati hazijaunganishiwa. Ukisikiliza maelezo wanasema wao kazi yao ni kupeleka umeme kwa wananchi kwa maana ya ule Mkataba anavyosema Mkandarasi, lakini kupeleka kwenye hizi Taasisi eti wananchi wanapaswa wachangie!

Mheshimiwa Spika, Waziri nilipomweleza akasema utaratibu ni tofauti na atasimamia kuhakikisha Taasisi za Umma, Vituo vya Afya, Zahanati, Shule za Sekondari na hata Shule za Msingi, zinaunganishiwa umeme moja kwa moja kupitia mkataba ambao Mkandarasi anakuwa amepewa, badala ya kutaka wananchi eti wachangie fedha za kuunganishiwa umeme kwenye Shule yao ya Msingi na Sekondari ya Nyikoboko, wakati Mkandarasi yuko *site* na umeme unapita kwenye kila Kijiji! Naamini ni marekebisho madogo ambayo kwa timu ninayoiona hapa kwa rafiki yangu, ameshafika rafiki yangu Naibu Waziri wa Nishati, wanaweza wakasimamia marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba niseme naunga mkono jitihada za Serikali, naunga mkono bajeti hii. Naomba tu tusaidiane sana katika kwanza, kuweka vipaumbele vinavyotekelezeka na kuvisimamia na kusimamia fedha ziweze kwenda kwenye Miradi. Miradi mingi ya ujenzi, kwa mfano, hata Wakandarasi wa Barabara, ukiangalia mpaka sasa hivi wanadai

zaidi ya shilingi bilioni 600. Fedha walizopelekewa mwezi mmoja uliopita ni chini ya bilioni 40, ambazo hazitoshi kuhimili gharama ambazo wametumia kutekeleza Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia bajeti yetu. Kabla sijaanza kuchangia, naomba nichukue nafasi hii niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Masasi, kwa jinsi ambavyo wamenipa ushirikiano kwa kipindi chote toka 2010 hadi sasa. Nasema ahsanteni sana na nawaomba waendeleo kunipa ushirikiano kama walivyozowea kunipatia.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu naomba nijikite sana kwenye suala la ucheleweshaji wa upelekaji fedha katika Halmashauri zetu. Naomba niwakumbushe kwamba, kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Masasi pamoja na Halmashauri ya Mji wa Masasi, mwaka 2013 tulipata maafa makubwa sana. Maafa ambayo yamesababisha Halmashauri yetu kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi, kushindwa kutekeleza majukumu yanayowagusa ya kila siku kwa sababu ya kukosa Ofisi, vitendea kazi na miundombinu hasa magari.

Mheshimiwa Spika, hili suala linasikitisha sana. Maafa yamefanyika 2013 leo hii ni 2015, hadi hivi sasa Serikali haijachukua jukumu lolote la kuweza kutoa fidia kwa Halmashauri hizi zote mbili, ambazo ofisi zake zilichomwa moto, vyombo vya usafiri vilichomwa moto na magari ya wagonjwa yalichomwa moto! Hivi Watendaji hawa watafanyaje kazi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watumishi wanafanya kazi katika mazingira magumu. Ofisi ya Elimu inabidi wapeane zamu kwenye chumba kimoja, anaingia Afisa huyu anafanya kazi zake, akipunguza anaondoka anaingia mwingine! Kweli hapo jamani tutafanya kazi kweli kwa ufanisi na maendeleo wananchi wakayapata ya kutosha?

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya pekee, nimshukuru sana Mama Salma Kikwete, baada ya kuliona tatizo hili amechukua jukumu la kutuletea gari la wagonjwa. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa sababu tulikuwa katika hali ngumu sana. Tulisharudi enzi za ukoloni za kubebana kwenye machela. Tunasema ahsante sana mama na tunaomba Serikali ifuate nyayo za mama huyu, tusaidiwe kulipa zile fidia tuweze kununua magari mengine, Wananchi waweze kupata huduma zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, suala la maafa ni la dharura halipangwi. Hivi tunavyokaa katika kipindi cha miaka mitatu bila kuchukua hatua yoyote ya kuweza kutatua na tumekuwa tukiangalia katika nchi yetu jinsi maafa yanavyotokea kila wakati. Kweli tuna sababu ya kimsingi hapa ya kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wananchi sasa hivi wako katika mazingira magumu. Mheshimiwa Waziri nakuomba, ninajua kuna sehemu umeweza kusaidia, lakini nakuomba sana ufanye kila utakaloweza, suala la fidia kwa Halmashauri ya Masasi pamoja na Halmashauri ya Mji, hebu tupe kipaumbele hili suala liishe, tuweze kujenga ofisi na vitendeakazi. Sasa hivi watu wa ardhi hawapimi viwanja wala hawafanyi kitu chochote, kwa sababu vifaa vyote vilishachomwa moto. Tunaomba sana au kuna mpango wa kuua hizi Halmashauri zetu, kwa sababu sasa hivi tumesharudi kabisa nyuma kimaendeleo?

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, uskilize kilio cha Watu wa Masasi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii vilevile kuiomba Wizara hii ya Fedha, kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati katika Taasisi zetu ni jambo la msingi sana. Sisi katika Wilaya yetu ya Masasi, fedha tulizokuwa tumetengewa ukiangalia hadi sasa fedha iliyoenda ni kidogo sana. Tulishafikia hatua nzuri, tulishaanza kujenga miundombinu ya barabara katika Mji wa Masasi, imesimama kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Miradi ya Maji kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, imesimama kwa sababu ya kutopeleka fedha kwa wakati. Vilevile tuna wazabuni wanaodai fedha katika shule zetu za sekondari, tumefikia hatua ya kukaribia kufunga shule za sekondari watoto warudishwe majumbani kwa ajili ya kukosa chakula. Ninaomba Serikali iangalie suala la kupeleka fedha katika hizi Taasisi ili kuweza kunusuru kufungwa kwa shule hizi na watoto wakakosa masomo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la wastaafu. Kwenye Wilaya yetu ya Masasi tumekuwa tukipata malalamiko makubwa sana kwa wastaafu wetu. Najua hili limepigwiwa kelele kubwa sana na Wabunge humu ndani, lakini na mimi kwa kuwa nimekuwa nikipata malalamiko haya ya wastaafu, sina budi kuwasemea.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wetu wako katika mazingira magumu sana, baadhi yao sasa hivi wameshageuka kuwa ombaomba. Huwezi kujua kabisa kwamba waliitumikia hii nchi na ni wastaafu ambao tunatakiwa tuwaenzi. Naomba nichukue nafasi hii niungane na wenzangu ambao wamesema kwamba, fedha iliyoongezwa kwa wastaafu kwa kweli haitoshi, ingeongezwa kidogo ikafikia angalau kiasi cha sh. 100,000/=. (Makofi)

Kuongeza pesa peke yake haitatosha kama fedha itakuwa haipelekwi kwa wakati. Wastaafu wanamaliza mwaka mzima, mtu anakwenda benki anapoteza muda wake anaenda kuangalia fedha yake haijaingia. Hivi kwa nini tunafanya hivi? Kwa nini tunawatesa wastaafu?

Wastaafu hawa hawa ndiyo tunaowategemea huko chini, kesho na kesho kutwa hawa hawa ndiyo tunakwenda kuwaomba kura. Tukinyimwa kura tutawalaumu hawa watu?

Wanafikia sasa hatua ya kutoielewa Serikali yetu inawatendea nini wastaafu hawa. Naomba sana tuwe makini kwa suala la wastaafu, tupeleke fedha kwa wakati na hasa ukizingatia fedha yenyewe wanayoipata kwanza ni ndogo na wanaipata kwa shida kubwa sana. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, katika kitengo hiki tuangalie tuweze kuwasaidia wastaafu wetu na wao waweze kuishi kuendeleza maisha yao kwa miaka iliyobaki waliyopangiwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nichukue nafasi hii kuzungumzia suala la umeme vijijini. Wananchi wamelipokea kwa mikono miwili kwa furaha kubwa, kuona kwamba sasa katika vijijiji vyetu kutakuwa na maendeleo makubwa kwa kupelekewa umeme vijijini. Kama alivyokuwa anazungumza msemaji aliyepita, inasikitisha sana kuona baadhi ya vijijini, kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Masasi, Vijiji kama Sululu, Nanganga na vingine, vingi nguzo za umeme zimepita lakini hakuna transfoma, wananchi hawapati umeme.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wananchi hao waligoma kabisa kupiga kura kwa ajili ya kuchagua Viongozi wao wa Vijiji. Tulifanya kazi kubwa sana ya kwenda kufanya vikao na kuwaomba na kuwaelimisha na kuweka ahadi kwamba wafanye uchaguzi, baada ya uchaguzi tutaisimamia Serikali ili na wao waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Rais ametembelea Wilaya ya Masasi, tulimweleza kilio hiki na akaagiza vijiji vyote ambavyo nguzo za umeme zimepita, wawekewe umeme. Inasikitisha hadi sasa vijiji hivi hawajawekewa umeme na mimi ninashangaa, ninatambua kwamba, Rais ndiyo msemaji wa mwisho katika nchi yetu; inakuwaje Rais anaagiza jambo lakini huku chini halitekelezwi? Anayekwamisha ni nani? Hatuoni kwamba tunaondoa hadhi ya Rais, anatoa tamko lakini utekelezaji hakuna! (*Makofi*)

Mimi ningeomba sana kama tatizo ni fedha, kama tatizo ni vifaa, basi liangaliwe katika maeneo yale yote ambayo nguzo za umeme zimepita na vijiji vile hawakupata umeme wapate umeme haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kilio changu kikubwa kilikuwa ni ucheleweshwaji wa pesa za maendeleo katika vijiji vyetu na katika halmashauri zetu; jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo yetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali fedha ambazo zilikuwa hazijapelekwa hadi sasa, muangalie ni namna gani mtazipeleka ili twende tukafanye shughuli zetu za maendeleo, kwa sababu mapato yao ya ndani ya halmashauri zetu kila senti tano inayokusanya pesa zinaenda kwenye maabara. Hakuna shughuli yoyote ya maendeleo inayofanyika katika halmashauri yetu, pesa zimekuwa zikienda katika ujenzi wa maabara. Tunaomba hizi pesa ambazo zilitakiwa ziende katika halmashauri zetu ziende ili Wananchi waweze kupata maendeleo na waweze kurudisha imani kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie suala la mgawanyo wa vijiji. Juzi zimetangazwa kata hapa, kwa masikitiko makubwa, mara ya kwanza vijiji vilipotangazwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu tulipeleka malalamiko kwamba kuna vijiji vingi vimeachwa vinavyostahili kugawanywa na tukaambiwa tuandike barua tupeleke TAMISEMI tukisema sababu za msingi. Tumepeleka, lakini matokeo yake juzi vimetangazwa vijiji vichache sana, kwa mfano, kwenye Jimbo langu tumepata vijiji tunashukuru, lakini vijiji vile ambavyo tulitarajia hasa ndiyo wangeweza kupata katika mgawo huu vimeachwa. Huko jimbo sasa hivi kuna vurugu na wananchi wanasema hawatashiriki katika uchaguzi ujao. Naiomba Serikali iviangalie vijiji hivyo na watueleze ni kwa nini vijiji hivyo vimeachwa bila kupata usajili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema nakushukuru sana. Nitaomba majibu kuhusu suala la maafa, fedha zitaenda lini kwenye halmashauri zetu zote mbili ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Serikali. Wabunge wenzangu wamezungumza sana juu ya hali halisi ya upelekaji wa fedha katika halmashauri zetu. Kwa kuwa na mimi natoka katika halmashauri lazima niseme ili kuonyesha masikitiko kwa namna ambavyo Serikali kwa muda wa miaka miwili, mitatu, hii imeshindwa kabisa kupeleka fedha kwa wakati na kwa ukamilifu kama ambavyo tunapitisha kwenye bajeti zetu katika Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kushindwa kupeleka fedha kwa wakati au kutopeleka fedha kabisa kama tulivyopanga kwenye bajeti na kupitisha Miradi mbalimbali katika maeneo yetu, limekuwa tatizo sugu na linalofanya wananchi washindwe kuelewa sasa Serikali yao kwa sababu Miradi mingi ya Maendeleo imekwama.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka zamani katika halmashauri zetu ndiyo palikuwa mahali muhimu sana pa utoaji wa huduma na kimbilio la wananchi. Leo Mkurugenzi pengine anatamani hata ajifiche katika halmashauri kwa sababu hawezi kutoa huduma hizo mbalimbali ambazo wananchi wanazitarajia kutoka kwenye halmashauri yake, kutokana na Serikali kutokupeleka fedha kwa wakati au kutokupeleka fedha kabisa. Halmashauri leo zimekuwa kama watoto yatima, vikao vya halmashauri kwa mujibu wa sheria havikai kwa wakati, kila unaposikia habari ya kikao ratiba inabadilishwa. Hata hivyo, vikao vyenyewe wamekuwa wakikaa kwa kubangaiza. Imefika wakati halmashauri zimekuwa ombaomba kwa wakandarasi na watu wengine. Kwa kweli jambo hili linatia aibu.

Kama imefikia serikali inaona hizi halmashauri hazina umuhimu, ilete sheria hapa mabadiliko ili tuweze kuzifuta, tuwaachie wao Serikali Kuu majukumu hayo, waweze kuyafanya badala ya kuendelea kuwatesa halmashauri na viongozi wake.

Kwa kweli haipendezi, leo hata Mkurugenzi wakati mwingine anaishiwa hela ya mafuta, hata likitokea jambo la dharura hawawezi kufanya. Jambo hili linasikitika sana na nadhani Serikali sasa ikae iangalie umuhimu wa hizi halmashauri kama ilivyokuwa zamani na kuweza kupeleka fedha kwa wakati kwa Miradi mbalimbali. Kila Mradi katika halmashauri umesimama na leo hii tunakwenda kumaliza mwaka tutapitisha bajeti Ijumaa, lakini halmashauri zingine ikiwemo ya kwangu ya Bahi, haijafikisha hata asilimia 50 ya mapato yaliyopitishwa na Baraza la Madiwani kupelekwa katika halmashauri yenyewe; tunatarajia nini?

Hata sisi Wabunge na Waheshimiwa Madiwani tunaona aibu hata kusimama mbele ya Wananchi. Ufike pale ulikwenda wakati tumepitisha bajeti mmewapelekea barua kwamba hata tutaleta fedha za Mradi huu na huu, lakini leo fedha zile hazikwenda, imefika mwisho sasa wa mwaka uchaguzi umefika, Mbunge na Diwani una kazi ya kwenda kujitetea pale. Kwa hiyo, kazi kubwa sasa imekuwa ya Mbunge na Diwani kwa sababu Miradi ile imeshindwa kutekelezeka wakati waliopaswa kuleta fedha zile katika halmashauri zetu wenyewe wamekaa huku, hatujui hata wako ofisi gani.

Mheshimiwa Spika, mzigo imekuwa ndiyo ule mzigo mzito mpe kabila fulani, sasa tumepewa sisi Wabunge na Waheshimiwa Madiwani. Imekuwa kazi ngumu sana, kuna vijiji unajua kabisa hapa sitopata kura kwa sababu Serikali haikuleta fedha. Wananchi wamehamasika vizuri na mahali pengine kama tunavyowahimiza, wamejenga Miradi ile mpaka hatua fulani na tukawaambia mkifikisha hatua fulani fedha za halmashauri zitakuja. Wamefika hatua ile mwaka wa pili huu, mwaka wa tatu, hawaoni kama tunaendelea nao! (Makofi)



Kwa kweli jambo hili limetuathiri sana kisiasa. Naomba kabisa tupate majibu ya kutosha, isiwe utaratibu wetu tunakuja kupitisha bajeti hapa kama utaratibu halafu bajeti hizo hatuzioni. Tunaona tu kwenye taarifa mbalimbali ongezeko la Pato la Serikali limeongezeka; hivi linaongezekea wapi? Huko linakoongezeka linakwenda wapi; maana mnajisifu hapa pesa zinaongezeka lakini huko ambako zilitakiwa ziende haziendi?

Sasa tuambieni zimeongezeka lakini zimekwenda wapi ili na sisi tuwe na majibu ya kuwaambia wananchi jamani zilikuwa zije hapa, lakini Serikali imezipoleka mahali pengine na kwa sababu gani. Kwa kweli inatumiza sana.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye Miradi ya Maji imesimama na hili ni jambo muhimu sana. Leo wananchi wameona wakandarasi wamefanya kazi kwa bidii na wakandarasi wengi wamelipa fedha zao wenyewe mpaka wamezifikisha zile kazi asilimia 70, asilimia 80, wameamua kusimama. Hauwezi kupata maji mtu akifikisha mkandarasi asilimia 70, hata akifikisha asilimia 100. Wakandarasi wamezuia hata kutoa huduma hizi za maji kwa sababu hawajalipwa fedha zao, wameondoa baadhi ya vifaa ili maji yasitoke katika jamii na wananchi wanaona Mradi umekamilika lakini hawajalipwa fedha zao.

Tuna Miradi mingi imekwama, ukienda mfano katika Wilaya yangu ya Bahi, Miradi yote iliyokuwa inatekelezwa katika Kijiji cha Chimendeli, Mkulugano, Mundemu, Chikuluga, Mchito, Nguji na maeneo mengine, yote zimekwama na wote huu umekuwa mzigo wa Mbunge. Unapofanya ziara yako ukifika Wananchi wanataka kujua kwa nini Mradi huu umekwama.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka majibu hapa pamoja na mimi nitakayowapelekea, lakini na wao kwa sababu wanasikiliza vyombo vya habari, wanaona televisheni hizi, mtuambie Serikali lini mtapeleka fedha hizo na Wananchi hao wangependa kunywa maji kabla ya uchaguzi wa tarehe 25 mwaka huu ili na sisi mtuweke salama katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari ya maji mijini. Mji wa Bahi umekuwa na shida ya maji kwa muda mrefu na nimelalamika hapa mara nyingi sana. Mji ule umegeuzwa kuwa wilaya na tumepeleka pale Makao Makuu ya Wilaya, miaka mitano sasa imepita. Wananchi wengi wameongezeka kuhamia na huduma zingine, tumepima viwanja pale wananchi wanashindwa kujenga kwa sababu hakuna maji.

Mheshimiwa Spika, tumelalamika sana, ilifika mahali hata nikaomba zile fedha za upembuzi yakinifu kutoka Mradi wa Mbwasa kuja pale Bahi zibadilishwe tupewe katika Mradi wa kutoka Makakatika kwenda Bahi, ambao tayari tumeianza, tumeishiwa fedha na tunahitaji shilingi milioni 400. Humu

humu ndani ya Bunge niliahidiwa kwamba, fedha zile wamekubali Wizara kuzibadilisha matumizi yake, lakini mpaka leo hata senti tano haijaja.

Tumefanya hata mazungumzo na Waziri ofisini kwake na akaahidi fedha hizo zinakuja, lakini hazijaja na ule Mradi umesimama. Mradi ule tulisaidiwa na wafadhili na walikuwa wanajua Serikali itaweka mkono wake. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe majibu ni lini hizo shilingi milioni 400 zitakuja Bahi tukamilishe ule Mradi kwa sababu wananchi wa Bahi hawana maji, maji yaliyopo ni machafu, maji ya chumvi, hayawezi kutumika kabisa kwa maisha ya binadamu na mji sasa umekuwa mkubwa na watu wamekuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, lalamiko langu la kila siku ni umeme katika Wilaya ya Bahi. Kila siku nashangaa hata najiuliza nikiwaona Waheshimiwa Wabunge hapa wanapongeza habari za umeme natamani nikatembelee hata majimbo yao. Hicho wanachosema hapa ni kiini macho au ni kweli! Toka nimekuwa Mbunge miaka mitano inakwisha hakuna hata kijiji kimoja kilichowaka umeme Bahi, lakini nina miaka miwili nyuma takribani miaka saba! Hili jambo hatuwatendei haki Wananchi wa Bahi. (Makofi)

Nataka nishukuru juhudi za Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya kuona malalamiko yangu hapa amejitahidi tumekwenda naye mpaka kwa wahusika na ametoa maagizo, hata yeye alipoletewa orodha ile ya wilaya mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma, akashangaa kuona wilaya moja inapewa vijiji 54 lakini Wilaya ya Bahi haina kitu kama vile haipo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa pia hivi karibuni alifanya ziara kwenye wilaya yangu na yeye akayaona matatizo ya Bahi na akawaahidi Wananchi wenzangu katika Vijiji vya Mtita, Nhome, Msimburi, Mpamantwa na Kigwe kwamba, angalau mpaka mwezi wa saba na mwezi wa tisa umeme utawaka. Mwezi wa saba huu hapa kesho kutwa, sijaona chochote kinachoendelea. Kwa hiyo, naomba na hapa nipate majibu sasa ili yasiwe majibu yangu mimi tu, mwenzenu nitanyolewa kule kavu kavu kwa sababu ya hii Miradi ya Umeme ambayo haijii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sana nipate majibu ya kuonyesha. Mheshimiwa Malima anacheka kwa sababu alikuja wilayani kwangu kuona wakati huo akiwa Naibu Waziri, mpaka sasa sina umeme. Naomba sana, Miradi ya REA imenitenga, Miradi ya MCC katika vijiji 17 wanavyopewa wilaya zingine Bahi unapewa kijiji kimoja, mpaka Wananchi wanasema hatuna Mbunge hapa! Kwa hiyo, ukienda Bahi ukiona juhudi za Bahi ukisikia Bahi wanampenda Badwel ni kwa juhudi zake binafsi na pesa yake ya mfukoni, lakini kwa maana ya Serikali pale ime-collapse.

Naomba majibu ya kutosha juu ya Bahi; ni kitu gani ambacho kinafanya hii Bahi ionewe?

Ukienda kwenye minara ya simu Bahi ya mwisho, ukienda kwenye umeme Bahi ya mwisho, ukienda kwenye Miradi ya Maji Bahi ya mwisho, kila kitu Bahi ya mwisho! Kwa kweli jambo hili haliridhishi na wananchi wa Bahi wamechoka wanataka na wao waone wanakuwa wa mwanzo katika Miradi mbalimbali na upangaji wa Miradi ya Serikali. *(Makofi)*

Ukienda zahanati, mmetuhimiza hapa kujenga zahanati katika kila kijiji, tumezikamilisha, tuna zahanati pale Chali Makulu, Mpinga, lakini zahanati zile kufunguliwa nayo pia imekuwa kizungumkuti. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Wilaya ya Bahi ninayo masikitiko sana, naomba majibu na siungi mkono hoja hii. Siwezi kukaa hapa kwa miaka mitano Wananchi wanaona hawana maendeleo lakini Mbunge wao nasimama hapa naunga mkono hoja. Sasa unaunga mkono hoja ipi? Unga mkono hoja ambayo unaona italeti maendeleo ya wananchi wako na siyo kuunga mkono hoja ambayo haipeleki maendeleo kwa wananchi wako. *(Makofi)*

Sina cha kujisifia kule Bahi, kila kitu ambacho kilitakiwa kufanyika Bahi kimesimama. Siwezi kuunga mkono hoja hii mpaka nisikie majibu ya Bahi na sisi katika hii miezi kadhaa iliyobaki, kunafanywa utatuzi wa Miradi ya Maendeleo ya Bahi iliyokwama.

Mheshimiwa Spika, mgao wa vijiji; katika Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Bahi ndiyo iliomba vijiji vichache kuliko Wilaya yote katika Mkoa wa Dodoma, lakini ndiyo imekwenda kupewa vijiji vichache kuliko wilaya yoyote; hivi kwa nini? Nimemlalamikia Waziri Mkuu, nimemwandikia barua, akaniambia unajua sababu kubwa huku ilikuwa Dodoma Vijijini sasa bado naona kuna taasisi zingine zinaihesabu kama Dodoma Vijijini, wakigawa vijiji wakigawa nini kumbe vingine unakuta vimekwenda Wilaya ya Chamwino kuliko Bahi. Hivi mpaka leo Serikali haijajua kwamba kuna Wilaya ya Bahi?

Sasa nawaambia kuna Wilaya ya Bahi na mmeigawa ninyi wenyewe, itendeeni haki kama mnavyozitendea haki wilaya zingine. Nataka Wilaya ya Bahi itendewe haki ili Wananchi wale wapate huduma kama wanavyopata wilaya zingine. Kama mlikuwa hamjui kuwa ipo sasa ipo. Wilaya ya Bahi kilomita 56 kutoka hapa Dodoma Mjini, kama kuna watu hawajawahi kuona twende nao kesho au kesho kutwa wakaone kwamba Wilaya ya Bahi ipo, lakini siyo kufanya hivi ambavyo inafanywa kwa Wilaya yangu ya Bahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa njaa na katika Mikoa ambayo inahesabiwa imepigwa na ukame ni pamoja na Mkoa wa Dodoma na Wilaya yangu ya Bahi. Nataka nirudie hapo hapo, nimekwenda mpaka Ofisi ya

Waziri Mkuu (Maafa), lakini nilipofika nikaambiwa Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Mpwapwa na Wilaya ya Kongwa wameleta takwimu, lakini Wilaya ya Bahi haionyeshi hapa kama ina njaa. Hivi mnataka kuwaua Watu wa Bahi? Maana sasa mmewachukia hamuwapi Miradi ya Umeme, Miradi ya Maji, sasa na njaa pia mnasema hawapo?

Nashukuru baada ya kulalamika Ofisi ya Waziri Mkuu imetuletea tani mia tatu za kuanzia, kwa hiyo, naamini na hiyo tathmini waliyosema watakuja kuifanya waje waifanye. Tumbo lenye halina masikio, mimi kule napita nawaambia Wananchi kuwa, Waziri Mkuu Ofisi yake imeahidi mwezi huu wa sita wataleta tathmini, hawangoji tathmini wanataka kuona chakula kinakuja ili wananchi wakomboke. Sasa hivi wako watu wanalala na njaa, wako watu wanakula vyakula vya ajabu katika Wilaya ya Bahi, naomba Serikali hii ijue na kwa kweli tuna hali mbaya sana ya chakula katika Wilaya yangu ya Bahi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana. (Makofi)

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi hii niweze kuchangia bajeti hii kwa siku ya leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu, kuweza kuichangia bajeti ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa pole kwa wale waliopata msiba hasa familia ya Sheikh wetu, Sheikh Simba na wale waliopata ajali za gari, ndugu zetu wengi sana wamepoteza maisha kule maeneo ya Mufindi, lakini tuungane nao katika misiba hiyo na majonzi mazito.

Nisiwe mwingi wa kukosa shukrani, nawashukuru Viongozi wangu wa Chama, kuweza kunichagua na kuwa Mbunge wao Mwakilishi katika Mkoa huu wa Dodoma hasa katika Wilaya ya Kondo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mwenyekiti wangu wa Taifa, kwa kuchaguliwa tena awamu hii kuweza kushika kinyang'anyiro cha kuwa Rais ndani ya Chama. Akipata baraka zake ndani ya UKAWA, anaweza akaongoza au atakayepatikana yeyote tutamuunga mkono ili awe Rais wetu katika UKAWA. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kuchangia. Nije na suala la pensheni ya wastaafu kwa wazee. Hili suala ni kilio cha muda mrefu katika nchi yetu. Napenda kujua Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje na majibu ni kitu gani kinachosababisha wazee hawa kutokupata haki zao kwa muda mwafaka?

Kwa kuwa wazee hawa tayari wameshaitumikia nchi hii kwa muda mrefu, wana haki sasa hivi wapumzike na wapate stahili zao bila tena ya kuanza kupata shuruba za kuweza kujilazimisha kutafuta haki yao. Leo hii imefikia hatua ya kuwadhihaki na kuwapatia fedha ambazo ni kidogo mno. Mmeongeza hadi shilingi 85,000, sawa na asilimia 70, ukitafsiri hapo ina maana kwa siku nzima mtu atapata mlo mmoja kwa shilingi 2800.

Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje na majibu mazuri. Sisi ni Wabunge, dada yangu, sikuonei nakupenda sana, lakini hao ulionao humo karibu yako hao wazee hao, naona hawawatendei haki wazee wenzao na uzee unakuja huo baba hauendi mbali. Hebu tuangalie, hivi kweli kwa siku sisi tunatumia hela kama hiyo! Sasa hivi thamani ya fedha jamani imekwishapanda na dola imeshaongezeka. Ikiongezeka tu dola, tayari huko madukani kumeongezeka kila kitu, uchumi umekuwa tofauti na ilivyokuwa. Hebu ningepomba muwafikishie angalau hata iwe 150,000/=, waweze kujisikia wako katika nchi yao, wametumikia kwa muda mrefu na wametoa jasho lao wamechangia mchango mkubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nihame katika suala la pensheni kwa wazee, nije kwenye Mifuko hii ya Jamii ya pensheni kwa watu wote. Mifuko hii imekuwa haichangiwi kama inavyotakiwa hasa wale waajiri binafsi, hawapeleki michango kwa wakati. Inawadhaliisha sana vijana wetu na vijana wetu. Kuna vijana ambao sasa hivi wana madai makubwa katika hizi kampuni za barabara, wanaletwa hapa kwa mikataba ambayo hawaitambui mikataba ile wanadanganywa, mwazo inakuwa sahihi lakini baadaye inakuwa tofauti. Serikali pia inatambua kwamba, vijana hawa wamo katika mikataba hiyo na wanastahili wapate fedha zao kama inavyostahili kima cha chini laki tatu angalau na nusu, lakini leo hii utakuta wanapewa laki mbili na sabini au laki mbili, mtu kashinda mchana kutwa katikati ya barabara anatengeneza barabara.

Tuwaangalie vijana wetu wa Jambo Plastic walilalamika mpaka kufikia katika Bunge. Zaidi ya vijana 400 wanadai pensheni zao, lakini leo hii haki zao zimedhulumiwa, mabilioni ya fedha na Serikali inatambua hilo. Tunawatetea watu wa kuja kuliko watoto wetu wazawa walioko ndani mwetu.

Mheshimiwa Spika, nije ajira kwa vijana. Ajira kwa vijana ni kipaumbele kwa nchi yetu ya Tanzania na ni nguvu kazi. Kuwa na vijana wenye nguvu, ambao wanapata mlo kamili, wenye matumaini ya kuamka leo na kesho, lakini siyo vijana ambao wanalala leo wanaamka kesho wapange kitu gani cha kufanya. Hii inasababisha wingu kubwa la vijana wetu kuingia vichakani na kuanza kufanya maasi mabaya, nchi inaharibika, nchi inakuwa siyo nzuri. Wao ndiyo wanakuwa wakaribishaji wakubwa hususan kule mipakani.

Mheshimiwa Spika, ndani ya mipaka yetu siyo salama. Tulishazungumza ndani ya mipaka yetu siyo salama, watu wakubali wakatae, hakuna usalama wowote. Kungekuwa na usalama wasingekuwa wanaingia wakimbizi mpaka katikati ya Mji ambao una dhana ya kuwa Mji Mkuu Dodoma. Wanafika katika nchi yetu hii, hakuna usalama! Mipaka mingapi? Maeneo mangapi? Mageti mangapi wanafika au yale mageti ni ya kuzuia mazao ya mahindi? Wakulima walime kwa nguvu zao, hawana masoko, lakini wakitoa tu pale tayari wanachajiwa hela, lakini vinavyopitishwa mle kama binadamu hakuna vitu kama hivyo kuangaliwa. Hebu turudishe katika Sekta ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, tukiwaenzi walinzi wetu wa amani ndani ya mipaka yetu, ndani ya vituo vyetu na ndani ya maeneo ya magereza yetu, hakika tutakuwa tumeimarika na tumelinda nchi yetu, hata sisi hapa tulipo tusingesimama leo kuongea kuipinga bajeti hii. Bajeti imekuwa ni ndogo, bajeti haikuzingatia zaidi kipaumbele cha hali ya sasa hivi ya uchumi tulionao.

Mheshimiwa Spika, kupandisha tozo ya mafuta ni kuwaangamiza Wananchi walioko vijijini. Hatujawatengea bado nishati mbadala, leo tumekwishakupanga tozo ya mafuta. Mkulima anahangaika apate wapi fedha hiyo, hana mtu wa kumsimamia, lakini anajikuta anauza mazao yake kwa bei ya chini, sukari anakuta bei juu, mafuta anakuta bei juu, akitaka kusafiri bei juu. Tayari gharama za usafiri zimekwishaongezeka mara mbili kabla hata ya tozo hiyo ya mafuta haijaingia. Hebu tuwaangalie wananchi wetu, tuna mawingu makubwa ya wananchi wanaotutegemea. Kundi la wafanyakazi wanajitegemea wenyewe, lakini kuna wingu kubwa la wakulima, ni wengi mno. Sasa kama hatukuwaangalia, hatukuwatengea ajira nzuri, kweli itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye Sekta ya Ajira Binafsi. Mheshimiwa Waziri, labda leo ningeseema tungekuja na bajeti mpya ambayo ingeweza kutuumiza kichwa katika Bunge hili tungekaa tunajadili bajeti iliyokuja mbele yetu. Hakuna kitu, kimerembwa kile kile, bajeti imejirejesha ileile. Hebu tuzingatie masuala mengine, tuangalie bajeti hii jinsi ilivyojipanga. Kweli nchi yetu ya Tanzania tuna bandari ambayo ni uvuvi, tuna maziwa ni uvuvi, tuna mito, mabonde, milima, misitu ni utalii na tuna mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, tungepanga vizuri taratibu za kuweza kuwapangia kazi vijana hawa, wangeweza kujichomeka maeneo yote haya na kazi zingefanyika. Tungefungua viwanda vya nyama, mbao na viwanda mbalimbali, hakika tungeweza kupata uchumi mkubwa na vijana wangepata ajira hapahapa nchini na wasingenda nchi za nje kudhalilika kule kama wanavyodhalilika sasa hivi. Hii yote ni kukosa ajira katika nchi yao Tanzania. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, turudishe viwanda vipya, turudishe mashirika ya

umma, vijana wetu waliosoma waweze kubaki hapa hapa kwetu Tanzania na kuweza kuitumikia nchi hii kuliko kwenda nchi nyingine za jirani.

Mheshimiwa Spika, tuangalie suala la kilimo. Tunasema tuna kilimo, tuna ardhi. Ardhi nzuri kweli tunayo tulime mazao yetu na tuweze kupangiwa bei, lakini ardhi hii bado inakuwa na migogoro maeneo mengi hawana uhuru na ardhi hii katika nchi yao. Hebu ongezeni hela katika sekta hizi ambazo ni muhimu hasa Sekta ya Ardhi waweze kupima mipaka haraka na waweze kuboresha kilimo ili angalau wakulima hawa sasa hivi wakatengewa bei za biashara zao za mafuta, tuna matunda. Leo hii tumeona hapa Dodoma watu wanalima zabibu, tuna mapera, tuna nini, lakini hawana masoko ya aina yoyote ya kupeleka, hakuna biashara wala viwanda. Tunategemea kitu gani katika nchi yetu hii ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wanakuja kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania, tuwape muda mfupi ili dola ikiongezeka na sisi tuwaongeze. Tusiwape miaka 30, leo dola imeongezeka mara ngapi tuambieni ukweli?

Dola imeongezeka lakini wawekezaji tumewapa kwa bei ndogo, angalau tungewapa hata kwa muda wa miaka mitano mitano, dola ikiongezeka na wao tunawaongezea ili tuweze kupata faida tuendane na wakati. Hii kwa kweli inatumiza sana.

Mheshimiwa Spika, nirudi katika sekta nyingine ambayo ni ngumu zaidi, Sekta ya Maliasili. Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri amsimamie huyu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kule Maliasili wanatufanyia sivyoo, wananchi wetu wanapata tabu sana, mnawanyanyasa wananchi na huu ni wakati wa njaa. Njaa imeanza hakuna cha kuwasaidia wananchi, ardhi mnawanyang'anya waende wapi? Mapori mnaongeza, wananchi wanaongezeka!

Naomba Maliasili na Utalii warudishe vizuri mahusiano yao na ardhi ili waweze kututengea maeneo ya kulima hasa kule Kondoza Mkungunero. Warudishe pia yule twiga mwuepe anaitwa kijana. Ndege zinatua kila siku pale jioni zinafuata nini?

Tusiwe tunafichana tuelezane ukweli, kuna twiga alikuwa anang'aa kweli kweli pale, ukiingia kwenye lile eneo unamkuta, lakini wakamsogeza kule halafu wakadanganya wananchi wakaanza kusogeza mipaka. Hii kwa kweli halleti maana nzuri katika nchi, wananchi walikuwa wana ushirikiano mzuri katika eneo lile, mmwabana mpaka leo hii wameingia katika mgogoro mkubwa wa ardhi; waende wapi?

Leo hii watu wanachomewa mazao yao pale, wanachomewa mahindi yao, wanachomewa vyakula vyao kila siku na ushahidi na barua kila kitu ninazo ziko hapa. Hivi kweli hawa wananchi hawana thamani katika nchi yao? Kila sehemu kuna mgogoro; Morogoro, Kilosa, Simanjiro, huko wapi!

Mheshimiwa Spika, ni hali ngumu sana katika nchi yetu, tusipojidhibiti sisi wenyewe, kwa kweli hatutatafuta mchawi, mchawi ni sisi wenyewe. Kama tukiona wenzetu sehemu zingine wananyolewa na sisi tuanze kutia za kwetu maji, sababu tunataka sisi wenyewe.

UKAWA safari hii lazima ichukue madaraka na lazima tuchukue kwa sababu leo hii wanakuja na sekta tofauti tofauti na maneno. Tulitegemea zile hela za watu wote walizoziba, leo hii zingerejeshwa hapa, hakuna Mtanzania ambaye angedaiwa hizi shilingi milioni nane na zaidi. Zingelipwa hizi hela zote na zile hela. Wale watu leo hii wameshitakiwa na kama wameshashtakiwa zile hela zimerudishwa Serikalini ili zitolewe migawanyo katika wilaya zetu wananchi wanufaike?

Tusitegemee misaada kutoka nje, tunaambiwa leo tuna deni kubwa ajabu la Taifa; kwa nini hizi fedha zilizokusanywa rundo zima pale watu wakaenda wakabeba na viroba na magunia zisichukuliwe zikaenda zikalipa kule?

Tunangoja kuwadai Wananchi kwa kuwaongezea tozo na kodi na tunasimama hapa mbele tunatanguliza makofi na wangine wanajichetua kusema hiki ndiyo chama ambacho kitaongoza, kumbe kinawafanyia watu utapeli mkubwa. Hii ni aibu sana kufanya vitu kama hivyo. Wanagombea wao Kiti cha Urais, Wagombea Urais kama utitiri, wamejaa chekecheke kila sehemu, ni hela hizo hizo za watu. Rudisheni hela za Escrow, msijidanganye kuweka Marais karibu 20, 30, hatuhitaji hilo. Rais makini lazima niwaambie ndugu zangu Wananchi, atatoka UKAWA tu! (Kicheko)

Naomba ifikapo tarehe 25 Oktoba, wananchi kwanza sasa hivi wajiandikishe kwa wingi sana. Natoa wito kwa Watanzania wote na kwa wananchi wote wa Kondo, wajiandikishe kwa wingi mno ili kuweza kumchagua Kiongozi aliyekuwa makini, mwenye sifa zenye uwezo, mwadilifu, Mcha Mungu, mwajibikaji, mchumi, mpenda amani. Tusipende kukumbatia vitu ambavyo tunaona vina athari mbele yetu halafu tunabaki tunasifia, hebu tuache sifa za Kidigo. (Makofi)

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*



**SPIKA:** Haya dakika kumi na tano, watu wakishindwa vya kusema wanaanza sasa kuogelea baharini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Kangi Lugola, atafuatia Mheshimiwa Agness Hokororo!

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nyeti ambayo itanipa nafasi ya kujadili Bajeti ya Serikali. Nianze na kunukuu kwenye *Hansard* ya tarehe 4 Juni, wakati Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Charles Mwijage anajibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, alimalizia kwa maneno haya: “Kwa hiyo, Mtendaji yeyote wa Serikali anayekiuka kusimamia agizo hilo, hii ofisi haimfai. Kwa hiyo, Serikali haijabadilisha ni hivyo, ukiona Mtendaji, Mkurugenzi wa Halmashauri anaruhusu ukiukwaji huo, ofisi hiyo haimfai na mumzomee.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wawepo Watendaji na Mawaziri ambao kwa kauli hii ya Serikali ya Mheshimiwa Mwijage, nitakwenda kuwazomea.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Mwibara, kwa sababu huu ni mchango wangu wa mwisho kwenye bajeti. Waliniamini wakanichagua kuwa Mbunge wao na wao wanajua tulivyoshirikiana nao, nawashukuru kwa kunipa ushirikiano. Tumejenga Mwibara yetu imekuwa Mwibara mpya. Zaidi ya miaka hamsini leo tunaongea tukiwa na Mwibara ambayo ni mpya kabisa. Nawashukuru sana, lakini nawaomba wasisahau kila wakati kusema ile kauli mbiu yao ya kwamba; “Mwibara bila Kangi Mwana wa Lugola haiwezekani.” Nawakumbusha wasiisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu nilivyoanza Bunge hili, hakuna siku ambayo niliwahi kuunga mkono Bajeti ya Serikali. Kwa mara ya kwanza leo nakwenda kuunga mkono Bajeti ya Serikali na ninazo sababu za msingi kwa nini naunga mkono Bajeti ya Serikali. Sababu iliyokuwa inanifanya nikatae Bajeti ya Serikali ni kuwa bajeti ya vinywaji, sigara, vileo, pombe, nikawaambia bajeti ya namna hii haitatuondoa mahali tulipo. Leo kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, tumepata bajeti ambayo haikuegemea kwenye pombe, sigara, soda na vinywaji. *(Makofi)*

Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuya Saada na Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu na Manaibu wao na Watendaji wote, kwa kuweza kutekeleza hili kwamba sasa tutakuwa na bajeti isiyo ya vinywaji pamoja na sigara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili, zaidi ya miaka hamsini wamepita Mawaziri na Mawaziri, baada ya Saada Mkuya kuingia hapo na Mawaziri wenzake, kwa mara ya kwanza, Jimbo la Mwibara wameweza kumpa Magufuli,

Waziri wa Ujenzi, fedha za kujenga barabara ya lami kilomita 51. Kwa niaba ya Wanamwibara nina kila sababu ya kuwapongeza Waziri pamoja na wenzake. Kwa mara nyingine tena zaidi ya miaka 55, baada ya kuwapata Mawaziri hawa, wameweza kumpa fedha Waziri wa Nishati na Madini, Simbachawene, leo anasambaza umeme vijiji 48 vya Jimbo la Mwibara. Nina kila sababu ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na eneo ambako Wananchi wamepata tabu hakuna kivuko, Kwiramba kwenda Majita, lakini Waziri huyu aliweza kumpa fedha Mheshimiwa Magufuli na leo kuna pantoni Wananchi wanavuka kwa shilingi 500. Nani kama Saada Mkuya pamoja na Mawaziri wenzake. *(Makofi)*

Nimegundua siyo lazima uwe Profesa ili uweze kufanya mambo haya na nimegundua siyo lazima uwe mwanaume ili uweze kufanya mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, kwa mara nyingine tena Wazee wetu walikuwa wanahangaika, leo tumeona Wizara imeweza kupandisha pensheni yao. Wazee hawa walikuwa wanatufia kwa sababu ya kuhangaika na pensheni zao. Naamini sasa wataongeza umri wa kuishi, waendeleo kutupa hekima na busara.

Mheshimiwa Spika, hii tozo inayogomewa ya nishati, kupandisha bei ya mafuta, tulipoanza wakati ule kusema REA tuwapatie fedha, naamini wananchi wameona kwenye vijiji mbalimbali na Mawaziri hapa ni mashahidi; vijiji sasa vinakwenda kupata umeme. Hizi fedha za tozo hizi ni kweli wananchi wanasema wanaumia na mimi niseme huwezi kupata kitu kizuri bila kumia upande mwingine na ndiyo maana leo tunapojenga barabara ya lami pale Mwibara, Wananchi walikuwa wanaililia barabara ya lami, sasa hivi wanaona inajengwa wanaanza kuniambia Mbunge usisahau kuwaambia watuwekee na matatu kwa sababu watu wengi watakufa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kitu kizuri kikija kina madhara tena kwa uhai wa mwanadamu. Kwa hiyo, nawapongeza ili Wanamwibara mwezi wa sita waendeleo kuona umeme unawashwa, hizi fedha zitoke haraka tuweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa nianze kuzungumzia mambo ambayo katika bajeti hii tusipoyatafutia ufumbuzi, Taifa hili litaendelea kuangamia. Nianze na la kwanza kabisa la kuporomoka kwa thamani ya Sarafu yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, leo tunatumia sh. 2,075 kununua Dola moja ya Kimarekani na maisha yanazidi kuwa magumu kwa sababu ya kuporomoka kwa thamani ya sarafu. Kwa nini jambo hili linatokea? Upande mmoja wa jambo hili kutokea, ambalo nitashauri Serikali, waache porojo wale wenye dhamana kwenye Wizara ambazo zitatua suala ninaloenda kulisema sasa, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa dampo la bidhaa nyingi utitiri, ambazo sisi wenyewe tunaweza tukazizalisha. Tunapokuwa na bidhaa nyingi kutoka nje utitiri, tunalazimika kuisaka Dola ya Marekani kila kona. Kitendo cha kuwa na mahitaji makubwa ya dola ni kuifanya shilingi yetu iweze kuporomoka kushuka thamani.

Waziri wa Viwanda na Biashara, tangu nimeingia Bunge hili, zimekuwa ni porojo tutajenga viwanda. Mheshimiwa Zamboni hapa leo wakati anajibu swali kuhusu sukari na yeye ameendelea kutudanganya hapa mchana kweupe kwamba, eti mtajenga viwanda. Zaidi ya miaka 55 tulijenga viwanda mmeuza leo havipo. Leo unatuambia unakwenda kujenga viwanda vya sukari; huu ni uongo! Leo mnaagiza tani 290,000, tunahitaji dola nyingi sana kwa ajili ya kuagiza sukari kotoka nje. Hii inaongeza kuporomoka kwa thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati nakwenda kumshauri Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Kigoda, leo nimelazimika kuja na *semi-trailer*, ambalo lina bidhaa mbalimbali sampuli 602. Kwa bahati mbaya nimeliacha nje *semi-trailer* haliwezi kungia humu ndani, lakini nimepakua baadhi ya bidhaa ambazo nataka kuzionyesha Bungeni na ziwe sehemu ya *Hansard* yako. Naomba nizimwage hizi bidhaa hapa. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Aaah, hapa tunaongea hatuleti bidhaa, bidhaa zinapelekwa kwenye maonyesho kule. Unapewa nafasi ya kufanya hivyo kwenye viwanja, siyo hapa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, bidhaa ambazo zinasababisha shilingi inaporomoka ambazo tunaziagiza badala ya kuzizalisha hapa, mojawapo ni hili dodoki la kuogea, ambalo tumeliagiza kutoka China. Kuna socks hapa ambazo tumezitoa Marekani, tungeweza kuzizalisha hapa. Tuna kitambaa cha mkononi (*handkerchief*), tumetoa Uchina tungeweza kuzizalisha hapa nchini. Kuna chaki tumzitoa Kenya pamoja na China tungeweza kuzizalisha hapa nchini. Tuna peremende ambazo tumepewa hapa tunatafuna tumezitoa Kenya tungeweza kuzizalisha hapa nchini. Tuna nyembe tumezitoa China tungeweza kuzizalisha hapa nchini. Tuna vipamba vya kutolea uchafu kwenye masikio tumevitoa China tungeweza kuvizalisha hapa nchini. (*Kicheko*)

Tuna *toothpicks*, vitu vya kutolea mabaki kwenye meno, tumevitia China tungeweza kuvizalisha hapa nchini. Aibu kubwa, tuna *chewing gum* tumetoa China tungeweza kuzalisha hapa nchini. Tuna kiberiti, tumeagiza Kenya, kiberiti, tungeweza kuzalisha hapa nchini. Tuna *ruler* tumeitoa China tungeweza kuizalisha hapa nchini. Tuna *pencil* tungeweza kuzalisha hapa nchini. Vinoleo vya kalamu, *note book* na mambo mengine. (Kicheko/Makofi)

Tumekuwa tukisema maneno haya pasipo kuleta vitu hivi na kuwaonyesha hawa hawatuelewi, hawatusikii. Inaumiza sana, tunakuwa na Wizara ya Viwanda, viwanda vililizwa, kila siku tunatenga bajeti hapa tufufue viwanda, tujenge viwanda, hakuna kiwanda hata kimoja! Leo mwananchi wa chini anaumia kwa sababu ya kuporomoka kwa shilingi. Mungu wangu, wananchi hawa wanaangamia na wanaangamia kwa sababu tumekuwa na maneno mengi ambayo hatuyafanyii kazi.

Mheshimiwa Spika, naiomba sasa Serikali na hasa Serikali ijayo, wahakikishe viwanda vinaoteshwa hapa nchini, ili tuweze kudhibiti kuporomoka kwa sarafu yetu. Vinginevyo, tukiendelea kununua vitu nje, Wananchi wetu wanaendelea kuumia.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la maji. Zaidi ya miaka 55 ya Uhuru, tuna Miradi ya Maji kule maji hayatoki. Mradi wa Nyabehu, nitaendelea kusema, wanadanganya kwamba maji yanatoka, maji ya Nyabehu wakati hayatoki. Buzimbwe, Buramba na Mwiseni, hawapati maji na Mradi huu unapeleka maji Bunda. Alipokuja Waziri Mkuu, walienda kuchota maji kwa kutumia punda, wakaenda kumwaga kwenye *tank* na kumwambia Waziri Mkuu maji yanatoka, wakati Mradi ule haujakamilika na hautoi maji! Hii ni aibu kubwa na sasa wapo watu wanatafuta Urais pale, maji yale yameshindikana zaidi ya miaka 55; kitu gani hiki?

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la chakula. Wananchi wa Mwibara hawana chakula, lakini tunatenga fedha nyingi kila mwaka na maghala ya hifadhi ya chakula yana chakula kingi, tunaomba sasa wananchi wale wanakufa, chakula kile kianze kusafirishwa kiende kwa Wanamwibara, ili wasije wakafa halafu nikakosa watu wa kunipigia kura. Vinginevyo, watangaze Jimbo la Mwibara kwa kuwa wapiga kura wamekufa, maana mimi nitakuwa niko huku Dodoma sijaenda kule, nije bila kupingwa kwa sababu hakuna watu wa kupiga kura. (Kicheko)

Niende kwenye posho ya askari polisi. Tangu marehemu Mgimwa akiwa hapa, tuliweza kupandisha posho ya askari polisi kutoka shilingi 6,000 kwenda 8,000. Zaidi ya miaka miwili, lakini hawalipwi posho hii; kuna kigugumizi gani? Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, leo usipotuongua utakapokuja kuhitimisha

hapa suala hili linakuhusu na wengine ndiyo hao sijui nasikia mnagombea Urais, umeshindwa kutetea posho ya Wizara moja tu ya Polisi, leo utatetea posho za Wizara chungu mzima?

Mheshimiwa Spika, inatia aibu na hawa ndiyo Mheshimiwa Mwijage ulikuwa unasema, wanaoshindwa kusimamia Wizara yao, wanashindwa kusimamia Sheria ya Matumizi ya Fedha, tumetunga hapa, wanashindwa kupeleka posho kwa askari, hawa ndiyo wanastahili kuzomewa.

*(Hapa Mhe. Alphaxard K. N. Lugola alizomea)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Tunawazomea watu kama hawa na wewe ulitoa kauli hapa tuwazomee na hatutaacha kuwazomea, posho hizi ziende. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye usajili wa leseni ya udereva na usajili wa bodaboda. Mheshimiwa Mkuya, nimekupongeza hapa, haiwezekani zaidi ya miaka 55 ya Uhuru, Mwananchi anatoka Kisorya, kilomita 150, anakwenda Musoma Mjini kwa ajili ya kwenda kubadilisha usajili wa pikipiki, ni aibu! Anatoka Kisorya kilomita 150, anakwenda kupata leseni yake ya udereva Musoma, ni aibu.

Mheshimiwa Spika, naomba jambo hili, Wananchi wetu waendeleo kuwa na unafuu wa masiha, wanachoma mafuta kutoka Kisorya zaidi ya kilomita 150, waletewe karibu. Kama kila Wilaya ina TRA; mliziweka za kazi gani? Ndiyo kazi yake sasa ya kuwahudumia wananchi ambao wako karibu na maeneo hayo.

Masilahi ya Walimu; Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, alitupatia Walimu ambao kwa miaka mingi tulikuwa tunawahitaji, lakini Walimu hawa walitelekezwa, wako mashuleni, hawana mishahara, hawakupata posho. Wanaanza kuwasumbua Wabunge ili waweze kujikimu; ni aibu! Kama mlikuwa hamjafika muda wa kupeleka Walimu, mlikuwa mnawapeleka kwenda kuwatesa!

Mheshimiwa Spika, tunataka maelezo, Walimu waliotuletea kule mpaka sasa hawajapata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kuzomea kungekuwa kama kupiga kigelegele, ingekuwa vizuri, hii kengele ya pili.

Haya, Mheshimwa Hokororo atafuatia Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Batenga ajiandae!

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema. Pili, nawashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Mtwara kupitia Chama changu cha Mapinduzi, kwa kuniamini na kunichagua niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Naamini tumeshirikiana kwa kipindi chote na kwa hakika tumefanya kazi pamoja. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia endapo nitapata ridhaa hiyo tena.

Mheshimiwa Spika, kipekee, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunitua kunipa nafasi ya Ukuu wa Wilaya, ili niweze pia kuwatumikia wananchi ambao ni sehemu ya Tanzania na kwa hakika nitaendelea kutimiza wajibu wangu. Nashukuru pia kwa sababu sasa nimepangiwa Wilaya ya Tunduru, ambako pia ni jirani na Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nikija katika bajeti ya leo, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja. Sote tunatambua kwamba, maendeleo ya nchi yanatokana zaidi na mifumo imara ya kodi na pia wigo mpana wa kodi. Naomba nitumie fursa hii kuishauri Serikali yangu kwamba ni vyema sasa tukapanua wigo wa vyanzo vya mapato kwa Serikali hasa kwa kuimarisha maeneo machache ambayo nimeyaona. Kuimarisha ukusanyaji wa kodi za tozo za majengo, uwindaji na kurasimisha sekta zisizo rasmi, ili nazo ziweze kuchangia katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Kuwawezesha Wananchi kiuchumi, ni Sera ya Chama cha Mapinduzi katika llani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2010 - 2015. Naamini hilo linawezekana, lakini changamoto kubwa tuliyonayo katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi naona ipo katika eneo la mabenki, ambapo kumekuwa na riba kubwa.

Mheshimiwa Spika, naona inawezekana kuwawezesha Wanawake na Vijana na wananchi kwa ujumla kupitia benki, iwapo tu Gavana anaweza akarekebisha kwenye hilo eneo la riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakulima wa korosho, ufuta, choroko, mbaazi na mazao mengine ambayo yanalimwa katika Mkoa wa Mtwara na Tanzania kwa ujumla na inafahamika kwamba, wanawake wa Tanzania, ambao ndiyo walio wengi, asilimia 51 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, ndiyo hasa *engine*

ya uzalishaji katika nchi yetu. Wanatamani sana na wao waweze kuchukua mikopo ya kuwasaidia kuendeleza sekta mbalimbali ambazo wamekuwa wakizifanyia kazi kama vile ufugaji, kilimo na maeneo mengine. Changamoto kubwa wanayokutana nayo ni riba kubwa katika benki zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na mambo mengine yanayofanyika ya MKUKUTA, MKURABITA na maeneo mengine na TASAF III ambayo tunaendelea nayo sasa, lakini ipo haja ya Serikali kuangalia eneo hili la riba ili sasa Wakulima wa korosho, ufuta na karanga katika Mkoa wa Mtwara, ambao wanakusudia pia kusindika, waweze kuingia benki na kupata mikopo ya bei nafuu.

Natambua Benki ya NMB ambayo inatoza riba ya asilimia 20, lakini napo pia hiyo ni kubwa, haituwezeshi sisi Wanawake na Vijana ambao tunakusudia kuongeza thamani ya mazao kwa yale ambayo tunayalima, tukaweza kufanya vizuri. Hilo likirekebisha, tunaweza tukachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu na ile Sera tutaiona sasa kwa vitendo, kwa sababu tutaona namna ambavyo wananchi wenyewe watakuwa wanaongeza mapato yao kwa ngazi ya familia, kaya, lakini na kwa jamii kwa ujumla wake.

Sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara, huu uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi tutaona na hasa lile lengo na azma ya Serikali ya kufufua Viwanda vya Korosho ikitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, natambua kwa bajeti zote ambazo nimehudhuria katika Bunge hili na hata katika kikao cha mwisho cha Bunge lako, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anahutubia Bunge, alituahidi wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwamba, vipo viwanda viwili ambavyo Serikali imeangalia na kuona haja ya kufufua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafsi hii, kuiomba sana Serikali kutimiza azma hiyo. Kwa sababu kule nyuma tulikuwa na viwanda vingi vya korosho, Masasi tulikuwa na kiwanda cha korosho, Newala kulikuwa na viwanda viwili vya korosho, Mtama kulikuwa na kiwanda cha korosho, Nachingwea na Tunduru, lakini hivyo vyote sasa hivi havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza mama yangu Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho, kwa jitihada kubwa wanayoifanya kwa kupitia Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho, ambapo sasa wameamua kujenga viwanda Tunduru, Mkuranga na Mtwara. Nikupongeza sana na ninaipongeza Menejimenti ya Mfuko wa Zao la Korosho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, Serikali ilikuwa na nia njema ya kuweka Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ambao kama ungewezeshwa vizuri, ungeweza kusaidia wanawake walio wengi Tanzania hii wakiwemo wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mtiririko wa fedha zinazokwenda katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ambao mimi natambua lengo lake ilikuwa ni kuleta chachu, kuchochea maendeleo na hasa kwa kushirikiana na zile fedha, asilimia tano inayotengwa katika kila halmashauri kwa ajili ya wanawake na asilimia tano kwa ajili ya Vijana, hivyo vyote vingeweza kuchochea maendeleo katika wilaya zetu na katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na 2014/2015, fedha zilizokuwa zimetengwa katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ilikuwa ni bilioni mbili, lakini kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2013, Wizara ilipokea sh. 315,628,846 tu na kile kilichobaki hakijatolewa hadi leo. Kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 haikutoka hata senti moja na hiyo inaashiria lile lengo zuri la Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwenda kuchochea kasi ya maendeleo ya wanawake katika mkoa yetu halitawezekana.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kwamba, pamoja na mambo mengine yote, lakini yale malengo mazuri ambayo tumeyaweka na hasa kupitia Mfuko huu, fedha zake ziweze kutolewa. Tutaona sasa wanawake watakavyokuwa wanachacharika kule watakapopata mikopo kutoka katika halmashauri. Tunajua changamoto kubwa tuliyokuwa nayo, hizi fedha asilimia tano kutoka halmashauri zetu za wilaya hazitengwi. Hazitengwi kwa sababu makusanyo katika kila halmashauri hayafikiwi, malengo hayafikiwi.

Mheshimiwa Spika, niombe pia hapa tuweke *mechanism* nzuri, namna ambavyo fedha hizi asilimia tano za Vijana na za Wanawake zitatengwa, zitolewe, zichanganywe na zile za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, ili ziweze sasa kutoa matokeo chanya kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimesoma Kitabu cha Hotuba ya Waziri, pamoja na mambo mengine, naomba niongee kidogo sana kuhusu ongezeko la mafuta ya taa kama linavyoonekana katika ukurasa wa 54 wa hotuba yake. Ongezeko hili limeonekana kwa mafuta aina zote, lakini niseme tu kwa mafuta ya taa, ongezeko kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 150, likiwa ni sawasawa na shilingi 100, wanasema linafanywa hivyo ili kuondoa uwezekano wa uchakachujaji.

Mheshimiwa Spika, lengo la ongezeko hili ni zuri sana, tumesema kuharakisha usambazaji wa umeme vijijini. Lengo hili sina upinzani nalo ni zuri sana, REA ni nzuri na Waheshimiwa Wabunge hapa hasa wale wa Majimbo



wamesema, wengi katika vijiji vyao wameona namna REA ambavyo inaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, rai yangu hapa, hili ongezeko la shilingi 100, mimi kwa mtazamo wangu linaathiri sana watu wa kipato cha chini. Kwa sababu hiyo ndiyo nishati yao kubwa na sote hapa tukienda kule vijijini, ukiwauliza Wananchi wa kawaida watatu au watano, ungependa kuwa na mambo gani muhimu, la kwanza watasema maji, la pili watasema umeme.

Kwa hiyo, tunajua kabisa maji na umeme ni vitu muhimu katika maendeleo yetu lakini swali la msingi hapa ongezeko hili la tozo kwenye mafuta ni tatizo? Tunaweza tukasema si tatizo lakini ni kwa kiasi gani limeongezeka? Tatizo mimi hii Sh.100 inapokwenda moja kwa moja kwa yule mwananchi wa kipato cha chini naiona ni kubwa. Niombe tuangalie eneo lingine ambalo tunaweza tukachukua fedha hii tukapeleka kwenye eneo lingine napo pia hiyo tozo ikasaidia usambazaji wa umeme vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba naamini Mheshimiwa Waziri hapa pengine kuja na hii ameangalia ile dhana ya kimaendeleo (*development by contradiction*) kwamba huwezi kufanikisha sekta nyingine bila kuathiri sekta nyingine. Hata hivyo, naomba hapa tuangalie eneo lingine ili tuweze kwenda nayo yote sambamba kwa sababu kule kwetu Kijijini Mraushi, Nanyindwa Nanjilini, Hinju, Mkonjwano tunatumia sana mafuta ya taa kuliko maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwenye hili Bunge ambalo sasa tunalimalizia na kwa kipindi kirefu tukiongozwa na Mheshimiwa Jenista tulikuwa tunazungumzia suala la mafao ya wazee. Niipongeze sana Serikali kwa kuja sasa na kutuambia kwamba wakati umefika na wao wametambua mchango mkubwa wa wazee katika nchi yetu. Wamesema kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016, Serikali inatarajia kuanza mandalizi ya kuwezesha. Maandalizi wanayokusudia ni kutunga sheria, kuwatambua na kuweka mfumo wa ulipaji.

Mheshimiwa Spika, mimi niombe, kama ambavyo wenzetu Zanzibar wamesema kabisa itakapofika Julai 1, wataanza kulipa mafao kwa wazee na kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano **imetambua** umuhimu wa wazee na kwa sababu kwa kipindi kirefu tulikuwa tunasema tuangalie vyanzo vya kudumu isije ikatuathiri na mambo mengine mengi, mimi niombe, tuseme kabisa kwa uwazi ni lini sasa tunakusudia kuanza kwa sababu 2015/2016 inaweza ikawa maandalizi tu halafu zoezi hili linaweza likienda 2017/2018. Nashauri tuseme kwa uwazi, je, ni mchakato wa kudumu au utachukua muda gani? Tuwe na muda maalum ili kuwajengea imani wananchi hasa wazee ambao waliendelea kuitumikia nchi hii kwa uaminifu na uhodari mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia maeneo mengine na hasa katika eneo la kuongezwa kwa mafao ya wastaafu, pamoja na kwamba wenzetu wamesema kwamba ongezeko hilo ni dogo lakini Waziri amesema ni asilimia 70 na kwa ukweli wameongeza kutoka Sh.50,000 mpaka Sh. 85,000 na kwa kuwa muda mrefu tulikuwa tunaomba na sasa limewezekana, naamini Serikali bado ina nia njema.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia wakati tunaendelea kutafakari suala hili la wazee, kwa sababu hawa wastaafu pia wengi ni wazee, wale ambao si wazee ni wale ambao labda wanatoka Jeshini kwa sababu wanastaafu kwa mujibu wa sheria zao, unaweza usiwe mzee lakini kwa vyeo na taratibu zao unaweza kuwa unastaafu. Kwa kiasi kikubwa, mafao haya ya wastaafu na mafao ya wazee yanayotarajiwa kutolewa na Serikali ni uwezeshaji huo wa wananchi kwenye eneo hilo kiuchumi kama ambavyo tumekuwa tukifanya vizuri katika huu mpango wa *TASAF III*.

Mheshimiwa Spika, tumeona namna ambavyo wazee katika maeneo mbalimbali wanavyohojiwa wakionesha kwa kiasi gani mpango huu umewasaidia kutoka hali ya awali ambapo wazee wale walikuwa wanashindwa kupata milo mitatu na sasa wameweza lakini tumewaona wazee wengine wenye nguvu wamediriki hata kuwekeza ile fedha ya *TASAF III* kwenye kuku na kwenye maeneo mengine. Hivyo sasa, hata hizi fedha za wastaafu, Sh.85,000 iliyoongezwa sasa na ile ambayo Serikali inakusudia kuwalipa wazee, likifanikiwa hili ndivyo tutakavyokuwa sasa tunapunguza umaskini katika maeneo mengi ya vijijini na hivyo lile swali la kwamba kwa nini uchumi wetu unakua na hauonekani uhalisia wake katika maeneo yetu, tukifanikisha haya ninaamini ukuaji wa uchumi utaonekana kwa uhalisia, kwa vitendo kwa sababu kipato cha mtu mmoja mmoja kitakuwa kinaongezeka na hali halisi ya maisha yatakuwa yanaendelea kuboreka lakini na mazingira ya kila Mtanzania yatakuwa yanaendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo sana bila kumpongeza sana Mheshimiwa Saada Mkuya, Mbunge mwanamke kwa namna ambavyo amebeba jahazi hili tangu alivyoingia na mpaka sasa. Lazima nimpongeze, ukiona Mheshimiwa Kange ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwishakwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Batenga na Mheshimiwa Deo Filikunjombe.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami kama kawaida nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Magogoni kwa ushirikiano wao walionipa kwa kipindi chote cha miaka minne na nusu na

namalizia sasa hivi wakiwa nami bado. Naomba niseme kwamba kwa watu wa Magogoni muhimu zaidi ni Mbunge atakayetokana na Chama cha Wananchi (CUF) na si lazima labda awe Hamad.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa mchango wangu kwa kusema kidogo yaliyotokea jana hapa wakati dada yangu Mheshimiwa Madabida alipopata nafasi ya kuchangia. Alisema kwa tabasamu sana na kwa hamasa kubwa, alikuwa anashangaa kwamba viongozi tangu mfumo wa vyama vingi vya siasa 1995 na mpaka leo ni haohao katika vyama vinavyounda UKAWA. Naomba nimwambie tu yeye na wenye mawazo kama hayo kwamba hii inathibitisha kwamba watu hawa wanajiamini na wanaaminiwa, wanakubalika katika vyama vyao na kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiangalia upande wa Chama cha Mapinduzi, kama wangukuwa wamepanga foleni kwenye uandikishaji wa daftari wangehitaji kutwa nzima. Watu zaidi ya thelathini wamepanga foleni wote wanahitaji kuwa Rais wa nchi hii kwa nafasi moja. Hii inadhihirisha wazi kwamba ndani ya Chama cha Mapinduzi hakuna mtu anayekubalika kushika nafasi ya kuwa Rais wa nchi hii. Ndiyo maana ni Mawaziri watupu na Naibu wao ambao kwa muda wote wamekuwa wakiisimamia Serikali hii kama viongozi lakini kila Mbunge anayeinuka hapa ana malalamiko kibao juu ya kero na matatizo yalivyo katika Wizara hizo zote. Hii inadhihirisha tu kwamba hakuna mtu ambaye anafaa kuwa kiongozi au kuwa Rais kwa sasa katika Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze mchango wangu kwa nukuu ya babu yangu, Kamanda wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi, Mzee Kingunge Ngombale Mwiru. Babu Kingunge wakati wa Bunge la Katiba kwenye ukumbi wa Msekwa pale alizungumza na waandishi wa habari na akawaambia, nanukuu:-

*“Tunapozungumzia maendeleo si maendeleo ya vitu, ni maendeleo ya watu”, mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hii sasa nizungumzie suala la posho ya wazee. Posho ya wazee ya Sh.85,000 kwa mwezi ambayo kwa siku ni sawa na Sh.2,800 ni wastani wa mzee anayetumia ugoro kununua ugoro tu dukani na kwa wale wanaotumia sigara nyota ni paketi ya sigara nyota tu. Hata akisema ananunua mafuta ya taa ya kupikia kwa sababu kijijini umeme hakuna kama Wabunge mnavyolalamika ni lita moja ya mafuta ya taa ya kuwasha jiko.

Mheshimiwa Spika, huu ni mzaha kwa wazee na wala hii siyo na wala haileti mantiki ya ile dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania kwani hawa wazee si miongoni mwa Watanzania mnavyowaona? Hivi unampa Sh.2,800 kwa kutwa umemsaidia au umemdhiki? Nadhani hii ni dhihaka kwa wazee na kwa sababu wajibu wetu ni kuwashauri japo mmeziba masikio, naomba niseme kwamba wazee hawa basi tungefikiria angalau basi Sh.5,000 kwa siku ili apate huo ugoro, apate na hayo mafuta, atatwanga mahindi yake apike mwenyewe ajisaidie kwa siku.

Mheshimiwa Spika, suala la kiwango cha chini cha mshahara, cha Sh.265,000, kiwango hiki ni sawa na Sh.8,833 na senti kwa siku. Kiwango hiki cha Sh.8,000, amesema kaka yangu Lugola hapa, tangu wakati wa Waziri Marehemu Mgimwa tulikuwa tunapambana kwamba Sh.8,000 angalau apewe askari polisi, huyu ambaye mnamtuma aje kusimamisha maandamano ya wapinzani angalau aende kwenye kioski akajisaidie akiwa kazini, si nyumbani mpaka leo imeshindikana leo mnasema kwamba mnampa mshahara mfanyakazi wa siku nzima hesabu hiyo ya Sh.8,000 msaidie nyumbani kwake, nauli ya kuja kazini na kurudi, huu bado ni uleule mzaha mnaowafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa akili na maarifa waliyo nayo na kwa utu uzima wao wanaelewa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikiwadhihaki kwa muda mrefu. Kwa hiyo, kwa kuwa wana akil, watajua ni nini cha kufanya hapo mbele, *inshallah* katika mwezi Oktoba unaokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie eneo la Zanzibar kule Bagamoyo katika eneo la Makurunge. Wiki iliyopita wakati wa maswali ya kawaida, kwenye swali la kawaida la Mheshimiwa Jaku nilipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza juu ya hekta 20,373 ambazo mliwakodisha wawekezaji au mliwapa wawekezaji. Nikataka kujua Zanzibar kama mhusika mkuu wa eneo hilo amepata kiasi gani au amepewa nini kwa muda wote huo? Kama kawaida ya Mawaziri wa Serikali hii kuyajibu maswali yanayogusa maslahi ya Zanzibar kirahisirahisi tu hivi, Naibu Waziri wa Ardhi akajibu kwamba kwa kuwa Zanzibar tumeungana, fedha iliyopatikana imepelekwa Hazina na kule Hazina Zanzibar tuna sehemu yetu.

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza mimi ni kitu kimoja, zile zetu pamoja na kwamba mnatushikia, zile za kwenu mnashika wenyewe lakini jamani hata zile zetu wenyewe, *per-se*, hizi zetu za Zanzibar mnatushikia jamani ndugu zetu? Nadhani mtakapokuja leo kwa kuwa ni bajeti ya Taifa mtuambie basi Wazanzibari hapa tuna kiasi gani, kiko wapi na mtatupa wenyewe lini, msiendelee kutushikia, haya mengine tuacheni tushike wenyewe, uwezo huo tunao.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Akaunti ya Pamoja kati ya SMZ na SMT. Kwa sababu hii ni mara yangu ya mwisho kuchangia, naomba nisije nikahukumwa kwa kuacha kuisemea Zanzibar juu ya maslahi yake ndani ya Muungano huu hasa kwenye Akaunti hii ya Pamoja. Leo ni mara yangu ya pili tangu niwe Bungeni hapa kuzungumzia juu ya jambo hili. Tangu kuvunjwa kwa *East African* (Jumuiya ya Afrika Mashariki) na tangu tulipozifanya fedha zile tulizozirithi au zilizokuwa mgao kwenye *East African Currency Board*, Zanzibar asilimia 11.5 ilitumika kama mtaji wa kuanzia Benki Kuu. Tulikubaliana kwamba tuwe na Akaunti ya Pamoja kati ya Zanzibar na Tanganyika au kati ya Zanzibar na Muungano.

Mheshimiwa Spika, ni uleule mzaha tu unaondelea. Kwenye kitabu cha Waziri wa Fedha, ukurasa wa 38 – 39, ana maneno ameyasema hapa, naomba kwa ruhusa yako niyanukuu. Amesema mengi lakini naanzia hapa aliposema kwamba:-

*“Aidha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mfumo bora wa uhusiano wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) umeandaliwa na upo katika hatua ya maamuzi. Maamuzi ya Serikali kuhusu waraka huu ndiyo yatawezesha kufunguliwa kwa akaunti ya pamoja kati ya SMZ na SMT.*

*Vilevile Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha mapendekezo ya kufanya study ya uwekezaji katika mambo ya Muungano”*

Mheshimiwa Spika, ameendelea kusema kwamba:-

*“Katika mwaka wa 2015/2016, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kukamilisha taarifa za study ya uhusiano wa mwenendo wa uchumi na mapato ya Muungano na kuyawasilisha katika pande mbili za Muungano. Aidha, Tume inakusudia kuendelea kufanya study ya uwekezaji kati ya mambo ya Muungano. Study hii inalenga kubaini ushiriki wa pande mbili za Muungano katika uwekezaji kwa mambo ya Muungano”, mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, hivi tangu tulipokubaliana kwamba tuwe na Akaunti ya Pamoja hadi leo, miaka zaidi ya 20 hatujawa na wataalam, hatujaweza kukubaliana au kuridhia kufunguliwa kwa akaunti hii, hivi kuna nini? Kwa nini kila jambo linalogusa maslahi ya Zanzibar linakuwa gumu? Nadhani hapa mtuambie tu kuna siri gani iliyojificha? Tulikubaliana kuwa na Akaunti ya Pamoja kwa sababu, kwanza kuridhishana kwamba kila pande ijue kinacholingia, kilichopo, kinachopatikana. Wasiwasi wangu kwamba hata gawiwo tunalopata, ile *dividend* yetu Wazanzibar bado ni mnavyojisikia tu kwamba labda mtupe kiasi hiki na msipojisikia hamtupi na hata mkitupa hamtupi kwa wakati na wala hatujui hata kiwango chetu ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja awaeleze Wazanzibar jambo hili limekwama nini? Tumekwama kwa sababu gani maana naona ni kwa sababu hakuna nia njema tu. Sisi tunajiita ndugu, tena ndugu wa damu tunakwamaje kukamilisha jambo hili moja dogo na hata kama ni kubwa kwa nini tushindwe mpaka leo? Suala hili msingi wake wa kushindikana ni kukosekana kwa nia njema kutoka kwa ndugu zetu ambao ndiyo mmeshikilia koti hili la Muungano tuseme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake amesema mambo ambayo ni changamoto lakini hivi, kwa muda wote huo, maana changamoto ni yale mambo ambayo tulihitaji tuyafanye lakini tumekwazwa na mambo fulani fulani. Hivi katika suala la kuwepo Akaunti ya Pamoja hallingii hata kwenye changamoto zenu, kwamba mmepata shida na mnaendelea kupambana ili jambo hili likamilike lakini limekuwa gumu? Hivi pia basi hata ile changamoto kwenu haiwi katika sehemu ya changamoto? Hii inazidi kudhihirisha kwamba hakuna nia njema juu ya jambo hili na hakuna hatma njema kwa Zanzibar juu ya haki hizi ambazo zinatokana na uwepo wa Benki Kuu. Kuna mambo mengi yanayopatikana hapa, Wazanzibari tutayajuaje kama hatuko pale ndani. Ndiyo maana labda linakuwa gumu ni kwa sababu ya hiyo nia isiyokuwa njema ya kwamba Wazanzibar waweze kupata haki yao stahiki.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba muda umekuwa mwingi na sitegemei kwamba kutakuwa na miujiza ya hao waliofoleni kuomba urais kwamba atakuja mtu hapo miongoni mwao aseme hili sasa tunalimaliza, inategemea miujiza mikubwa. Nikiwaangalia sura zao hakuna ambaye anaweza akawa na miujiza hiyo, Mwenyezi Mungu mwenyewe tu kadiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niseme nakushukuru kwa kunipa muda huu, hayo ndiyo yalikuwa yangu machache, nilikuwa nina budi niyaseme ili Wazanzibari kule wasije wakaniambia mbona wewe hukusema hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambue watoto waliokuja hapa, wako wanafunzi 70 na walimu wanne kutoka shule ya msingi ya Martin Luther Dodoma, kama wapo wasimame. Ahsante na karibuni sana, msome kwa bidii. (*Makofi*)

Sasa namwita Mheshimiwa Batenga na Mheshimiwa Filikunjombe, Mheshimiwa Christowaja na Mheshimiwa Dkt. Kafumu wajiandae. Mheshimiwa Batenga.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika ajenda iliyo mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nizidi kuwashukuru na kuwaenzi sana wanawake wa Mkoa wa Kagera kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi hii ya kuwa katika Bunge hili ambalo linaelekea mwishoni. Nitawaenzi daima kwa hiyo naomba Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni vema na mimi pia niwapongeze Mawaziri wote wawili waliowasilisha hotuba zao. Mawaziri hawa ni wanawake wameonyesha uwezo wao wa kumudu kazi zao walizokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nawapongeza sana, wanawake wanaweza wakipewa nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua wanawake ni jeshi kubwa kwa sababu wanamudu majukumu mazito katika taifa hili. Wanawake wanamudu majukumu mazito ya kujenga uchumi kupitia kilimo, biashara ndogondogo, ufugaji na njia nyingine. Pia, ni jukumu zito sana wanalobeba wanawake katika uzazi wa kuongeza Taifa, malezi ya watoto na familia. Wanachohitaji wanawake kutoka kwenye Serikali yao ni kupewa huduma ya maji safi na salama na wayapate karibu na maeneo yao. Ingependeza sana kama tulivyojua awali kwamba wangepata mita 400, mtu anatoka ndani ya nyumba angalau atembe mita 400 apate maji. Ingewasaidia sana wanawake kuwapa muda zaidi wa kufanya shughuli zao za kulea watoto, kutunza familia lakini pia katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana katika miradi ya maji, sehemu nyingine maji yamepatikana vizuri lakini sehemu nyingine miradi ya maji imesuasua pia inaonekana kwamba kuna uchakachujaji katika miradi ya maji. Nizungumzie mradi mmoja ninaoufahamu wa maji katika Kata ya Nyakahura. Inasemekana gharama yake ni takribani shilingi bilioni 1.2 lakini ukiangalia namna mradi wenyewe ulivyo, unaona kwamba hapa sanasana kilichofanyika ni kuiba ile pesa. Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji wauangalie ule mradi kwani wananchi wameukataa mbele ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi wanasema kwamba kama ni huo basi waje wao wenyewe watumie hayo maji kama wanaona yapo. Kwa sababu kama ni mradi una *pump* maji masaa 18 ndiyo unapata lita 10,000, hivi huo mradi utawafikisha wapi watu?

Mheshimiwa Spika, inaonekana kwamba kuna namna fulani ambayo Wizara haikuwa makini katika usanifu wa mradi huo au na miradi mingine ambayo haikufanikiwa lakini pia katika kuteua wakandarasi kwa sababu mambo yote yanafanyika Wizarani bila halmashauri kujua, wao wanapelekewa tu ni mradi na wakandarasi ni hao. Najua kwamba Katibu Mkuu wa CCM atashughulikia lakini kwa sababu niliona ni vema nikalisema hapa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho wanawake wanahitaji wakienda hospitali, kituo cha afya au *dispensary* wapate huduma iliyokamilika. Wapate vipimo, waandakiwe dawa, wapate ushauri na vyote wavipate siyo wanaambiwa kwamba dawa hakuna, ukimwambia dawa hakuna anakwenda wapi? Kwa hiyo, wanawake wapate huduma hizo na zipo baadhi ya hospitali hasa Hospitali ya Biharamulo yasemekana kwamba bado huduma za mama na mtoto zinatolewa kwa kulipiwa. Kwa hiyo, tunaomba kama zipo hospitali za namna hiyo basi mambo hayo yaachwe wanawake wapate huduma bila kuambiwa hakuna dawa au kulipia wakati siyo sahihi kulipia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wanalohitaji wanawake ni hii mifuko ya mikopo hasa kupitia Halmashauri za Wilaya ya Miji ziongezewe fedha, fedha iwepo nyingi ya kutosha kwani vikundi vya wanawake Mkoani Kagera ni vingi sana lakini na mikoa mingine yote, fedha iongezeke ili wanawake wakope. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nawaomba waweke fungu ambalo litasaidia kuelimisha wanawake mambo ya ujasiriamali, jinsi ya kuendesha miradi na jinsi ya kutunza hesabu ili kwamba mikopo wanayopata ifanye kazi vizuri wanufaike lakini pia warejeshe mikopo iwe ya mzunguko wote wanaohitaji wapate.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hayo na mimi nichangie kidogo kuhusu pensheni. Pensheni kwa kweli ni kitu muhimu sana kwa wastaafu hasa waliostaafu miaka hiyo ambao walifanya kazi kwa uadilifu, kulikuwa hakuna cha kudokoa wakati huo. Wengine wamekuwa wazee na unapokuwa mzee unanyemelewa na maradhi mengi na yanayotibiwa kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, hiyo pesa wanayopata haitoshi kula lakini pia haitoshi hata kwa matibabu. Maana yawezekana kwenda hospitali ukatibiwa bure kwa sababu ni mzee lakini ndiyo hayohayo ya kwenda kuambiwa hakuna dawa. Sasa ukiambiwa hakuna dawa inabidi ujipigepige ukajinunulie dawa ili uponyeshe maisha yao. Kwa hiyo, hii pensheni ni vizuri wameongeza lakini niseme kwamba ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo kundi la wanajeshi wanalalamika sana pensheni yao ni kidogo mno. Kwa hiyo, nashauri wafikiwe waongezewe kiwango cha pensheni ili waweze kukimu mahitaji yao tukizingatia kwamba bado tunawahitaji, inaweza ikatokea huduma yao ikahitajika.

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi ya kuongea lakini naomba mambo niliyoyaongea yazingatiwe na nakushukuru sana wa kunipa nafasi hii. Hata hivyo, haitakuwa vema nimalize mazungumzo yangu bila kukushukuru wewe na ofisi yako kwa jinsi mlivyonitunza nilipokuwa mgonjwa, nilitembea na fimbo kwa kipindi lakini kwa huruma yako na kwa juhudi yako kwa kweli nakushukuru sana na ofisi yako kwa jinsi mlivyonihudumia, nimetibiwa sasa hivi na mimi



ukinituma naweza nikakimbia mbio za marathoni. Kwa hiyo, nakushukuru sana na Mungu akubariki sana katika maisha yako yaliyobaki na yatakuwa marefu tu, Bwana Asifiwe.

**SPIKA:** Ahsante. Yakiwa marefu kwenda mbinguni ndiyo safi tu. Mheshimiwa Deo Filikunjombe na Mheshimiwa Christowaja na Mheshimiwa Dkt. Kafumu wajiandae.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Ludewa ambao walinipa nafasi ya kuwatumikia kipindi cha miaka mitano sasa kama mtumishi na mwakilishi wao hapa Bungeni. Naomba pia niwashukuru sana wananchi wa Ludewa kwa ushirikiano wao katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwe mkweli sana na naomba niwe muwazi, tumepita katika changamoto nyingi na matatizo mengi lakini kwa kifupi tumesonga mbele. Tumetoka sehemu moja tumesogea mbele na kwa hakika matatizo hayajaisha na changamoto hazijamalizika lakini kule nyumbani wenye macho wanaona nuru ya matumaini ipo na mwanga wa matumaini juu ya maendeleo yetu upo. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Ludewa kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kusema wazi kwa niaba ya wananchi wangu kwamba kwa mara ya kwanza na mimi nitaunga mkono bajeti hii kwa sababu mbalimbali. Naunga mkono bajeti hii kwa sababu nina imani na Waziri wa Fedha na niseme bayana nampongeza sana Mheshimiwa Saada Mkuya. Ni Waziri msikivu na yuko makini, wengi tunamlaumu humu ndani lakini nafasi hiyo ni ngumu, umejitahidi sana. Nakupongeza kwa niaba ya wananchi wangu na mimi kama Mbunge wao nina imani na wewe na wananchi wangu wana imani na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze pia Naibu wako wote wawili, wanafanya kazi vizuri. Nampongeza Katibu Mkuu na ninawapongeza wataalam wako wote kwa ajili ya bajeti hii ambayo mmeileta Bungeni. Watakosoa ndiyo, sisi siyo Malaika lakini kwa niaba ya wananchi wangu wa Ludewa naunga mkono bajeti hii kwa sababu kubwa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwanza, Mheshimiwa Waziri amenipa bajeti ambayo inagusa Ludewa moja kwa moja, siyo matatizo yote, siyo changamoto lakini yale ya msingi yanaguswa. Ludewa mimi nina wazee na wastaafu, wanaosema Sh.85,000/= ni ndogo, siyo wakweli. Katika maisha ya sasa hizo Sh.55,000/= walizokuwa wanapewa wazee wale walikuwa wanazifurahia lakini Waziri ameonyesha kwamba una uchungu na kwamba kweli wewe ni mama

wa Watanzania, ameongeza kutoka Sh.55,000/= mpaka Sh.85,000/=. Naipongeza Serikali, nakupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, hili siyo la kubishana kwa sababu kila mmoja wetu humu ndani atakuja kuwa mzee siku moja, tunajivunia ujana leo lakini uzee unakuja, kwa hiyo, tunachokifanya hapa tunaboresha maslahi ya wazee wa sasa na wa baadaye. Kama walivyosema wenzangu, ingekuwa ni jambo la busara sana mkasema hawa wazee pensheni yao ya malipo ya uzeeni wataanza kulipwa lini, tuweke kikomo au muda ili ijulikane, hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, lakini cha pili, kwa niaba ya wananchi wangu wa Ludewa, nimesema siwezi kupinga bajeti hii kwa sababu wakati mimi nachaguliwa kuwa Mbunge miaka minne iliyopita, mimi nina vijiji 77, Ludewa nilikuwa na vijiji vitatu tu vyenye umeme yaani Ludewa Mjini, Mavanga na Lugalawa. Sasa hivi navyozungumza na kwenye bajeti hii nimeona kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuleta umeme Ludewa, katika vijiji 77 tunapeleka umeme kwenye vijiji sitini na saba. Kutoka vijiji vitatu mpaka vijiji sitini na saba, haya ni mafanikio makubwa ya CCM, ni mafanikio ya Wizara yake, ni mafanikio ya Mbunge na ya wananchi wa Ludewa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme bayana, kule Ludewa ni muujiza leo umeme kwenda Nindi, Kilondo, Lwilo, Manda, Luvuyo, Ziwani, Utilili, Mlangali na Ligumbiro. Nikipinga bajeti hii wananchi wangu hawawezi kunielewa ndiyo maana naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu mmezungumzia tozo za mafuta ya Sh.100/= na Sh.150/= ni nyingi mno. Tuwe wakweli, fedha hizi kama kweli Waziri atazipeleka kwenye umeme, zitakwenda REA zifike vijijini hii tozo ni ndogo mno, *in actual fact* tuongeze. Haiwezekani Wabunge mnataka maendeleo na maisha bora lakini kuchangia hamtaki, tusiwapotoshe Watanzania. Wananchi wangu wa Ludewa wako tayari kuchangia kwa sababu harusi wanachangia na humu ndani Wabunge harusi mnachangia mpaka shilingi milioni 90 au 100 na harusi zenyewe hazifanyiki, michango imekwenda, mbaya sana. Kwa hiyo, harusi mnachangia lakini tozo ya umeme hamtaki, tusiwapotoshe wananchi, haiwezekani! Maendeleo bila jasho hayawezi kuja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba urudie hapo.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Kwamba maendeleo bila jasho hayawezi kuja?

**MBUNGE FULANI:** Ile ya harusi.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Ile harusi ile? (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika wananchi wangu wa Ludewa wanachangia harusi na humu ndani tunachangia harusi, lakini kuchangia umeme hatutaki. Niseme bayana na niwe mkweli kabisa, kule Ludewa umeme na maendeleo tunayapokea vizuri, tunachangia mpaka nguvu zetu siyo fedha tu. Pamoja na wananchi wa Ludewa tunakwenda kushirikiana, Serikali inapoleta mradi tunakwenda kuchimba na kufyeka na wananchi wanaelewa. Leo Mbunge anayegomea tozo ya mafuta Sh.100/=, ndiyo, wanasema ni nyingi na miti itakatwa mno. Miti wanakata hata mafuta yalipokuwa bei ndogo tu na ni afadhali tukate miti miaka miwili au mmoja kwa sababu baada ya hapo hatutakata tena. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono tozo na ni ndogo na *in fact* hata tungeongeza kwa ajili ya wazee itawasaidia zaidi. Tupo tayari kuchangia vitu ambavyo siyo vya msingi lakini vya maendeleo tunawapotosha Watanzania. Bajeti hii siwezi kuipinga *as long as* fedha hizi zinakusanywa zinapelekwa sehemu husika. Leo nina vijiji 67 vinabaki 10, lazima vijiji 10 navyo vipate umeme, lazima hizi fedha ziende kule, ndiyo maana naunga mkono kwa niaba yao. Mnaopinga kwenu mna umeme, lakini kwangu Ludewa sina umeme kwa hiyo siwezi kupinga. Kwa hiyo, cha pili, nimefurahi hii *component* ya kuwashirikisha wananchi kuchangia sisi wenyewe, matajiri na maskini tuchange ili umeme uende vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, cha tatu, kwenye bajeti hii kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na kuimarisha barabara za Ludewa. Wakati naingia humu ndani hatukuwa na hata na sentimita moja ya lami Ludewa, miaka minne iliyopita. Tulianza mwaka wa pili baada ya mimi kuingia kilomita moja na nusu, tumekwenda kilomita tatu na ninavyozungumza sasa hivi tuna kilomita 15 tunajenga Ludewa mjini, kwenye bajeti hii zimetengwa kilomita 50. Mimi nikipinga bajeti hii maana yake napinga lami Ludewa, ndiyo! Tutakuwa bado hatujamaliza kilomita 200 mpaka Manda lakini haya ni mafanikio makubwa. Roma haikujengwa siku moja kwa sababu kuna fedha za lami huu ndani, mimi naunga mkono na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wataalam wake nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, ni daraja la Mto Ruhuhu kule Manda kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ni kweli upembuzi yakinifu unaendelea lakini Serikali Mheshimiwa Waziri mmetenga fedha lijengwe daraja la chuma wananchi waweze kuvuka kwenda Mbinga, Lituhi na waje Manda. Siwezi kupinga bajeti hii, naiunga mkono ili wananchi wangu waweze kupata usafiri kwenye Mto Ruhuhu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la tano ni meli Ziwa Nyasa. Kuna fedha zimetengwa humu ndani na mimi nimekwenda Kiwira kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, kwa macho yangu nimeshuhudia meli inaundwa na fedha ziko humu ndani kwenye bajeti hii ili wananchi wa Ziwa Nyasa kule Manda, Lupingu, Lifuma, Makonde, Likonde mpaka Lumbila na Kilondo waweze kunufaika nayo. Niseme tu bayana kwamba bajeti hii hii ni nzuri sisi Wabunge tuunge mkono tumsaidie Waziri na wataalam wake waitekeleze badala ya kuipinga.

Mheshimiwa Spika, sita, mradi wa Liganga na Mchuchuma. Namshukuru Mheshimiwa Mary Nagu yuko humu ndani alisimamia na kusaidia. Sasa hivi upembuzi yakinifu umemalizika, ujenzi wake unaanza mwaka huu na wataalam wako kule chini, wananchi wanalipwa fidia, hatugombani tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, saba, chuo cha VETA fedha zake nimeziona ziko humu ndani ziweze kuwasaidia vijana na watoto wetu waweze kupata ajira. Nikipinga bajeti hii wananchi wa Ludewa hawawezi kunielewa ndiyo maana naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kitu kimoja kuhusu wafanyabiashara. Nimesoma ukurasa wa kumi kuhusu matumizi ya EFD. Nawaomba Wabunge wenzangu tuunge mkono kodi ni lazima kulipa, wote matajiri na maskini. Haiwezekani tusilipe kodi halafu tunataka maendeleo. Tunaposafiri nje tunalipa kodi mpaka pipi na vitu vidogovidogo mpaka mama ntilie wa nje wanalipa kodi, haiwezekani sisi tuweke mipaka. Tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri aweze kupata fedha, Majimboni tunataka fedha, wananchi kule chini, Wabunge tulipe kodi na kila mmoja alipe kodi tusilete siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mgomo wa wafanyabiashara, kuna mfanyabiashara mmoja nilimuuliza kwa nini umegoma akasema kwa sababu wenzangu wamegoma. Sasa unagoma kwa sababu wenzako wamegoma? Tutoe elimu ya kutosha, tuwe kitu kimoja, wafanyabiashara kazi yao ni kukusanya kodi wao wanakuwa mawakala tu. Ukisikiliza madai ya wafanyabiashara wanasema mitaji yao inakufa, mtaji hauwezi kufa, mtaji utakufaje wakati fedha yako iko palepale na kimsingi aliyepaswa kulalamika ni mlaji, *consumer* wa chini. Mlaji wa chini halalamiki, analipa kodi, inakwenda kwa mfanyabiashara, mfanyabiashara akusanye kwa niaba ya Serikali. Wafanyabiashara nawashauri wao wadai *agency fee* ya kukusanya kodi kwa niaba ya Serikali lakini kodi ni lazima sote tulipe na hili halina mjadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Malima yupo hapa ndani, Ludewa wananchi wangu ni wakulima na Serikali inapowakopa wakulima hili si jambo zuri, halipendezi machoni na fedha inayodaiwa ni kidogo sana. Naamini mkiamua mnaweza kuwalipa wale wananchi, wasikate tamaa, wawe na imani na sisi na wawe na imani na Serikali

yao. Nawaombeni sana muwalipe wale wakulima ili nao wapate stahiki yao kwa sababu msipofanya hivyo tunakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nataka niwashukuru wananchi wa Ludewa kwa ushirikiano wao na niwaombe tuzidi kushikamana, Mwenyezi Mungu akituweka wazima tutazidi kushikamana na mimi niseme nawapenda sana Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Christowaja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho nadhani katika Bunge hili la Kumi sio la Kumi na Moja kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutoa shukrani kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida hususan wanawake kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Nina imani kabisa sikuwaaibisha wala sikuwaangusha kutokana na *feedback* ambayo naipata.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Nilifikiri katika michango yetu ya bajeti ya mwaka huu wa kumaliza Bunge la Kumi, tusingekuwa na mipasho ambayo tunapashana hapa leo. Nilitegemea kabisa Wabunge wote tutaweka mustakabali wa nchi yetu kwa mambo yale ambayo tutakwenda kuyafanya kwa mwaka wa fedha unaonza. Cha kushangaza nimesikia mipasho, huyu anamwambia mwenzake hivi, kwa kweli nisiende huko, naomba Wabunge watakaokuja Bunge la Kumi la Moja wasiige yale ambayo sisi tumeyafanya. Wawe wanachangia kwa manufaa na mustakabali wa taifa letu kwa sababu taifa hili ni letu sote. Taifa hili halina itikadi, taifa hili si la watu wachache ni la Watanzania wote. Tukiwa nje ya nchi tunasimama kama Watanzania, tunabeba bendera ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba Wabunge watakaokuja Bunge lijalo wasifuate haya ambayo tumeyafanya mabaya sana.

**SPIKA:** Na tuwaombe radhi wananchi kwa tabia mbaya. (*Kicheko*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kuchangia bajeti ya Serikali. Tumesikia michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge, nianze kuchangia kuhusu kuporomoka kwa shilingi. Sababu moja ambayo imesemwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo mimi naiona ni kubwa, zingine zote ni sawa, hii ya matumizi holela ya dola, hii ipo sana. Tanzania ni nchi pekee ambayo inaruhusu matumizi ya dola kwenda sambamba na pesa yetu. Ukienda dukani sasa hivi kwa mfano ukienda kwenye

mall kwa mfano, Mlimani City, Quality Center unalipa kwa dola unapewa bidhaa unayoitaka lakini nchi zingine, Kenya tu hapo hawataki dola, hata ulie machozi hawapokei dola, wanapokea shilingi yao ya Kenya. Hivi sisi Tanzania tuna nini? Hili nalo linahitaji kweli kwenda shule kuona kwamba matumizi ya dola yanavyozidi katika nchi yetu? Hivi ndivyo ambavyo tunaporomosha shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, hebu sasa ifike mahali nchi hii ipige marufuku matumizi ya dola kwa shughuli zote ambazo hazihitaji. Hapa unanunua hata nguo kwa dola, ukitaka hereni hizi unanunua kwa dola, kweli! Hebu tusaidieni suala hili. Sababu zingine zote zilizotajwa ni za msingi zinahitaji maandalizi mengi lakini hii ambayo inahitaji *immediate action* hebu fanyeni upesi tupige marufuku matumizi ya dola.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye hoja ya vyanzo vya mapato, tumesikia hoja mbalimbali, kuongezeka kwa tozo za mafuta ya *diesel*, *petrol* na mafuta ya taa. Wazo ni zuri, nia ni nzuri ya kupeleka umeme vijijini, kweli kabisa ili kukabiliiana na mabadiliko ya tabia nchi, tusipofanya bidii mabadiliko ya tabia nchi katika nchi yetu yatafika katika kiwango kibaya sana, miti itazidi kukatwa na ukame utaongezeka. Hata hivyo, kwa kuongeza tozo ya mafuta ya taa kutoka Sh.50 mpaka Sh.150, hivi huyu mwananchi wa kijijini, mimi nimekulia kijiji, nimefanya shughuli zote za vijijini, nimekuja kupata nafuu nilipoanza shule ndipo nikaondoka kijijini lakini wazazi wangu bado wako kijijini, njia mbadala ya kupata nishati ya umeme ni kuni.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuongeza hii tozo ya mafuta ya taa hivi tunategemea hawa wananchi waende wapi? Tuwe makini, hatukatai huo umeme, mpaka huo umeme uje kufika kijiji kwangu ni miaka mitano na zaidi. Kwa sasa hivi hao wananchi ambao tunawaongezea hii kazi ya kununua mafuta ya taa kwa tozo hiyo ambayo imeongezeka waende wapi hawa wananchi? Kwa kufanya hivyo, tutaongeza wanawake wenye macho mekundu, tutaongeza mauaji ya vikongwe, tutaongeza matatizo kwa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naombeni hii tozo ya mafuta ya taa itafutiwe sehemu nyingine. Kuna watu wali-*proposal* hapa ipelekwe kwenye *petrol*. Sikatai sana kwa sababu *petrol* ndiyo tunatumia kwenye magari yetu sisi lakini siyo kwenye *diesel* kwa sababu mashine za kusaga ziko vijijini, mabasi, daladala, bajaj na magari mengine yako vijijini, hivi hawa wananchi mnataka kuwarudisha kwenye karne ya mawe waanze kusaga kwenye mawe? Fikiria mwenye mashine ya kusaga, anatomia *diesel*, utakapongeza hapa, wananchi hawatajua ni kiasi gani kimeongezeka na yeye atapandisha anavyojua.

Mheshimiwa Spika, kuna zile *associated costs* ambazo ataangalia, *maintenance* ya mashine yake, *service* yake na kila kitu ananunua *diesel* kutoka mjini, atasafirisha kwenye basi amelipia nauli, amelipia na huo mzigo wake mpaka afike kijijini ni kilomita kwa kilomita, kule bei haiwezi ikawa sawasawa na yule wa mjini. Tuangalie jamani haya mambo yanawagusa wananchi wa kijijini wenye kipato kidogo. Mimi sipingi umeme wa REA lakini napinga hizi *cost* zingine ambazo zinakuwa *associated* na kuongeza tozo ya mafuta ya taa na *diesel*.

Mheshimiwa Spika, watu wamezungumza hapa wana mabasi yao, wengine wana vituo vya mafuta, hivi unafikiria hii tozo mwenye kituo cha mafuta au mwenye basi inamgusa nani? Inamgusa mwananchi wa kawaida ambaye ndiye mlaji wa mwisho. Mimi kama nina basi langu nita-*calculate* zile *cost* ambazo nitazitoa na faida nitaweka. Kwa hiyo, hata kama utaongeza Sh.9,000/- kama nilivyosikia jana au shilingi ngapi sijui haitakuwa hivyo, vyombo vyetu vya usimamizi SUMATRA vimeshindwa kazi. Vipo miaka yote lakini je, vinafanya kazi sawasawa kuweza ku-*regulate* hizi nauli zinazowekwa, tunajuaje kama watafanya hivi, hatupingani.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kinachotupa wasiwasi, huu umeme wa REA, mwaka jana tulipitisha tozo ya Sh.50/- lakini imefanya kazi wapi? Tulisikia zimedokolewa-dokolewa hapa, je, tuna uhakika gani kama hazitakwenda kuishia kwenye matumbo ya watu wachache? Tunahitaji usimamizi hapa, zikitengwa basi zifanye kazi sawasawa zisidokolewe na wale wachache wanaoangusha hii Wizara. Zisimamiwe sifanye kazi yake vizuri, hatutakuja kupiga kelele hapa. Mwananchi akiona umeme umekuja kwa wakati kwa hiyo tozo ambayo tumeiona hata kama ni kubwa angalau ile simanzi inafutika kwa sababu kitu anakiona. Sasa pesa zinatengwa hazitoki, hazifanyi kazi, zinapoishia zinaishia kwa wachache, huu ndiyo wasiwasi kwa kweli tunasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kuzungumzia fedha zinazotengwa kwenye miradi. Niende kwenye kipaumbele kilichowekwa na Serikali cha elimu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tunashughulikia bajeti ya Wizara ya Elimu na nilizungumza hapa wakati wa kuchangia wa bajeti hiyo, miradi inayohusiana na vyo vikiu, ujenzi wa *lecture theatres* na majengo ya vyo vikiu kwa mwaka unaoisha huu hakuna senti tano iliyopelekwa. Kama kipaumbele ni elimu, watoto wa shule kwa mfano hawa ambao wapo hapo juu, hawa naona ni shule ya binafsi wanasoma vizuri lakini wanataka wakimaliza *O' level* na *A' level* waende chuo kikuu na wakifika chuo kikuu wakute mazingira mazuri kama yale waliyokuwa nayo kule nyuma.

Mheshimiwa Spika, sasa wanafunzi wanakuta *lectures theatres* wanarundikana wengine ni watu wazima, wengine wanakaa chini, wanaoathirika ni watoto wa kike kwa sababu hawawezi kukimbia kuwahi viti,

wanakaa nje, hawasikilizi, huyu *lecturer* anahutubia kitu gani mle ndani, mwishowe wanafeli na tunasema watoto wetu hawana akili, si sawa. Kwa nini Wizara ya Fedha haipelekei fedha za miradi ya ujenzi wa hizi *lectures theatres*?

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Chuo Kikuu cha Dodoma hapa, Serikali kweli mnafaa kujivunia na sisi tunawapongeza kwa kuanzisha chuo hicho, tunawapongeza kwa kweli. Chuo kile ni *image* ya Dodoma na ni *image* ya nchi yetu. Ni chuo kizuri sana sisi tulitembelea yaani ni *executive* chuo. Chuo hiki walituambia kwamba ujenzi wa Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati pamoja na ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Ardhi vinahitaji jumla ya shilingi bilioni 104. Bajeti ambayo imekuwa inatengwa kila mwaka, wanasema mwaka huu wametengewa shilingi bilioni 1.5, mwaka unaoisha walitengewa shilingi bilioni 2.3 nako hazikutoka zote zilitoka shilingi bilioni 1.3 bado shilingi bilioni 1.1 haijatoka.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mtiririko huu wa kutoa shilingi bilioni 1.5 watachukua miaka 60 kumaliza kujenga vyuo vikuu hivyo viwili tu basi lakini waliomba angalau mtenge shilingi bilioni tatu tatu waweze kuchukua miaka 20 kumaliza hizi *campuses*. Mnatafuta namna ya kumuenzi Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano anayemaliza muda wake, Chuo Kikuu cha Dodoma hicho hapo, malizeni hicho chuo mtamuenzi vizuri sana. Tutawasifia na watoto wetu watasoma vizuri. Msitafute kitu kingine cha kumuenzi Rais, malizeni hicho chuo ili hivyo vipaumbele viende sambamba.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kingine ni cha afya. Afya tumeona kwamba vifaa tiba na majengo mbalimbali hususani *MOI,MOI* wanataka pesa kwa ajili ya kununua vifaa kuweza kufanya *operations* zingine kupunguza *referrals*. Nilisema hapa, hizo *referrals* zitapunguza deni la *MSD* inayoidai Wizara. Tukipunguza *referrals* kwenda nje, maskini na matajiri wote tutatibiwa hapa. Pelekeni pesa pale *MOI* ili operesheni zifanyike pale, pelekeni pesa kitengo cha moyo ili operesheni za moyo zifanyike pale, pia pelekeni pesa kitengo cha figo, tutaokoa pesa nyingi sana ambazo sasa hivi Wizara inadaiwa, *MSD* wanasema mpaka Desemba, 2014 ni shilingi bilioni 103. Hii ni aibu, shilingi bilioni 103 acha hilo la Apollo, kwa kufanya hivi vitu vingine ambavyo tunawashauri mtapunguza sana gharama za kusafirisha watu nje.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuwapongeza wanafunzi wote waliosoma Msalato Sekondari, maana wamejitolea kujichangisha fedha kutoka mifukoni mwao pamoja na mimi mwenyewe kuweza kufanya ukarabati wa shule ile ya sekondari Msalato, tusaidie Serikali. Angalau sisi tumesoma bure basi tunachanga wenyewe, akina Mheshimiwa Ester Matiko wako hapo. Wanafunzi tuliosoma Msalato na wengine ambao wako sehemu mbalimbali tunachanga ili kukarabati shule yetu.



Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wanafunzi wale waliomaliza Msalato miaka ile ya 1980 na kuendelea na pia Wabunge wengine muige mfano huo, tukarabati shule zetu vizuri kwa kutumia jasho ambalo Serikali ilitusomesha tupeleke *feedback* kule ili wadogo zetu na watoto wetu waweze kusoma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa mara nyingine, niwatakie kila la kheri katika uchaguzi unaofuata. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Nakupongeza kwa uzalendo wa hali ya juu, kama Wabunge wote wangepadili kama wewe wananchi wangepurahi sana. Ahsante sana. (Makofi)

Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kama Wabunge wengine hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niwape pole Watanzania pamoja na mimi mwenyewe kwa msiba mkubwa uliotufika huu wa Mufti wetu kutangulia mbele ya haki. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wananchi wa Igunga kwa kunipa nafasi ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki kifupi cha takribani miaka miwili na nusu lakini tumefanya kazi vizuri, tumeweza kuendeleza yale yote ambayo yalikuwa yameanzishwa na Serikali zote. Nashukuru sana wananchi wale pamoja na Serikali, japo kuna watu wengine wanasema kwamba Serikali haijafanya kitu lakini kwa kweli imejitahidi sana kufanya mambo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme Igunga matatizo ya maji, Waziri wa Maji alijitahidi sana kutuletea miradi ya visima kumi, tumeweza kufanikisha visima vinne ambavyo vinahudumia vijiji zaidi ya 20. Kwa kweli, naishukuru sana Serikali. Mradi wa maji Mwalala, Bulumbela, Matinje na Bulangamilwa unasaidia sana wananchi na nawashukuru sana wananchi kwa kuwa pamoja nami kushiriki katika kuleta maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali imefanya jambo zuri pia la kuanzisha mradi wa kuleta maji kutoka Ziwa Victoria. Upembuzi yakinifu umefanyika na tunategemea mradi huu utaanza kujengwa hivi karibuni. Mji wa Igunga pia ulikuwa una matatizo ya maji sana wakati naingia pale lakini Serikali pamoja na wananchi tumeweza kujenga chujio zuri katika Mji wa Igunga na linafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, masuala ya umeme, tulikuwa na tarafa moja ambayo haina umeme, kwa kupitia Umeme Vijijini sasa hivi Tarafa ya Igulubi iko kwenye Mradi wa Awamu ya II ya kupeleka umeme. Pia kupeleka umeme katika kijiji cha Itumba ambapo nilizaliwa na natokea huko, naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, miundombinu, daraja mashuhuri la Mbutu nalo limejengwa katika kipindi hiki. Naishukuru sana Serikali, imefanya kazi nzuri ya kushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusahau masuala ya shule za sekondari yaliyoanzishwa tumeyaendeleza, tumejenga maabara.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweza kupata Mji Mdogo wa Igunga katika kipindi hiki, tunaishukuru sana Serikali kuona jambo hili la msingi. Bajeti kwa ajili ya mji wetu tumepata tutakuwa na maendeleo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali imeamua pia kutafuta bajeti kutupa Jimbo lingine. Tumepata Jimbo la Manonga, tunaishukuru sana Serikali, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya yote ninayoyasema kwa ajili ya Igunga na Kitaifa, nimesema ya Igunga tu lakini mafanikio ya Kitaifa yako mengi sana, bado kuna changamoto nyingi sana ambazo tunatakiwa tuzifanyie kazi na hasa kwenye bajeti ya Serikali inayokuja kwa kweli ni lazima wavae soksi vizuri, waendeleze haya mambo kushughulikia hizi changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, nitapenda niseme machache ambayo yanahusu zaidi suala la kukuza uchumi. Yote haya tunayafanya lakini tuna tatizo la uchumi wetu kutohimili uwezo wa kutoa huduma hizi za jamii na tunatakiwa kwa kweli kuongeza juhudi. Nimeona mipango mingi sana kwenye hali ya uchumi na kwenye bajeti ya Mheshimiwa na Wabunge wengi wamesema ni lazima tukuze uchumi. Ukiangalia *statistics* kwenye hali ya uchumi hapa utakuta kwa mfano mauzo ya madini nje, *export* zetu zinazidi kuporomoka na uchumi hauwezi kukua bila ya kuwa na *export* za kufaa pamoja na kuzalisha ndani na kukuza viwanda ndani lakini *exports* ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma *statistics* unaona madini tumepungukiwa kwa -17%, wametoa sababu wanasema bei ya dhahabu lakini kuna sababu nyingi za sisi wenyewe, migodi miwili imefungwa tumeshindwa kui-*replace* kwa sababu tumeshindwa kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya utafiti na kufungua migodi mipya. Tunazidi kuwasema vibaya wawekezaji kwa hiyo wanapofunga wanafunga kweli na baada mitano, sita, saba ijayo migodi yote itafungwa na hapatakuwa na *export* katika dhahabu. Kwa hiyo, ni lazima tuweke mazingira

mazuri lakini pia na sisi wenyewe tushiriki kwenye jambo hili. Ukiangalia pia export za kahawa na zenyewe zimepungua. Kwa hiyo, naomba export tuziongeze, tuzalishe na kupeleka mazao nje ndipo tutaweza kukuza uchumi wetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wamesema sana Wabunge kuhusu viwanda. Tunaposema viwanda tuna maana pamoja na viwanda vinavyosindikiza mazao ya kilimo. Siwezi kurudia sana lakini ni jambo la msingi, ni lazima bajeti zetu zinazokuja tuzielekeze katika kuinua viwanda, *industrialization* ndiyo jambo la msingi. Ukiangalia nchi kubwa hizi zenye mafanikio kama China, 43% ya GDP yao ni kutokana na viwanda na sisi ni lazima twende huko, tukuze kilimo lakini tukuze viwanda.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme vijijini, watu wengine wanaponda hapa wanasema ooh umeme hauhitajiki vijijini lakini ni jambo la msingi. Ukipeleka umeme vijijini utahakikisha kwamba viwanda vidogo vidogo vinafufuka kule. Kwa hiyo, jambo la kupeleka umeme ni la msingi. Kuhusu tozo, nawaomba sana wananchi msipotoshwe juu ya tozo, Serikali yoyote haina mapato zaidi ya yale yanayotokana na wananchi, wananchi walipe kodi, wananchi watoe tozo, walipe ada, wananchi wajitolee, wafadhili wajitolee na sisi Wabunge tujitolee, ndiyo Serikali inapata mapato. Sasa unaposema kwamba wananchi wananyonywa kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini nashindwa kuelewa. Naomba wananchi wote sisi tulipe hii tozo iliyowekwa kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini na baada ya miaka kadhaa kwa kweli tutapata viwanda vidogo na vikubwa vitakuwa kwani tusipofanya hivyo haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme vijijini kule Igunga, naiomba Serikali ijitahidi sana kukamilisha. Igulubi tunahitaji umeme na tulisema mpaka tarehe 30 Juni, tuwe tumepata. Naomba tarehe 30 Juni, basi umeme ufike kwenye tarafa yetu ya Igulubi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuunge mkono sana Dada yangu Christowaja, jambo hili na nataka niliseme pamoja na kwamba amelisema naomba nilirudie, matumizi holela ya fedha za kigeni zinaua uchumi wa nchi yetu. Ni jambo la msingi na tumesema mara nyingi lakini sisi unakwenda kila mahali unatumia fedha za kigeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukienda Kenya kwenye hoteli kubwa ya kimataifa ukitaka kulipa dola wanakwambia nenda ukabadilisha hapo kwa sababu usipobadilisha ile hela kuna uwezekano wa kutoka nje isiingie kwenye mfumo wetu lakini ukibadilisha kwenye duka la fedha inabaki na kuingia kwenye uchumi wa nchi yetu. Ni kwa nini tunaliacha jambo hili? Kila mwaka Wabunge wanasema lakini Serikali haisikilizi. Ni jambo la msingi kwa kweli ukienda kwa

wenzetu kuna mifano mizuri. Naomba sana Waziri hebu lifikirieni jambo hili *next year*, Serikali ijayo sijui itakuwa ya nani, jamani pambaneni sana na fedha za kigeni tulipe kwa hela yetu ndiyo itakuwa na thamani na uchumi utaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie changamoto iliyojitokeza kwenye mradi wa kupeleka maji kutoka Igunga mpaka Tabora kutoka Ziwa Viktoria, upembuzi yakinifu umefanyika lakini imejitokeza kwamba hili bomba litapita sehemu ambazo kwa kweli zina nafuu katika masuala ya maji. Sasa wananchi tunafikiria kwamba ni vizuri wangepitisha maeneo yale ya mbungani wakitokea Shinyanga wakakatiza katikati hapo ili bomba hili lipite katikati ya maeneo ambayo ni makame na tunapotoa matoleo wananchi wengi waweze kupata lakini tukipitisha upande wa juu huku karibu na barabara kuu, maji haya wananchi wale wa mbali kabisa wanaweza kushindwa kuyapata. Tunaomba Serikali mlitazame hili kama inawezekana na kama haiwezekani kwamba limeshakamilika hilo basi mtengeneze matoleo bomba kubwa liende upande ule ambako hakuna maji kwenye Tarafa za Igulubi, Manonga na Igunga watu wana taabu sana ya maji, tunaomba hilo bomba litusaidie. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena kusema kwamba naomba wananchi wasipotoshwe kuhusu tozo ya umeme. Tozo hii ndiyo mkombozi wa kuleta mazingira ya viwanda katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kidawa nadhani dakika kumi zinakutosha.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyokuwa mezani.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa pole kwa Waislamu na Watanzania wote kwa kufiwa na Mufti wetu.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa ujumla wake kwa kazi nzuri iliyoifanya katika kipindi chote hiki cha kuleta maendeleo ya nchi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ingawa kazi hii siyo rahisi.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato. Naipongeza TRA kwa kazi ngumu wanayoifanya ya ukusanyaji wa mapato. Katika kipindi cha mwaka wa bajeti unaoendelea TRA kufikia mwezi Juni matarajio yamekuwa ni kukusanya karibu 90% ya mapato ingawa hawatafikia lengo lakini kukusanya 90% kama

wako shule wanapata A+. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika katika ukusanyaji wa mapato hasa kupanua wigo wa vyanzo vya mapato na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji kwa sababu ukiongeza ufanisi mapato yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa mtizamo huo, TRA inahitajika kufanya utafiti wa kina kuona uwezo wa kuzalisha mapato kutokana na vianzio vilivyopo hivi sasa na vilevile kutafuta vianzio vipya kutokana na sekta mbalimbali mpya ambazo zinakua hivi sasa kwa mfano sekta ya gesi. Vilevile kuangalia ni namna gani watazuia ukwepaji wa mapato. Kuna wimbi la kukwepa mapato kwa maana hiyo mapato mengi yanapotea kutokana na ukwepaji huo.

Mheshimiwa Spika, kuna ujanja mwingi unatokea pale TRA. Mfano mmoja Mama Madabida pale amezungumza yaliyomfika yeye mwenyewe, haya watu hawadanganyi na wala siyo uongo, ni kweli yanatokea. Kwa hiyo, TRA pamoja na Serikali nzima ijitahidi kuziba mianya hiyo na wasimuogope wala kumstahi afisa anayefanya hivyo hata kama zitatoka karatasi kutoka wapi, huyu msameheni, hakuna kumsamehe mhalifu. Ukimsamehe mhalifu ataendelea kufanya uhalifu wake. Maadili ya maafisa ni jambo muhimu sana katika upatikanaji wa kodi halisi inayostahiki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile wafanye utafiti, mbali na utafiti wa ndani lakini waangalie nchi zinazofanana na mazingira ya kwetu, ni vianzio gani vya mapato wanavyo. Pengine wanaweza kuja na vianzio vipya tu ambavyo ndani ya nchi yetu pia tunaweza kuvitumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi. Mara nyingi tunatupia macho TRA ukusanyaji wa mapato ya kodi lakini vilevile kuna nafasi nzuri tu ya kukusanya mapato yasiyo ya kodi lakini Wizara, Taasisi na Idara za Serikali zile ambazo nazo wanatakiwa kukusanya mapato hawachukulii kama hili ni jukumu lao la msingi. Ndiyo maana takwimu siku zote zinaonyesha kuwa mapato yasiyo ya kodi yako chini na hata siku moja hayajafikia malengo. Kwa hiyo, Maafisa Masuuli na viongozi wa Wizara wajue kwamba hili ni jukumu lao la kitaifa na wao wanatakiwa wachangie kwenye bajeti ya Serikali, wasikae kusubiri na kulaumu kwamba Hazina haileti mapato ya kutosha lakini na wao wafanye kazi ya kukusanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya mapato kutoka katika sekta isiyo rasmi, makusanyo haya ni madogo mno na ni kwa sababu bado ile sekta haijafikiwa. Tulizungumza hapa kwamba kupatikana kwa Vitambulisho vya Taifa kwa kila mmoja wetu kutasaidia kupatikana kwa mapato zaidi katika sekta hii kwa sababu kutawatambua hawa walipa kodi, wako wapi na wanafanya nini. Naona Serikali bado kabisa haijatilia uzito suala hili kwani bajeti inayotengwa kwa Wizara hii inayoshughulikia masuala ya NIDA ni ndogo sana na hata hiyo

inayotengwa haitolewi. Kwa maana hiyo, haiwezekani mapato kutoka sekta isiyo rasmi kuweza kupatikana kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mapato kutoka Serikali za Mitaa vilevile yako kwa asilimia ndogo kabisa. Vilevile kuna uzembe unafanyika, mambo mengine ukiyasikia yanauma kabisa. Ripoti ya CAG inasema, kuna fedha zimekusanywa na mawakala lakini halmashauri zinashindwa kwenda kuchukua zile fedha. Ametuambia kwenye ripoti yake ya mwaka 2013/2014 kwamba kuna karibu shilingi trilioni 4.9 wamekusanya mawakala, wao hawaendi kukusanya na katika mikataba yao hakuna hata kile kipengele kinachoonyesha kwamba wasipozipeleka zile pesa wafanywe nini. Ina maana unamnufaisha yule wakala, anazikusanya na kufanyia biashara zake sisi wenye pesa tumekaa tu, Serikali imekaa tu haifuatili halafu inalalamika haipatiwi fedha. Ni lazima kila mmoja katika Serikali na sisi viongozi tutimize wajibu wetu wa ukusanyaji mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Spika. utumiaji wa EFDs, yalikuwepo malalamiko mengi tu ya wafanyabiashara lakini wafanyabiashara wanajua ni nini wanachokitaka, wanajua ni nini wanachokisema. Jambo hili likitekelezwa, litasaidia Serikali kupata mapato stahiki kwa sababu zile mashine hazisemi uongo labda ziwe *tempered* na kama kuna *room* hiyo ya ku-*temper* lakini wanafanya kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, tumesema hii itazuia hata ile mianya ya rushwa kwa sababu hakuna tena mtu kwenda kuonana na mtu, mkusanya kodi kwenda kwa mlipa kodi na kumwambia lete nakuandikia hiki, ni kitu kinakwenda huko huko *electronically*, Serikali inapata haki yake na wafanyabiashara nao wataacha kulalamika kwa sababu kile kinachokatwa kitakuwa ni halali kabisa kukatwa lakini sasa kuna malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi nao waelimishwe umuhimu wa kudai risiti, hawadai risiti. Wanaambiwa bei kubwa inawekwa kama hudai risiti na bei ndogo kama unadai risiti basi wanaridhika mimi nitachukua hiyo bei ndogo hawadai risiti kumbe wafanyabiashara wanajua ni nini wanachokifanya, Watanzania wa kawaida hawajui wanaona wamepata kwa bei ya chini kwa kuwa hawakudai risiti lakini kumbe kwenye ile bei tayari kuna kodi ndani yake na kodi ile haifikishwi Serikalini, wanachukua wao wafanyabiashara.

Kwa hiyo, ndugu zangu, viongozi wa ngazi zote, wa Serikalini, wa kwenye taasisi mbalimbali hata kwenye vyama tushirikiane na Serikali kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili kwa sababu wote tunahitaji kodi kwa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na tozo ile ya mafuta iliyoongezwa, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti tulilijadili sana katika Kamati yetu, manufaa na hasara ya tozo hii kuongezeka. Tukaona kwamba tukubaliane na tozo hii kuongezwa kwa sababu manufaa yake ni makubwa kuliko ile gharama inayopatikana kwa muda mfupi ya kupanda kwa maisha. Hapa Mheshimiwa Mbunge wa Muheza na Mheshimiwa Shabiby wamefanya *calculation* na kutuambia kile kima kinachoongezeka katika bei za magari na kadhalika siyo kubwa sana lakini umeme vijijini utasaidia kukuza ajira ya mtu mdogomdogo, umeme vijijini utasaidia kujenga viwanda kwa maana hiyo na ajira humohumo, umeme vijijini utasaidia kupatikana huduma nzuri hospitalini na shuleni.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunalalamika kuwa akina mama wanakwenda kujifungua hospitali na tochi mkononi lakini kukifika umeme kule katika vijiji vyote shida hiyo itaondoka. Kwa hiyo, ndugu zangu Watanzania tutoeni hii tozo kwa imani yote kusaidia Serikali kwa sababu mambo mazuri yanakuja huko. Ni bora tuumie kidogo sasa hivi lakini kwa mapana yake na muda mrefu tuendelee kupata manufaa ndani ya nchi yetu. Hakuna nchi iliyoendelea bila ya kuwa na umeme, umeme ni kichocheo cha maendeleo. Kwa hiyo, watu hapa wasipige kelele gharama itapanda, itapanda sikatai lakini kwa kiasi kidogo kuliko manufaa yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hii kengele yao imekurusha dakika mbili, tunakushukuru sana. Tukirudi baadaye saa kumi na moja, Mheshimiwa Fakharia Shomar, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, Mheshimiwa Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mheshimiwa Dkt. Huvisa mjiandae.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

(*Saa 06.57 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae! Tutaanza kuongea sisi peke yetu.

Kabla ya kusitisha kikao nilikuwa nimesema tukirudi tutaanza na Mheshimiwa Fakharia Shomari, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta na Mheshimiwa Abdulsalaam Amer. Mheshimiwa Fakharia!

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kutoa salamu za rambirambi kwa Mufti wetu Issa Shaban Bin Simba, Mungu amjalie amuweke mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, vilevile sina budi kuwajulisha waislamu wote kwamba tuko pamoja kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na nasema Ramadhan Karim. Pia, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na watendaji wake wote na Waziri anayeshughulikia mipango na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya waliyotuletea hapa Bungeni, na sisi tunaendelea kuijadili.

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia kidogo kuhusu mapato. Vyanzo ni vingi ambavyo Mheshimiwa Waziri amevizungumza na namshukuru kwamba hakuna kinachotosha, lakini kajitahidi kupita kila upande ili kuhakikisha kwamba mapato yanaweza kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jitihada ziendelee kwa viongozi wetu kuhakikisha mapato yanaweza kupatikana na kuweza kukidhi haja ili tuweze kutumia na kufikia malengo. Tukae tukijua na tukumbuke kwamba tunatumia *cash budget*, maana yake ukusanye na uweze kutumia. Bila ya kukusanya fedha za kutosha, tujue tutakwama katika mipango yetu yote tuliyoipanga.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wale watendaji wote watakaozembea kusimamia kupatikana kwa kodi zetu, Wizara isiwaonee haya, ni kuwafukuza moja kwa moja, ni kuwatimua, hakuna uhamisho, tumechoka na uhamisho, kaharibu hapa anapelekwa hapa! Mtu kakosea anafukuzwa kazi, tuendeleo mbele! Maana sasa hivi ni mfumo wa vyama vingi. Hawa maafisa wako CHADEMA, CCM, CUF! Sasa kuna wengine wanafanya kusudi ili kuiangusha Serikali na ukimhamisha huku, anakwenda kuharibu huku! Sasa naomba Mheshimiwa Waziri hilo ulisikie na ulipokee kama ni rai yangu na yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, vilevile hizi mashine za *EFD*, tuhakikishe zinafanya kazi, kutokana na maelezo yako katika bajeti yako umesema usimamizi utakuwa mkubwa kuanzia Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, wafanyabiashara na watu ambao wanaweza kutumia mapato yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nitakuja na mambo ya ushuru, kulipa mara mbili, ambayo Zanzibar ndiyo ilikuwa kelele yao. Lakini, Mheshimiwa Waziri ametujulisha kwamba kuanzia sasa suala hilo halipo tena, marufuku na wala halitokuwepo. Nampongeza, tena nampongeza sana, lakini natoa tahadhari, jambo hili alilotuletea hapa Bungeni litendeke kwa vitendo na sio libakie katika karatasi, kwa sababu moja kwa moja kero ya Muungano hapa tumeishaiondoa na muarubaini wake umeshapatikana.

Mheshimiwa Spika, nakuja na suala la tozo ya mafuta kwenda *REA*. Mimi siipingi, naikubali, lakini ningemuomba Mheshimiwa Waziri, ilivyokuwa *dizeli* 50, petroli 50 na mafuta ya taa wangepanya 50. Ikawa wote tupo sawa tu, kwa sababu sasa hivi kweli tukubali, vijijini wanatumia mafuta, lakini sio wengi sasa



hivi wanaotumia mafuta. Unajua huyu Mchina katuharibu, kila mtu ana taa ya Mchina sasa hivi, kama hatumii kwa betri, atatumia ya kuomba chaji kwa jirani, lakini kile kibatari cha kuwasha vile kizamani tukaingia moshi puani kidogo ile imepungua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa ningemuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili kwa upeo wake ili kupunguza hii ghasia, kelele, malumbano aweke sawa, na kwa kuwa zote zinakwenda REA itakuwa hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni machache tu; ni kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa vipaumbele alivyoviweka ambavyo navikubali na ninampa *big up*. Vilevile maelezo yake aliyotuambia kwamba hakuna miradi itakayoongezwa isipokuwa iliyokuwa haijamalizika ndiyo watachukua jukumu la kuimaliza. Naipa hongera Serikali, nawapa hongera watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulsalaam Amer.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nipate kutoa mawazo yangu kidogo katika hoja hii ya bajeti ya Serikali iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa uwezo wake ameweza kutuweka Wabunge wote hapa kwa miaka mitano, na tunasikitika kwa waliopoteza maisha, basi ni mpango wa Mungu, lakini tuombe Mungu basi baada ya uchaguzi tuweze kurudi wote hapa ili tuendelea kutumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nitaongea machache. Lakini kwanza, nitaongea kuhusu BVR au uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura ambalo sasa hivi linaendelea katika nchi yetu. Uboreshaji wa daftari unafanywa kwa bajeti ya Serikali, na fedha ambazo tunapitisha leo ni michango au ni kodi za Watanzania wote wenye vyama na wasiokuwa na vyama. Kwa hiyo, tunategemea kwamba hili zoezi litaendeshwa vizuri na liache sasa kuwa adhabu kwa Watanzania ambao sasa hivi wanaenda katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza zoezi hili Serikali ilishauriwa kwamba ingekuwa vizuri ikatambua watu wake kwa kutoa vitambulisho vya wapiga kura, ambavyo vingeweza kuwasha kutambua nani ambaye ni raia na nani siyo raia. Lakini, kwa masikitiko makubwa Serikali hii iliyo madarakani imeshindwa kabisa kutoa vitambulisho kwa wapiga kura na sasa imeanza zoezi la wapiga

kura. Mimi nitajikita katika Mkoa wa Kagera kwa sababu Mkoa wangu unazo Wilaya ambazo zipo mpakani. Kwa hiyo, zoezi linavyoendesha katika...

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja kidogo, wenzio umewachanganya. Unazungumzia cheti cha kupiga kura au cha uraia.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nilisema kwamba tulitaka Serikali kwanza ingeweza kutambua watu wake, kwa kuwapa kitambulisho cha utaiifa ambacho Serikali imeshindwa kufanya hivyo kwa sababu Watanzania wengi hawajapata kitambulisho cha utaiifa na hawatapata labda mpaka uchaguzi uishe au mpaka mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, kushindwa sasa kutokuwepo vitambulisho vya utaiifa kumefanya zoezi hili la kuandikisha kuwa gumu na hasa katika wilaya za mpakani. Naomba nitoe mfano wa Wilaya ya Kyerwa ambayo inapakana na Uganda lakini pia inapakana na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana iliendesha hapa Operesheni Kimbunga, watu ambao sio raia, Waganda wakarudishwa kwao, Wanyarwanda kwao. Sasa imekuwaje Serikali imeshindwa kudhibiti raia hawa wameweza kurudi nchini tena? Na ni kwa nini Serikali sasa itumie zoezi la kuboresha daftari la wapiga kura kama ndiyo njia ya kuweza kutambua watu ambao sio raia na kuwazuia kujiandikisha kupiga kura?

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka hapa na kwenda kuhamasisha kama kiongozi wa chama, nimezunguka katika mkoa na nimeona kwa macho yangu maneno ambayo nitakwambia hapa. Nimeenda katika Kata ya Kibingo, kata hii ipo mpakani mwa Tanzania na Mrongo, ambao ndio Mpaka wa Tanzania na Uganda. Kipo kijiji kinaitwa Kijiji Kiinda, kijiji hiki kimeandikishwa kina *registration*, wananchi wake wameshiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Lakini kijiji kizima kimezuwa kuandikwa kwamba eti sio raia! Unaweza ukajiuliza, kijiji kimeandikishwa, kijiji kina hati, wananchi wake wameshiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wamepata Mwenyekiti, Serikali ya Kijiji, sasa kijiji kizima kimezuwa kuandikishwa kwamba sio raia, naunaweza ukashangaa!

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kuona tumegundua katika Wilaya ya Kyerwa, kama kijiji kinaendesha na CHADEMA au Mwenyekiti ni wa CHADEMA na chama kingine, wanazuiwa katakata kujiandikisha. Na hii ipo hata sasa hivi katika kata nyingine tano ambazo zinaendelea kujiandikisha, Kata ya Isingiro na vijiji vyako vyote, Lukurairo na vijiji vyako vyote na kata nyingine kwa kadri inavyokwenda. Kwa hiyo, hii imekuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hata wanapozuiwa hawapewi ile Fomu Na.3 A, na hata wakipewa, Mkurugenzi anawapiga danadana, ukienda ofisi ya Mkurugenzi, watu wamejaa utitiri pale wanasubiri kusaidiwa, lakini Mkurugenzi anakimbia ofisi, anafunga ofisi, watu wanakaa pale kutwa kucha, wengine wanalala pale kutaka kuthibitisha kwamba watu wengine wanazo hati za uraia.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya. Pia, nimeenda kwenye Kata nyingine ya Bugomora, nimeona maajabu, mwandishi anamwandikisha mama anamuacha mjomba. Sasa unaweza kushangaa ni namna gani mama mtu anaweza kuandikishwa, lakini mjomba ambaye ni kaka yake na yule mama asiandikishwe, kisa sio CCM!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka kujua, je, hili daftari limeandaliwa kwa ubaguzi wa kisiasa? Tunaomba majibu katika hili kwa sababu, nimeyasema hapa, kuandaa uchaguzi ni pamoja na kuandaa daftari. Mara nyingi tumeona katika nchi nyingi, vitendo vinavyofanya vita, vurugu vinatokana na uchaguzi, na nchi yetu imekuwa inafanya vizuri katika hili na inasifika. Sasa kama daftari linaandaliwa namna hii, katika ubaguzi huu, watu wananyimwa haki, watu wanapigwa! Nimeenda katika Kata ya Kibingo, polisi wamekuja tumewakabidhi watu ambao wanapigwa na Watendaji wa Vijiji. Yaani mtu anapigwa, lakini anaogopa hata kwenda polisi. Watu wamejengewa hofu ya ajabu!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba Serikali itueleze ni kitu gani inafanya! Najua Waziri yupo hapa, nimeishaongea na wewe, lakini nimeona niyasema haya, inawezekana na wewe unaweza kushindwa kuyashughulikia, kwa sababu hata ambayo umepewa mwanzo mpaka sasa hivi hujaweza kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, ukienda Bukoba Manispaa, kuna Kata ya Kashai ambayo ni kata mama, ina wakazi zaidi ya 36,000. Sasa hivi watu wanakisiwa watakaoandikishwa ni 17,000. Na mimi nataka kwenye Kata hiyo hiyo, mwaka 2010 tulikuwa wapiga kura zaidi ya 13,000, mwaka huu tumekisia na makisio yaliyopo kutokana na Tume yenyewe ni kwamba wataandikisha karibu watu 17,700. Lakini ninachotaka kuwaambia, sasa hivi BVR zipo pale zinakwama, watu wapo kwenye mistari siku tatu yaani watu wanaamka asubuhi saa kumi na mbili, saa kumi wanakaa pale wanalala, yaani watu wamekaa pale mpaka siku tatu mtu haondoki kwenda nyumbani.

Mheshimiwa Spika, BVR zinaandikisha watu 130 kwa siku. Kwa vituo kumi ni kama wanaandikisha watu ambao sio zaidi ya 1500. Kwa siku saba kama wataandikisha watu wengi, wataandikisha watu 10,000 tu. Je, na hawa watu wengine watakaobaki watapata haki yao ya kuweza kujiandikisha?

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukuambia, kipindi hiki kumekuwa na mwamko mkubwa, sio kama miaka ya nyuma. Kwa sababu mbalimbali watu wanataka vitambulisho hivi, labda watashiriki kupiga kura au wanahitaji kwa sababu hawana hata vitambulisho vya kitaifa, kwa hiyo, mtu mwingine anatumia kitambulisho hicho kujilinda yeye kama raia wa nchi hii. Sasa kama vitendo vinaenda namna hii, nina hofu kwamba watu watakuja kudai kutaka kupiga kura zao, watu watadai kushiriki katika kuandikishwa, kwa sababu ni haki yao kikatiba.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda Serikali ituambie, je, pale ambapo watu watabaki na hasa mijini, na nina wasiwasi hili zoezi litafanyweje Dar es Salaam, kama katika miji midogo kama ya kwetu Bukoba Manispaa limekuwa namna hii kwenye kata ambazo zina watu wengi, itakuwaje itakapokuja Dar es Salaam mtawapa siku saba?

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa inajua kwamba kuandikisha kupo, hakuna sababu ya kufanya *crash program*. Kuandikisha kumekuwa mateso., watu badala ya kufurahia zoezi hili, ili waweze kujiandaa kuweza kuchagua viongozi wao, sasa imekuwa ni kero, sasa imekuwa ni adhabu! Watu badala ya kufuarahi, wanapata mateso, vurugu zipo kwenye vituo, watu wanapigana ngumi kwa sababu *BVR* zile watu wengine wala sio wataalamu, hawawezi kufanya kazi vizuri, hawaandikishi, *BVR* zinakwenda *too slow!* Je, watu watakaobaki mtawaongezea muda ili waweze kupata haki yao?

Mheshimiwa Spika, nimeona niyaseme haya na hasa ya Wilaya ya Kyerwa, tunaomba Serikali iingilie kati. Kama ni mkakati wa Chama cha Mapinduzi wa kushinda, je, mna uhakika gani kwamba watu ambao hawajandikishi ni watu wenu au ni watu wa mageuzi?Maana unapozuia mtu kuandika, wewe hujui siri yake! Hujui siri yake! Kwa hiyo, anaweza akawa ni mtu ambaye ni wa chama chako, lakini wewe kwa kuhofia labda ni mtu wa CHADEMA au UKAWA, ukamnyima nafasi ya kuandika, kumbe angetaka kukupigia wewe mwenyewe kura. Kwa hiyo, naomba mtoe haki kwa watu wote, waweze kujiandikisha na wapate haki ya kuweza kupiga kura itakapofika tarehe 25 Octoba.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kwa muda uliobaki, naomba niongelee watoto wa mitaani. Bajeti yetu inapaswa kuwatendea haki watoto. Watoto wetu wawe ndani ya familia zenye uwezo, familia maskini, watoto yatima, watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto wa mitaani! Lakini wote ni watoto wa kitanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la watoto wa mitaani limekuwa likijibiwa majibu ambayo sio sahihi hata Wabunge wakiuliza maswali hapa. Jamii inayowajibika inaanza ndani ya familia, lakini Serikali inapaswa iwe juu ya jamii

na familia ili iweze kuona kama watu wake watakwenda ndivyo ilivyo kwa ajili ya ustawi wa maisha yao. Kama Serikali ikishindwa kusimamia familia hizo ama *society* ili iweze kutengeneza familia zao na kulea watoto vizuri, Serikali inapaswa iweke mikono yake kwa mtendo.

Mheshimiwa Spika, ukitazama, nilikuwa nasoma kwenye bajeti ya Maendeleo ya Jamii, Wizara hii ni Wizara mtambuka ambayo inaangalia maisha na maendeleo ya watu. Ukurasa wa tano, pale ambapo wamesema maendeleo ya watoto, kifungu cha tisa, wanasema; naomba kunukuu: Wizara inaandaa na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano wa Ushiriki wa Watoto. Mpango huu utatoa fursa kwa wazazi na walezi kujifunza njia bora za mawasiliano na mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Spika, mipango mingi ambayo ni ya Kimataifa inasemwa hapa na hasa Mawaziri wanapoulizwa kuhusu watoto. Lakini ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba watoto wa Taifa hili wanapewa malezi mazuri, wanasomeshwa, wanasimamiwa na baadaye wanakuja kuwa wakaaji na raia wazuri, wema katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kusema kwamba familia zisiwe *responsible*, (kwamba zisiwajibike), lakini je, sera tulizonazo zimeondoa umaskini ndani ya familia? Tunapoongelea maji kwa mfano, miradi ya maji inatekelezwa ipasavyo? Nichukue mfano hapa Dodoma tunapokaa, mvua inakaa miezi nane bila kunyesha, wananchi wanalima mazao yanakauka mwaka hadi mwaka. Mimi nimekaa Dodoma hapa nina watoto wangu wana bustani ya mahindi, kama humwagilii ni kwamba unaparua yale mahindi baada ya miezi kama mitatu, kila mwaka. Sasa wale wenye mashamba makubwa na wenyewe wanafanya hivi. Sasa unawezaje kujenga mahusiano kati ya mzazi na mtoto wakati hata chakula hamna ndani ya familia, wakati watu ni maskini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukifika Dodoma hapa ukiangalia familia zilivyo, hawana chakula, hakuna mipango ya umwagiliaji ambayo inaweza kuwafanya watu waweze kulima, wapate chakula, walishe familia zao, ili familia ziweze kuwa na afya nzuri, ziweze kupata lishe na baadaye kuwepo na mahusiano mazuri ndani ya familia. Huwezi kujenga mahusiano ndani ya familia wakati familia ina njaa, wakati familia ni maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali ifikirie na ije na mpango wa kuangalia namna. Tunasafiri tunaenda katika nchi nyingine tunaangalia jinsi nchi zinavyoandaa kwa ajili ya watoto wao, wengine wanapanga hata mfuko rasmi kwa ajili ya watoto wao. Hatuwezi kukubali watoto waishie mitaani, ukifika Dodoma hapa nenda mahali uagize chakula uone, watoto wanakuja kukuzunguka mpaka unaona aibu! Watoto wa Taifa hili, nenda Dar es Salaam, nenda katika miji mikubwa, watoto wamefurika na Serikali inasema ni wajibu wa

wazazi! Sawa, ni wajibu wa wazazi, lakini hizi familia maskini ni vipi tunaziangaliaje? Tunaziwekea mipango gani? Sera zinawawezesha kuweza kutunza hizi familia zao na kuandaa Taifa ambalo ni bora?

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuja na mipango, inapaswa kuweka mkono wake pale ambapo wananchi wake wameshindwa, aidha kwa kutunga sheria, kuzisimamia vizuri, kulinda familia, lakini pia kujenga hata vituo. Serikali haijengi vituo kwa ajili ya kulea watoto hawa. Zamani watoto walikuwa wanakusanywa, wanakwenda kwenye vituo, wanalelewa, wanatunzwa. Lakini ninaposema muandae vituo...

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Bahati mbaya sauti ya kengele ni mbaya. Mheshimiwa Abdulsalaam Amer atafuatiwa na Mheshimiwa Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Dokta Anthony Mbassa atafuatia, kasha Dokta Huvisa ajiandae.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema kubwa na ndogo kwa kuniwezesha leo kuwa hapa na mimi kuchangia bajeti ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kutoa pole kwa wote waliotangulia mbele ya haki na pia ninawatakiwa mkono wa ramadhani njema waislamu wote wa nchi hii na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa ushirikiano wanaonipa katika maendeleo ya jimbo letu na naamini wamestahimili mengi kwa upande wangu na mimi nimewastahimilia kwa mengi kwa upande wao, na nashukuru pia kwa kazi nzuri tunayofanya mimi na wao kuendeleza Jimbo la Mikumi na ninasema tupo pamoja, tuongeze ushirikiano wa hali ya juu katika kuendeleza Jimbo la Mikumi. Pia, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa kuweza kunikubali kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ahadi yangu kama Mbunge nimeweza kutimiza kwa asilimia 70. Nawatakiwa kila la heri na Mungu akipenda tutakutana mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Nagu, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Kighoma Malima na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa hotuba yao nzuri ya bajeti ya mwaka huu ambayo kwa kweli ni bajeti ya kwanza yenye mwelekeo wa kuiweka Serikali yetu kujitegemea badala ya kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa Serikali ni wa kwanza wa kujitegemea, naona umechelewa, lakini nashukuru wanajifunza kutokana na makosa. Wafadhili wanaahidi, lakini hawatekelezi na naamini wafadhili nao hali yao kiuchumi siyo nzuri hasa Dunia kwa ujumla, lakini Mheshimiwa Waziri kutegemea sana wafadhili nao pia wana masharti yao ambayo ni ya chini chini na mengine ya kuudhi kama ya jinsia moja ambayo baadhi ya nchi wamepewa masharti ili wapate misaada kukataa wameshindwa ila wanasingizia visingizio ambavyo havina kichwa wana miguu. Naona bajeti hii kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu itatusaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu na tuweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuongeza kodi kwenye mafuta kwa kweli ni mpango mzuri kama alivyosema Waziri tuweze kujitegemea na kuendeleza mpango wa miundombinu na umeme vijijini. Lakini, kwa wananchi hawajui, wao wanajua kwamba bei ya mafuta ikiongezeka ina maana kila kitu kinaongezeka. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, afafanue vizuri kwa nini wameongeza bei ya mafuta na ina faida gani kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, bei ya ongezeko la mafuta kwa kweli Serikali imefanya mpango wa kuongeza jambo moja ambalo wananchi walitegemea miaka yote huenda ikapanda sigara, bia ambapo baadhi ya wafanyabiashara watajificha ili wapate faida mara mbili wakidhania kwamba miaka yote bei inayopanda ni ya sigara pamoja na vinywaji.

Mheshimiwa Spika, naongelea suala la matrela: Suala la matrela kuongeza kodi kwa matrela ya nje itawaathiri sana wasafirishaji wa Tanzania. Kwa kweli makampuni ambayo anayasema Mheshimiwa Waziri asilimia kubwa ni makampuni yanayo-*assemble* tu, *chassis* kutoka nje, *deef* kutoka nje na kila kitu kutoka nje, na sasa hivi wamevamia Wachina nao wana-*assemble* matrela yao Tanzania, kwa kweli itaathiri sana usafirishaji. Naomba Serikali mliangalie suala hili kwa undani, kwa sababu bei yake ni tofauti kubwa sana, itawaumiza wasafirishaji nchini na kushindwa kufanya kazi hii ya usafirishaji, ambapo usafirishaji ni tegemeo kubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nje kwenye suala la riba: Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba riba imepungua mwezi Machi kwa asilimia 15 na pointi kidogo. Ni nia nzuri ya Serikali, lakini bado mabenki yetu pamoja na wao kupata faida kutokana na riba wanayopata kutoka Benki Kuu, lakini bado riba zao ni juu sana. Leo, mpaka mwezi Machi au mpaka sasa hivi imefika asilimia 21 mpaka 22 ambayo ni vigumu kwa mkulima au mfanyabiashara kwa sasa kuweza kulipa deni hilo kwa asilimia 22. Leo mfanyabiashara anayepata faida sana ni asilimia tano anapata kwa biashara yake. Kwa hiyo, kwa asilimia 22

Wizara na *BoT* ifuatilie suala hili ili kweza kuweka mambo sawasawa angalau wananchi wafaidike na mabenki yao.

Mheshimiwa Spika, mabenki mengi yanaingia nchini kwa mtaji mdogo, lakini kwa faida wanayopata kwa biashara ya Tanzania wanapata faida mara tatu mpaka mara nne na kuwaumiza wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza utegemezi wa pesa za kigeni, napenda kuipongeza *CRDB* kwa mpango iliyofanya wa kuweza kufanya biashara na Wachina na kulipa Tanzania *Shillings* na kule kupokea fedha ya Kichina, kwa hiyo imerahisisha kwa upande mmoja kutegemea sana pesa ya nje hasa dola katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iweze kuongeza mapato ya fedha za kigeni, ingeweza kutoa motisha kwa wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima. Serikali itoe motisha yaani kipaumbele cha hali ya juu, kama timu fulani iundwe kuwa-*support* watu hawa, kwa sababu ndiyo wanaingiza fedha ya kigeni nchini kwetu. Lakini Serikali kusema kweli haiwajali, wanapata vikwazo vingi sana katika kusafirisha hizo bidhaa nje hasa kwa wakulima. Kwa hiyo, ningepomba Serikali iangalie suala hili sana, wawape motisha ya kupunguza kodi ndogo ndogo au ikiwezekana hata kuwatolea kabisa ili kuwapa motisha kusafirisha bidhaa zetu nje ili wapate fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nje kwenye suala la sukari. Viwanda vyetu kama nilivyongea kwenye swali langu leo asubuhi, naamini Serikali ina hisa yake katika Kiwanda cha Kilombero pale na sidhani kama inakumbuka kuchukua pesa za hisa katika kampuni ile. Hii kampuni ni kubwa sana na kwa imani yangu inaweza kutosheleza sukari kwa nchi yetu kwa asilimia takribani sitini.

Mheshimiwa Spika, mabonde ya Ruhembe na Kilombero ni makubwa sana na viwanda vile vina uwezo wa kuongeza mitambo ya kuongeza kuzalisha sukari. Mara ya mwisho walileta mtambo wa kutoa *spirit* ambao waliweza kuuleta kwa ajili ya kupata faida ambayo inatokana na malighafi ya miwa inayozalishwa, kwa hiyo, ni *by-product* inayotumika kwa ajili ya kutoa *spirit* ambayo itawasaidia wakulima ambao miwa yao miaka yote inalala na wanakula hasara kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa miwa naona kama Serikali imewatenga au imewatupa mkono kwa sababu Serikali haiwangalii. Ukiangalia sana mlolongo wa kodi kwa wakulima wa miwa ni nyingi sana, mpaka *VAT* mkulima wa miwa analipa. Sasa mkulima wa kijijini mdogo mwenye heka kumi, *VAT* anajua wapi? Ningepomba Serikali iangalie suala hili, kuwaonea huruma wakulima wa miwa, kwa sababu sidhani kama baadhi ya mazao ya biashara wanalipa *VAT* kama wakulima wa miwa. Kodi ni nyingi sana, naomba Wizara



iangalie suala hili ili kuwalinda wakulima wa ndani na waweze kujitegemea kiuchumi na kupata faida ya kilimo cha miwa.

Mheshimiwa Spika, viwanda vyetu vya sukari vya K1 na K2 viko Wilaya ya Kilosa na Wilaya ya Kilombero, wao kimsingi wanakubali kuongeza mitambo, lakini nina shaka kuna maongezi kati yao na Serikali wapunguziwe gharama ya kodi au kitu fulani ili waweze kuongeza mitambo na kuweza kuvuna miwa ya wakulima wadogo wa Bonde la Ruhembe na Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala lingine la maendeleo ya nchi yetu. Kwa upande wa jimbo langu tumekwama kwa upande wa umeme, lakini nashukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa kuweka umeme kwenye jimbo langu, karibu asilimia 60 ya jimbo tumepata umeme. Nashukuru sana kwa hilo. Lakini, kuna baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri aliniahidi mwaka jana, kuna eneo kama Zombo - Lumbo, Ulaya - Kibaoni, Ulaya - Mbuyuni mpaka Muhenda, barabara inayotoka Kilosa kwenda Mikumi watatuwekea umeme, lakini mpaka sasa najua hali ya uchumi siyo nzuri, nategemea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na hili wazo la bajeti ya mwaka huu kupata fedha kwa ajili ya umeme vijijini tuweze kufanya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Wilaya ya Kilosa, jimbo langu pale katika Kijiji cha Kisanga tumepata mradi wa uzalishaji wa umeme ambao Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi na unaweza kutoa megawati nyingi na inaweza kusambaza umeme kwa wilaya nzima hata kwa Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Nishati na Madini iangalie suala hilo, kwanza tuanze wenyewe wa nyumbani kupata umeme *and then* wafuate wa mikoa jirani na wilaya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu suala la maji. Mji Mdogo wa Mikumi mradi wa maji umefikia asilimia 80, lakini mkandarasi amesimama kwa sababu hajalipwa pesa zake, na pesa anazodai siyo nyingi sana. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji amesema kwamba Wilaya ya Kilosa tutapatiwa shilingi milioni 440 kwa ajili ya kumaliza miradi ya maji ya vijiji kumi kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala hili kwa sababu wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais kuomba kura, aliahidi kwamba maji yatapatikana katika Mji Mdogo wa Mikumi na naomba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu lifanyike haraka ili mwenyewe Rais azindue na kuwakabidhi mradi huo wananchi wa Jimbo la Mikumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la barabara: Suala la barabara katika wilaya yetu katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 tuliambiwa tutakuwa na barabara ya lami kuanzia Kilosa mpaka Mikumi, lakini mradi huu kusema

kweli umesimama na sasa hivi hatujui itakuwaje, na sasa tunaingia uchaguzi mwingine mwakani. Naomba wanaoandaa Ilani ya Chama cha Mapinduzi wasisahau suala hili la kuweka barabara ya lami kuanzia Mikumi mpaka Kilosa hadi Ludewa. Hata hivyo, nashukuru kwa kuanza mradi huo kuanzia Dumila hadi Ludewa, watu wanafaidi barabara hiyo na usafiri umekuwa nafuu kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi ya kusema, napenda kuwashukuru sana Watanzania, naishukuru Serikali ya Tanzania kwa kazi nzuri inayofanya, kwa kipindi cha miaka minne katika Serikali yetu. Pia napenda kuchukua fursa hii, nilipoingia Bungeni mwaka 2011 kuna suala la watu wa Kijiji cha Malolo kuharibiwa mazao yao kwa kupasuka bomba la TAZAMA, tangu mwaka 2011 mpaka leo wananchi hawa pesa hawajalipwa na tathmini yao ilikuwa milioni 300.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya TAZAMA ambayo ni yenye bomba la mafuta imekataa kulipa pesa hiyo, sasa angalau milioni 50 watusaidie kutupa. Lakini nashukuru nimeongea na Naibu Waziri wa Nishati ameniahidi kwamba tupate barua kutoka kule na barua itakuja siku mbili hizi; na naomba tu asisitize tu kwamba wananchi hawa wapate haki yao, kwani leo mwaka wa nne, wengine wamekimbia miji yao, wameacha familia zao kwa ajili ya madeni ambayo yanawakabili.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuongelea ndugu zangu wanasiasa. Unajua kuna methali inasema; “kukiwa na wafalme watatu, nani atampanda punda?” Kwa hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Obama Ntabaliba atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Anthony Mbassa.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya, vilevile hotuba ya Waziri wa Nchi, Mahusiano na Uratibu Dokta Mary Nagu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kwapongeza kwa hotuba zao nzuri, jinsi walivyoziandaa na mipango mizima ya Serikali. Lakini vilevile naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, kwa miaka hii minne au mitano ambayo tumekaa na wewe umeonyesha kwamba hicho Kiti kinakufaa na unafaa uendelee nacho. Kwa kuwa wengine tuna uhakika wa kurudi na tunakuomba hii *label* ya hapa ya Obama usije ukatoa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuongoza nchi hii kwa amani, mpaka sasa hivi anapofikia muda wa kupumzika, na niwapongeze ma-candidate wote wa Chama cha Mapinduzi waliochukua fomu kuhakikisha wanatoa nia ya kuongoza nchi hii. Ukiwa na darasa ambalo watu wengi wana akili, watu wote wakipata A, huwezi kushangaa, kwa hiyo, ndiyo Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti zilizopita tumeshuhudia kwamba bajeti zinaandikwa vizuri kabisa na mipango yote inafanywa vizuri, tatizo tulilionalo bado ni makusanyo. Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba miradi ya maendeleo kama ya maji ambayo tulijivunia kwamba ungeweza kuwa umetimiza fedha ili miradi hii iweze kuisha, lakini kwa kweli wewe mwenyewe unayo taarifa kwamba fedha ulizozileta kwenye halmashauri zetu, mfano kama kwangu nilikuwa na miradi mikubwa ya karibu bilioni 3.4, lakini mpaka sasa fedha ambazo umeweza kuleta ni karibu bilioni 1.6. Kwa hiyo, bado tuna upungufu. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Waziri, unaposukuma fedha za mwisho, Wilaya yangu ya Buhigwe usije ukaisahau, tuna miradi ya kuweza kumaliza sasa ili wananchi wetu waweze kuendelea na maji yaweze kutoka.

Mheshimiwa Spika, tunayo miradi mikubwa mingine ya maji ambayo tulikuwa tumeiainisha ya Mnanila ambayo bado fedha zake tunazisubiri. Kwa hiyo Waziri, Wilaya ya Buhigwe naomba uiangalie kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa kutusambazia umeme, tunakupongeza Waziri, tunaomba uendeleo. Tunaomba fedha za wakandarasi zinazokwenda ziendeleo ili waweze kumaliza hiyo miradi tuliyonayo. Asilimia 65 ya jimbo langu ya miradi ya umeme inaenda vijijini, kwa hiyo ni kitu kizuri na ningepomba mkandarasi aliyeko pale sasa aweze kwenda kwa speed inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, napongeza makampuni ya mawasiliano, *Vodacom, Tigo, Zantel, Airtel*, wamefanya kazi nzuri sana kwenye Jimbo langu la Manyovu. Jimbo langu sasa hivi lina coverage tunaenda asilimia 90, lakini mwanzo kabla ya hapo tulikuwa na asilimia 40, kwa hiyo tumetoka mbali na mpaka sasa tuko mbali.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, makampuni haya yameingia mikataba na vijiji, kuna minara ambayo wana mikataba na vijiji wanalipa kila mwaka, lakini nilikuwa naongea na Mwenyekiti wa Kijiji changu cha Mnanila, ameniambia mpaka sasa wanadai karibu milioni 27. Kwa hiyo, makampuni haya hayajalipa wale walioingia mikataba, aidha wananchi na vijiji. Kwa hiyo tungeomba hilo nalo ulisukume ili waweze kuwalipa ili mipango ya Serikali za Vijiji iweze kwenda vizuri. Kwa hiyo, bado pale tuna

madeni mengi, hivyo tunaomba kwa kweli hilo *Vodacom* na *Tigo* waweze kulipa kulingana na mikataba, wamekuwa sehemu zingine miaka mitatu minne hawajalipa, kwa hiyo mambo ya kuanza kupelekana Mahakamani siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali imeendelea kusukuma walimu na jimbo langu walimu wengi wamekuja, nawashukuru kweli kweli. Lakini najjuliza kwa nini sasa hizi stahiki zao hamuwapi? Unapomleta mtu kama mwalimu, unampangia mpaka Kigoma, anakuja Buhigwe, anakuja Manyovu, halafu unakuta kwamba, zile stahiki zake hujampa, kwa kweli hamuwatendei haki. Sasa hivi, Wabunge tunachangia walimu ili waweze kuendelea kuishi pale! Sasa nafikiri ni kitu ambacho kwa kweli, Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba, makusanyo yako sio mazuri, hebu jitahidi hili la walimu uweze kulimaliza mara moja. Ukiacha matatizo ya wao kupandishwa madaraja, wako wengine wa 2011 hawajapandishwa madaraja, lakini hii ya kujikimu nayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, niipongeze tena Serikali ilitupatia Wilaya yetu ya Buhigwe, lakini watumishi wale waliohama kutoka Wilaya ya Kasulu hawajalipwa fedha. Mpaka sasa hivi wanadai halmashauri karibu milioni 260. Sasa ni kitu ambacho watumishi pale wanasikitika. Tunaomba kwa kweli, Wizara ya Fedha iweze kupeleka fedha ili halmashauri waweze kulipa. Watumishi wamekaa pale wamefanya kazi nzuri, lakini wanadai Serikali hela za uhamisho kutokea Wilaya ya Kasulu kuja Buhigwe.

Mheshimiwa Spika, tunayo madeni Wizara ya Kilimo, Naibu Waziri nimemuona pale! Naibu Waziri aendeleo kushughulikia mapunjo, wakulima wangu karibu 430 walipunjwa na wanadai Dola 74,00, kwa hiyo, ni vizuri suala hili analijua, tungeomba wananchi waweze kulipwa mara moja na alishughulikie kwa *speed* ya kutosha. *Speed* anayoitumia sio nzuri, inawakatisha tamaa wakulima wangu wa kahawa wa vijiji vyote vinavyozunguka Jimbo la Manyovu na Jimbo la Kaskazini, kwa hiyo, ni vizuri sana hilo nalo aweze kuliona.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo madai ya vibanda vya Mnanila; na ni mazungumzo kati ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya *TAMISEMI*, tunaomba hayo mazungumzo yaendeleo haraka ili wale wakulima wenye vibanda 120 wanaodai karibu milioni 900 ili nao waweze kulipwa na hilo suala liweze kuwekwa vizuri, tulifute kwenye vitabu vyetu. Kwa hiyo, kwa kweli ningepomba hayo yaweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, upande wa Polisi; sisi tuko mpakani na kwa kuwa, kuwa mpakani sasa hivi wakimbizi wanaingia wengi sana na tunavyo Vtuo vingi vya Polisi ambavyo tumevianzisha, tunaishukuru Serikali imetuwekea maaskari pale, lakini vitendea kazi bado ni tatizo, hata pikipiki kwenye baadhi ya vituo hamna. Kwa hiyo, tungeomba kwa kweli maeneo ya pembezoni, ya mipakani

usalama uweze kuimarishwa vizuri, hali sio nzuri, kwa hiyo, tunawaomba kwa kweli, vituo viko sita, angalau kila kituo kipate pikipiki moja. Tukiweza kupata, ziko pikipiki za milioni saba, milioni 42 unakuwa umemaliza mpaka mzima, umeulinda, umeenda vizuri. Kwa hiyo, ni vizuri kwa kweli, mengine muweze kuyamaliza kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, uko utaratibu ambao sasa mkandarasi ambaye anasaini fedha milioni 50 kwenye kandarasi ndani ya Wilaya, *documents* hizo lazima ziende kwa Mwanasheria Mkuu. Mimi nilikuwa nashauri, hii milioni 50 ukiacha watu wa mkoani wakasaini, tatizo ni nini, ili Mwanasheria Mkuu aanze kusaini milioni 200, 500, 600! Milioni 50, barua inakuja mpaka Dar es Salaam, miezi mitatu, minne bado wanafuatilia mkataba kusainiwa! Nafikiri sio kitu kizuri, Serikali iweze kubadilisha huo utaratibu. Milioni 50 ni kitu kidogo ambacho hata Mkurugenzi mwenyewe anaweza kusaini.

Mheshimiwa Spika, nipende kukushukuru tena. Upande wa afya tunayo mikataba ambayo tumeingia na *Heri Mission Hospital*, tunayo Bihalu, tunayo Kalege. Kwa hiyo, ni vizuri nayo hiyo mikataba kwa watoto na wazee iweze kuheshimika. Halmashauri yangu inajua, kwa hiyo, nasisitizia kwamba, waendeleo kuwalipa, ili huduma za wazee na watoto ziweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, sina mengi. Nakushukuru sana, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Manyovu, tunaendelea nao vizuri, wao wanajua, sitaki kusema sana hapa Bungeni, kazi yangu wanajua ya kimyakimya. Mungu abariki Bunge hili na Tanzania nzima, amina.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa moyo wa dhati kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia jioni hii katika suala muhimu lililoko mbele yetu. Lakini, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia pumzi ya uhai na uzima kuweza kutimiza majukumu yangu ambayo niliyaomba kwa wananchi kama Mbunge.

Nawashukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo kwa moyo wa dhati kadri walivyoniunga mkono na kwa hatua tuliyoifikia, nazidi kusema kamba ni ileile, uzi ni uleule, tutahakikisha Biharamulo yetu tunazidi kuivusha.

Mheshimiwa Spika, wasishangazwe na maneno ya juzi ya *Comred* Kinana na kijana wake Nape, hao ni wa kupita! Ninarudi, majibu yapo na nitawaeleza nini kilichopo na takwimu tunazo ndani ya halmashauri yetu na nyingine zipo kwenye Ripoti ya CAG, kwa hiyo, hatuna jambo la kutia shaka. Nawashukuru sana wana Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie na suala zima la BVR. Suala hili la uandikishwaji katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limekuwa tatizo kubwa sana, badala ya kuwa hamasa kwa wananchi, imekuwa sasa ni kero ambayo haina mwanzo wala mwisho. Ni kweli, nimeenda kujiandikisha jimboni kwangu tarehe 21 Mei, lakini nilipata bahati ya kuzunguka hata maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tusiangalie tu tatizo la kwamba, vifaa vimeharibika na nini, lakini vilevile kuna kushuka kwa morali kwa watendaji wetu. Ni kweli Serikali ilipanga kiwango cha kuwalipa na wao waliomba kazi, wamepewa, lakini kazi hiyo, imefika mbele ya safari sasa imekuwa ni yale maneno ya mzigo mzito watwishe wale jamaa fulani. Ni kweli, hawana namna ya kuweza kuacha ile kazi, lakini yale malipo jamani ni kidogo na ndio maana hata hiyo speed imeteremka! Katikati hapa walikuwa wanaweza kuandikisha watu 120, 150 kwa siku, lakini imefika mahali wamedorora.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba tu nifikishe haya malalamiko yetu kwa Waziri mwenye dhamana, yupo hapa na yeye anatusikia, tumeandika na maelezo, lakini tutafute njia mbadala ya kuonesha jinsi gani Tume itaweza kuwasaidia watu hawa. Nilipolalamika hapa na kushukuru Mheshimiwa Spika, Kiti chako kiliweza kunipa nafasi na Waziri alinisikiliza na Mkurugenzi wa Tume alikwenda kule Kagera, lakini kweli maeneo mengi watu wameachwa bila kuandikishwa. Mpaka hivi sasa kila uchao wa Bunge tunapata *text messages* za watu ambao hawajajiandikisha. Tunaomba utaratibu ufanyike kabla ya mashine hizi hazijahama katika mikoa yetu huko tuliko, tafadhali watu hawa warudiwe waandikwe! Ni haki yao ya kimsingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Conchester ametangulia kulieleza kwa uwazi na ukweli. Tumekuta kuna sehemu watu wana vile vipande vya 2010 wameshiriki katika uchaguzi mkuu, mwaka 2014 wameshiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, lakini leo hii jambo la ajabu wanakataliwa! Sasa haijulikani kwamba, hapa katikati walibadilisha uraia au imekuwaje na wakati vyombo vyetu vya uhamiaji vipo vinafanya kazi kila uchao! Naomba tafadhali haki hii ya kuandikishwa kwa kila raia wetu ni ya msingi na ni ya kikatiba, wapewe haki hiyo na watendewe haki.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala moja ambalo limeongelewa na mjumbe hapa kuhusu tatizo la maji au mradi kutapeliwa bilioni 1.4 katika Kata ya Nyakahura ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wangu wa Halmashauri wa Chama Cha Mapinduzi na mke wake akiwa Diwani. Suala hili ni tatizo kubwa sana sana; na kwa kipindi chote cha miaka 15 mradi huu umekuwa hauwezi kuleta matunda. Ajabu na kweli, mradi ambao umefunguliwa mara mbili, Mheshimiwa Wassira anazo taarifa alivyopita katika jimbo langu alipewa kufungua mradi huu, lakini na kiongozi wa mbio za

mwenge na yeye alipewa fursa hiyo. Sasa mradi unaofunguliwa mara mbili unatia wasiwasi, tija yake iko wapi?

Mheshimiwa Spika, lambo limechimbwa pale, DP47 zimekwishakujengwa pale, mashine ya *Lister Peter* ilikuwa imeishatafutwa kuwekwa pale, lakini mpaka sasa umekwama!

Mheshimiwa Spika, tunapoongea haya, na mimi nashukuru Mwenyezi Mungu kwamba, asubuhi hapa wakati namuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu swali la Mheshimiwa Mbowe, ushirikishwaji wa Madiwani na kusimamia miradi, dhana hii tunaposema kwamba linapita kwenye *process* za manunuzi na nini, Mwenyekiti wa Halmashauri anajua! Haiwezekani leo hii watu wakose maji, pale Kata ya Nyakahura wanahangaika akinamama sasa imekuwa ni shida tupu, watoto shuleni usafi hakuna, tunalifumbia macho! Naomba tafadhali Serikali, hili sio suala la chama wala la nini, mahitaji ya maji ni kwa ajili ya watu wote na mahitaji ni ya wote! Naomba Serikali ichunguze ubadhirifu kama upo umeanzia wapi na ukoje na watu wachukue hatua stahili.

Mheshimiwa Spika, suala zima la afya katika Mkoa wetu wa Kagera, ni kweli Sera ya Afya inasema akinamama wapate huduma bure, watoto wadogo na wazee, lakini jambo ambalo kwa kweli utekelezaji wake umekuwa ni mgumu, haupo. Leo hii katika Mkoa wa Kagera tunazo hospitali mbili tu za Serikali, Bukoba Hospitali ya Mkoa na Nyamiyaga iliyopo Wilaya ya Ngara, zilizobaki zote *voluntary agency* au *DDH* zote ni za makanisa!

Mheshimiwa Spika, hospitali hizi nimekuwa nikongea hapa kwenye bajeti yangu kama Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, upatikanaji wa dawa na vitendanishi na vifaa tiba ni tatizo. Tukiongea hapa basi, watu wanafikiri hili jambo limekwisha, lakini kule ni matatizo! Na mbaya zaidi sasa ni pembezoni, na watu wengi wanaowekeza hata kama ni haya maduka muhimu ya dawa wanapenda wawekeze mjini, nani aende kuwekeza kijijini, inakuwa ni kazi.

Mheshimiwa Spika, tumeomba na tumesema kwamba, basi angalau hata hili suala la kupata Mfumo wa Pamoja wa Afya (*Universal Health Coverage*) ufanyiwe kazi haraka ili kusudi uweze kuwanusuru watu hawa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hali kule ni mbaya, sio Hospitali ya Biharamulo tu, ni sehemu zote ni mbaya! Tunaomba tafadhali watu hawa kama sera ilivyo, basi itekelezwe kwa matendo, isitekelezwe kwa maneno, watu hawa wapate huduma. Vinginevyo tutakuwa tunaongelea habari za vifo vya akinamama na watoto, takwimu zisizoshuka! Takwimu zenyewe tunazopata ni zile ambazo tu zinatoka kwenye vituo vya kutolea huduma, lakini kule vijijini wapo watu wengi

wanapoteza maisha, hawawezi kufika kwenye vituo vya afya, hawawezi kufika kwenye zahanati na hawawezi kufika kwenye hospitali! Ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Jimbo langu la Buharamulo, tunategemea mgonjwa akipata *complication* atoke kilometa zaidi ya 100 aje Hospitali ya Wilaya. *Ambulance* zilizopo zimechoka na nimewahi kuomba hapa *ambulance*, Mheshimiwa Waziri akaniambia halmashauri imeishatenga pesa, nimekwenda pale hamna kitu! Nikafuatilia kikao cha Bodi kilichokuwa kinakaa kwamba kuna mpango huo na ajenda hiyo, ilikuwa hakuna! Sasa tunapokuja kueleza matatizo ya wananchi, tunakuja na mambo ambayo tunatoka nayo kwenye *ground* ambayo ni ya msingi na yanaeleweka. Tunaomba tafadhali masuala haya muyaangalie vizuri tunapo ya-*address* hapa, yana umuhimu na ni msingi kutokana na maeneo tunakotokea.

Mheshimiwa Spika, mgonjwa atoke Biharamulo kwenda Bugando, kilometa 250, wangapi wenye uwezo wa kufika? Ni tatizo! Kwa hiyo, naomba hizi huduma tulizozieleza ziweze kushushwa ngazi kwa ngazi, ili kusudi watu hawa wapate huduma inayostahili.

Mheshimiwa Spika, nimevisoma vizuri vitabu viwili hivi vya Mheshimiwa Waziri, kuna suala la mafao ya wazee limeongelewa. Kwa kweli suala hili sasa limekuwa ni tatizo ambalo kila mara tunaliongelea, lakini halipati ufumbuzi, halipati jibu.

Mheshimiwa Spika, tumefanya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, inabainisha kabisa idadi ya wazee waliopo, wastaafu waliopo, lakini mpaka sasa bado Serikali inasema kwamba iko katika mpango na maandalizi ya kuanza kuwatambua, hawa watu itawatambua lini?

Mheshimiwa Spika, kama hakuna juhudi za makusudi za kuwatambua wazee, ni bora tuwaambie kabisa kwamba suala la kuwatambue wazee limekuwa gumu, haliwezekani! Leo hii tunasema kwenye hospitali zetu kuwe kuna madirisha ya kuwahudumia wazee, ni hospitali chache sana ambazo zinatekeleza suala hili, lakini wanapofika pale tatizo linakuja anaenda kuandikiwa dawa, mwisho wa siku akienda *pharmacy*, anaambiwa katafute dawa hizi kwenye duka la dawa hapa hatuna! Huyu mzee ataenda kuzipata wapi? Pesa amepata wapi?

Mheshimiwa Spika, sambamba na wastaafu, ni kweli, wastaafu wetu wana maisha magumu sana na hali ngumu sana. Nasikitika kuna mstaafu mmoja kwangu pale nikimuona anaendesha baiskeli ambayo haina *mud-guard*na alikuwa mtu mzito sana Serikalini, inanisikitisha sana, leo inafika mahali hata hiyo *pension* yake mnayoisema 50,000 mnaongeza mpaka 85,000 anaenda kwenye duka la dawa, pale sio chini ya 20,000 ataiacha kupata



dawa, na hizo za kwake yeye mwenyewe na uzee wake, bado mwenzake kama yupo, bado watoto ambao ameachiwa, ameletewa kulea, na unajua hawa ndio wanaolea!

Mheshimiwa Spika, kweli kabisa haya mapendekezo ya mafao ya shilingi 85,000, naomba tupige moyo konde, hayawatoshi. Bora tusogeze hata iwe 150,000/= walau waanzie na yenyewe wapate katika muda muafaka. Tofauti na hapo tutazidi tu kuwapaka mafuta kwa mgongo wa chupa, hakuna linaloendelea.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa la ushughulikiwaji wa mirathi. Kuna watu kweli wamepoteza maisha yao wakiwa kazini wanaitumikia nchi hii, lakini imefika mahali mpaka sasa haki zao hazipatikani. Kila makaratasi yakiletwa hawapewi majibu. Sasa tunashindwa kuelewa hawa watu wafanyeje, wapateje haki zao? Unatumwa Mbunge kama Mbunge unapeleka sehemu husika, anayejibiwa sio Mbunge, anayejibiwa ni yule mwenye anuani, lakini cha ajabu hapati majibu ya nini kinachoendelea!

Mheshimiwa Spika, sidhani kama ni kosa kubwa sana na hakuna anayeomba na hakuna ambaye amefunga ndoa na Mungu kwamba, ampoteze mwenzie aingie katika maisha magumu kama hayo! Lakini maadam sheria inasema huyu mtu kapata tatizo hili au kapoteza maisha akiwa katika sehemu ya kazi, basi alipwe hizo stahili. Hebu tuwatendee haki na wenyewe tuone kwamba ni haki yao ya msingi, waweze kulipwa mirathi waone jinsi gani watakavyosaidia familia zao.

Mheshimiwa Spika, leo hii inageuka kwamba Wabunge tunapokwenda majimboni kila mmoja anakuja na kueleza, mimi nina tatizo hili, nimepeleka *documents* zangu! Mtu kutoka Kagera, Biharamulo mpaka Dar es Salaam ataweza wapi! Maisha ya Dar es Salaam ameshindwa yenyewe kuyamudu, atafanya nini?

Mheshimiwa Spika, ningepomba Serikali ifikirie ni jinsi gani ya kuwasaidia hawa watu wanaoshughulika na mambo ya mirathi, ikiwezekana, basi iteremshe dawati mpaka kwenye ofisi zetu za wilaya huku, ili kusudi suala hili liweze kufanyiwa kazi kwa uharaka na hawa watu waweze kupata stahili zao.

Mheshimiwa Spika, suala zima la vijana tunasema hawana ajira, ni kweli, na wengine wamejajiri, lakini jinsi gani tunavyoweza kuwasaidia katika ajira zao. Kumekuwepo na suala la hivi karibuni la kubadilisha namba za pikipiki, kitu ambacho sasa imekuwa ni kazi kubwa. Vijana wameshajiandaa na nini, lakini wanapiga moyo konde ili yeye apate hela ya kumlipa tajiri na ya kwake, apate na nauli ya kwenda Makao Makuu ya Mkoa TRA ndiko akabadilishe pikipiki; kule nako ndio hivyo tena danadana nyingi, inakuwa ni kazi.

Mheshimiwa Spika, niombe Mheshimiwa Waziri, katika hili uweze kuwasaidia hawa vijana. Tafadhali kama unaweza kuteremsha *mandate* kwenye ofisi zetu za *TRA* za Wilaya, najua zinafanya kazi vizuri, hawa vijana wasaidiwe kwa utaratibu uliopo, lakini vilevile tunaomba basi elimu ya mlipa kodi iwe inatolewa. Kuna wengine kweli wanakuwa hawaelewi kinachoendelea ni nini, lakini wanalalamika zaidi, lakini kama elimu kwa mlipa kodi itatolewa na wakaelezwa umuhimu, nafikiri suala hili litakuwa rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, hawa vijana tunaweza tukawagawa katika makundi mawili, wapo wanaomiliki vyombo vyao binafsi na wapo ambao wanatumikia vyombo vya watu wengine. Kwa hiyo, wote hatuwezi kuwaweka katika haki sawa tukapunguza au tukaongeza kwa kufikiria wote tu wamejiajiri, hapana! Naomba hilo tuliangalie kwa karibu ili waweze kusaidiwa katika nyanja hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni wakandarasi wetu. Ni kweli, kumekuwa na ukata wa kuwalipa wakandarasi. Kuna kipindi hapa tulieleza hali iliyokuwa imejitokea mashuleni, wazabuni wameshindwa kulipwa hela zao mpaka shule zimefungwa! Watu wakasema hapana, hii sijui wame-exaggerate, lakini hali halisi ndivyo ilivyo! Leo hii maeneo ya ujenzi wa uendelezaji wa miradi, kwa mfano barabara, nina barabara ya kutoka Bwanga mpaka Kalebeze kilometa 68; nashukuru wakandarasi walikuwepo barabarani, lakini wamesimama hawajalipwa pesa yao. Wanaposhindwa kulipwa pesa yao, hasara wanayoipata ni kubwa sana na Serikali inaingia mzigo mkubwa sana, lakini bado wapo wale wananchi waliopitiwa na mradi huo hawajalipwa pesa zao kuanzia Bwanga mpaka Kalebezo!

Mheshimiwa Spika, naomba tafadhali Serikali ifanye mpango wa makusudi wa kuhakikisha wanawalipa hawa wananchi fidia zao ili kusudi basi nao waishi kwa amani, maadam wameishapisha ujenzi unaoendelea sasa hivi. Vivyo hivyo ningeliomba kwa Nyakanazi ambako tunategemea kujenga *power station* pale, lakini bado kuna mzani utajengwa pale na vilevile barabara ya kutoka pale kwenda mpaka kwa jirani zangu pale Buyungu kwa *Engineer Chiza*, nao vilevile wanaopitiwa basi na mradi huu waweze kulipwa, ili kusudi maisha yao yaendelee kuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Ahsante!

**MHE. DKT. TEREZYA P. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti. Lakini, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha mahali hapa na kuweza kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii. Vilevile niwashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Mama Nagu, Waziri aliyetoa Hotuba ya Mipango na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya, kwa Hotuba nzuri walizotuletea na bajeti nzuri ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa moyo wa dhati kabisa kwa sababu bajeti hii imezingatia vipaumbele vichache. Imezingatia miradi ambayo tunaendelea nayo, miradi ya umeme, miradi ya maji, miradi ya barabara. Lakini niombe tu Serikali kwamba, iweze kukusanya mapato ya kutosha ili miradi hii sasa iweze kukamilika, tusije tukafikia mwaka mwingine tena wa 2016/2017 bado tunazungumzia miradi hiyohiyo.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa maji, kwa sababu, ya mabadiliko ya tabia ya nchi, maji baridi sasa hivi yanapotea kwa kiwango cha juu sana, kwa kasi. Basi, niombe kwenye miradi ya maji vilevile waongeze umuhimu wa kuweka maji kwa njia ya uvunaji. Kwa hiyo, mabwawa yachimbwe ili maji mengi yaweze kuvunwa na watu hatimaye waweze kupata maji ya kutosha, kwa sababu hii miradi ya kuchimba visima itafikia wakati hata hivi visima virefu havitakuwa na maji, kwa hiyo, lazima tuwe na mkakati mbadala wa kuhakikisha kwamba, maji yanavunwa, mvua chache tunazo tunazozipata maji yanavunwa ili kuweza kuyahifadhi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuondoa kodi kwa bidhaa muhimu. Katika kitabu cha bajeti, ukurasa namba 5, Serikali imeweza kuondoa kodi kwenye pembejeo, zana za kilimo, zana za uvuvi, lakini pia na vifaa vya tiba. Vitu hivyo vinawagusa wananchi moja kwa moja hasa wale ambao ni maskini, wananchi wa vijijini. Kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wakipunguziwa zana za kilimo, hii itawawezesha wao hata kuweza kununua matrekta, kununua mbolea na dawa ili waweze kulima vizuri zaidi. Kwa hiyo, niipongee Serikali kwa hatua hiyo muhimu. Niwaombe tu kwamba tunapozungumza hapa ndani kwamba tumepunguza kodi, basi ufuatiliaji uwe wa kina kuhakikisha kama kweli bidhaa hizo zinakuwa na bei ya chini ili wananchi wote hasa vijijini waweze kupata vifaa hivyo na kuongeza uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee madeni ya mifuko ya hifadhi. Nakiri kabisa kwamba Serikali iliweza kuchukua pesa kwenye hifadhi zetu za jamii na kuweza kuendeleza miradi mbalimbali, lakini madeni hayo sasa yamekuwa makubwa kiasi cha kutishia mafao ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba madeni hayo yanalipwa ili wastaafu waweze kupata mafao yao kwa wakati kwa sababu yanapozidi kuongezeka basi hata na wastaafu nao wanapata tabu kupata pesa hizo hasa wakati wa kustaafu unapofika. Niiombe Serikali yangu sikivu iweze kurudisha pesa hizo ili kulipa madeni hayo kwa wakati ili wastaafu wanapofikia muda wa kustaafu waweze kupata mafao yao bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuongelea ni suala la pensheni kwa wastaafu pamoja na mafao ya wazee. Sote tunajua kwamba wazee hao wametumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa na maendeleo mengi makubwa tunayoyaona sasa hivi tumeyapata kwa sababu yao. Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali ihakikishe kwamba hao wastaafu pamoja na mafao ya wazee wayapate. Lakini vilevile ongezeko hilo la kufikia shilingi 85,000 mimi binafsi naona bado ni dogo, basi tungeweza kujikwamua tuongeze angalau ikafikie 100,000 ili wastaafu hao waweze kuishi na wanapoenda sehemu mbalimbali kupata mahitaji yao kwa mfano hospitali na sehemu nyingine basi pesa hizo ziweze kuwasaidia hata wawekeze kwenye miradi midogo midogo ili waweze kuwa na maendeleo. Kwa hiyo, mimi naomba tujitanue kidogo angalau tuongeze hizi pesa ili wastaafu pamoja na wazee waweze kupata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la tozo za mafuta ni suala jema kabisa kwa sababu tumeishaambiwa pesa hizo zitaenda kwenye miradi ya umeme na miradi hii ya umeme ikisaambaa katika vijiji vyote, basi tutakuwa tumepunguza sana tatizo la kutumia nishati ya kuni. Lakini, mimi naomba elimu hapa itolewa kwa wananchi ili hili lieleweke vizuri. Vilevile wote wanaohusika na vifaa vya kusafirisha bidhaa mbalimbali, kusafirisha abiria, kusafirisha bidhaa zetu mbalimbali pia nao wapewe elimu ili wasije wakaanza kuongeza tu nauli na kuongeza gharama za bidhaa mbalimbali kwa sababu hiyo itawaumiza walaji wa mwisho ambao hasa wako vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba hili Mheshimiwa Waziri alieleze vizuri kabisa lieleweke kwa sababu nia yake ni nzuri ya kupata umeme. Pia, katika utekelezaji, basi ufuatiliaji uwe wa makini sana ili kuhakikisha kwamba hata kama ni nauli inaongezwa, basi iongezwe ile inayopaswa na siyo kuongeza tu nauli kiasi ambacho wananchi wanaweza kupata matatizo. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo kwa makini.

Mheshimiwa Spika, vilevile iangalie vyanzo vingine vya mapato, kwa sababu tunaona sekta nyingine, kwa mfano sekta ya utalii bado haijatumika vizuri. Kwa hiyo, tukiongeza tozo kule kwenye utalii tutakuwa tumeongeza pato na hivyo kuinua viwango vyetu vya uchumi. Pia, kwenye sekta ya ardhi na majengo bado sekta hii haijatumika vizuri, tuna sekta nyingine ya mifugo, bado pia nayo haijatumika vizuri. Kwa hiyo, mimi niombe kabisa Serikali kwamba iweze kuangalia maeneo haya vizuri kabisa ili tuweze kupandisha uchumi wetu na kupata Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri naona na Naibu Waziri wa Kilimo pia kwa sababu kuna wakulima wengi wa mahindi mpaka sasa hivi bado hawajalipwa, ingawa Serikali imejitahidi kuwalipa wakulima, lakini bado wakulima wengine hawajalipwa fedha zao.

Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali ifanye mbinu za makusudi kabisa kuhakikisha wakulima wanalipwa pesa zao ili waweze kujikimu na wanapoingia kwenye msimu mwingine wa kilimo waweze kununua pembejeo hizo na kujikumu katika mahitaji mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mimi nichukue masikitiko yangu kwamba katika hotuba hii sijaona hasa msisitizo mkubwa wa hifadhi ya mazingira. Kwa sababu nchi ambayo haihifadhi mazingira inapatwa na matatizo makubwa sana na hatimaye umaskini unakuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha, basi angalie aliweke hili katika msisitizo ni namna gani wananchi wanaweza kushirikishwa kwenye bajeti hii ili kuweza kuhifadhi mazingira vizuri na kuifanya nchi yetu iweze kuwa na uchumi mzuri. Kwa sababu unapohifadhi mazingira sekta nyingi zinakuzwa na hivyo kuweza kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, mimi niseme ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na mimi ili niongee kidogo yanayohusu bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniweka hai hadi leo. Nawashukuru vilevile watu waliokuwa wanafuatilia kuhusua afya yangu, mmojawapo ni Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, na wewe binafsi Mheshimiwa Spika ulinijali; na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wilaya yangu ni wilaya mpya, na ujenzi wa wilaya mpya una changamoto nyingi sana. Sasa kinachoshangaza kuna bajeti zingine sisi wala hatufikiriwi, mfano, fedha ya maendeleo, mimi nafikiri hii fedha ya miradi ya maendeleo ilitakiwa moja kwa moja Serikali iingie. Mheshimiwa Rais alitupa ahadi mwaka 2010, alisema kuwa wilaya mpya zote atahakikisha zinajengwa kwa haraka ili zilingane na wilaya za zamani, lakini miradi yote inaenda inasua sua, tutalingana lini na wenzetu wa zamani!

Mheshimiwa Spika, nikiangalia suala barabara, Mheshimiwa Rais alituaahidi kuwa barabara inayotoka mkoani itaunganishwa mpaka ifike wilayani kwa kiwango cha lami. Sasa mpaka sasa hiyo ahadi haijatimizwa na haijulikani lini itatimizwa, matokeo yake wananchi wanalalamika, wanashindwa wafanye nini, mazingira siyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, basi tunaomba na sisi tuwekwe kama wilaya zingine, ni kilometa 60 tu kutoka Singida Mjini kwenda Makao Makuu ya Wilaya, lakini barabara siyo nzuri sana, tunaomba tuwekewe lami kama Mheshimiwa Rais alivyosema.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kutoka Msingi, Yulansoni, Lelembwe, Kitumbili hadi Iguguno, hiyo barabara ilishakufa. Tuliomba tupewe angalau bilioni mbili tuweze kujenga tukamilishe. Lakini fedha tuliyopewa ni milioni 450 tu, kwa hiyo, hazidakidhi haja, wananchi wanalalamika wanaona kama wametengwa; na kama tunavyojua utamaduni wetu, Mheshimiwa Rais akitamka kitu huwa kinatimizwa. Kwa hiyo, tunaomba hii Mheshimiwa Waziri, uje uwasaidie hao, ikiwezekana twende wote, uende uone jinsi hao wananchi wanavyohangaika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la maji; Wilaya yetu imetokana na Bonde la Ufa, kuna miamba migumu ambayo haitoboleki. Kwa hiyo, tunachoomba Mheshimiwa Waziri atufikirie huko nako, miradi hii ili ianzishwe maji yatoshenze wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna Bwawa la Mwangeza, hili bwawa lina zaidi sasa ya miaka kumi halikamiliki, ujenzi wake unasuasua. Tunaomba likamilishwe kwani wananchi wa Mwangeza watapata na maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna mradi mwingine wa maji wa Msingi umwagiliaji, umeachwa zaidi ya miaka kumi haukamiliki, watu walijitoa, wengine wakaacha na ardhi yao ili mradi uendelee. Huu mradi bado haujakamilika unasuasua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hii miradi inayokusua, lakini wananchi wana mategemeo kutoka Serikalini. Serikali ndiyo tegemeo lao, Mbunge unayetumwa ili uweze kufikisha kero zao unapwaya, unaonekana wewe huwa hutoi hizo kero zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aangalie sana hizi wilaya mpya zina matatizo na changamoto ni nyingi mno.

Mheshimiwa Spika, suala lingine; wananchi tuliwahamasisha kujenga maabara. Wilayani kwangu maabara zilishajengwa zote, lakini sasa kinachoendelea Serikali ilete sasa vifaa vya kukaa mle maabara ili maabara zianze kufanya kazi. Namuomba Mheshimiwa Waziri aangalie hilo ni suala ambalo tunataka tuboreshe elimu yetu. Kwa hiyo, hizi maabara hazikujengwa kama mapambo, zianze kutumika sasa, zipelekewe mahitaji yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, lingine, nashangaa sana, tuliwahamasisha wananchi wajenge vituo vya afya na zahanati, wananchi wamefanya hivyo katika Wilaya yangu ya Mkalama, wamejenga maboma yote yalishamalizika, lakini kumalizia

bado. Mfano, Iguguno kuna kituo cha afya kizuri walichojenga wananchi, lakini kimebaki hivyo hivyo, hakijapauliwa, tunaomba fedha Serikalini, Serikali haitufikiri. Naomba sana hili suala la vituo vya afya, tafadhali tunaomba ulikamilishe. Kwa sababu tuingojea eti mpaka mwakani tena, maana yake wananchi watakuwa wanazidi kupata tabu, matibabu hawatapata kisawasawa. Sasa hivi vituo vya afya vyenye madaktari wanafanya hata operesheni, sasa sisi hata operesheni za wagonjwa hamna, kufunga vidonda hamna, jengo limesimama tu.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, ahakikishe hivi vitu vinatendeka ndiyo turuke hatua nyingine, tuliobaki nyuma, naomba utusaidie *tusi-lag behind* katika maendeleo, maendeleo yanatakiwa yaende sambamba na watu wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, vilevile nashukuru sana sana, nawashukuru wananchi wangu, nawaomba wawe wavumilivu kama walivyoniwumilia, nimerudi ili tushikane tena katika kujiletea maendeleo ya Wilaya yetu mpya ya Mkalama. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na namshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kunipa uhai, neema yake, ulinzi wake na fadhili zake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwa kuliongoza Bunge hili vizuri kwa miaka mitano ambayo tumekaa katika Bunge hili, umekutana na changamoto nyingi, lakini umekuwa jasiri na mpaka ukatufikisha hapa, mimi nakuombea sana kwa Mwenyezi Mungu azidi kukupa afya njema na uhai pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wanawake wa Dodoma pamoja na wananchi wote wa Dodoma kwa ushirikiano mkubwa sana niliopata katika kipindi changu cha kazi. Nawapenda, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema na nitakaporudi kwao naomba ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambazo zimefanywa na Serikali ya awamu ya nne, wamefanya kazi nyingi nzuri zinazoonekana na hii ni sifa kwa Chama cha Mapinduzi na ni sifa kwa Watanzania ambao ndiyo wanaofaidi matunda haya.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wengine kwa dhamira safi ya kuamua sasa Serikali yetu ianze hatua ya kukusanya mapato na mwisho wa siku tufikie hali ya kujitegemea wenyewe bila kutegemea wahisani.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Waziri imeeleza mikakati ambayo imeweka kwa ajili ya kuanza sasa na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu. Nchi zingine ukienda huwezi kununua kitu wala kuuza bila kutoa *receipt*, basi ifike wakati ambapo Watanzania tunaponunua na kuuza tudai stakabadhi, hii itasaidia sana kujua mapato ya nchi yetu na hasa mapato ya ndani na pia itatusaidia kufika kule tunakopenda kwenda.

Mheshimiwa Spika, nimesoma mikakati mizuri sana katika hotuba ya Waziri na naamini kwamba huko ambako anatamani sisi twende tutafika Watanzania tukiwa na umoja na tukiamua kulipa kodi bila kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, nimesoma pia hotuba ya Kamati na Kamati ya Bajeti, na nimeona hapa ambapo wamesema kwamba sekta ambayo imekua kwa kusuasua katika mwaka wa fedha tunaomaliza ni sekta ya kilimo, ufugaji, misitu na uvuvi. Wamesema kwamba, sekta ambayo imesusua katika mwaka huu tunaomaliza ni sekta iliyobeba wananchi wa Tanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwa mawazo yangu kwamba sekta ya kilimo imesusua kutokana aidha sisi kutopata mvua ya kutosha katika kipindi hiki na ni kweli ni kutokana na tabia ya nchi, lakini kutokana pia na pembejo zinazotumika kwa walima. Pembejeo zinazotumika, wananchi bado wanatumia mbegu zilezile za kununua sokoni, bado wakulima wanaolima kwa jembe la kukokotwa kwa mifugo siyo wengi, wanaotumia jembe la mkono ni wengi. Kwa hiyo, hatuwezi kupiga hatua sana na ndiyo maana ikaonekana kwamba sekta hii inasuasua.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya kutotegemea sana kilimo kinachotegemea mvua atakayoleta Mungu. Nadhani sasa maeneo ambayo yakawezekana tukalima kwa kilimo cha umwagiliaji, tufanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, sisi tuliahidiwa kwamba tutajengewa bwawa kubwa sana pale Farikwa Wilayani Chemba, na mto ule wa Farikwa unasaidia sana wakulima wa Wilaya ya Bahi, wakulima wa Wilaya ya Kondoa na wakulima wa Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maji alituahidi, tukaambiwa upembuzi yakinifu unafanyika, lakini mpaka leo lile bwawa halijaanza kujenga. Tuliambiwa bwawa lile likijengwa litahudumia wilaya nne, Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Dodoma Mjini na Wilaya ya Bahi; na wakulima ambao maji



yangepita katika maeneo yao wangelima kilimo cha umwagiliaji; na tungesahau njaa Dodoma. Dodoma ardhi yetu siyo mbaya, hatupati mvua za kutosha, lakini tukipata mvua ndani ya miezi mitatu, tunavuna vizuri sana. Sasa kama tutaweza kupata mabwawa ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji nadhani tutafika mbali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bahi sasa hivi kuna kilimo kizuri sana cha mpunga; na akiana Said hawa kutoka Zanzibar wanahunua mpunga sana pale Bahi. Lakini mwaka huu hatuna kitu, hatuna kitu kwa sababu hatuna maji na bwawa la Farikwa halina maji na hata hivyo halijajengwa, kwa hiyo, wakulima hawana namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, sisi ni nchi ya tatu Afrika lakini Sekta ya Ufugaji, pia haijawanufaisha sana wafugaji na kila leo tunasema wafugaji wapunguze mifugo. Wanapunguzaje mifugo wakati hawana soko? Wana Soko la Nyama tunayokula sisi. Wangeweza kuuza nyama Arabuni, Dubai, tena mfugaji wa kawaida tu! Lakini hatuna viwanda vya kusindika nyama. Tuna viwanda vichache sana vya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Spika, kama Dodoma hatuna kabisa kiwanda cha kusindika maziwa. Kila siku wakulima wanagombana na wafugaji hapa Kiteto. Wana mifugo mingi lakini hawana namna ya kupunguza mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa na Kiwanda cha Maziwa, Kiwanda cha Nyama na Kiwanda cha Ngozi, wafugaji wangeona faida ya kufuga na mifugo ingeweza kupunguzwa kwa kuuza nyama na maziwa kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Viwanda na Serikali yangu, waone namna ya kuanzisha viwanda kwa ajili ya wafugaji na hata kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, pia wamesema misitu na uvuvi; na Pwani yote ni wavuvi. Sidhani kama Watanzania ni maskini, nadhani umaskini tunajitakia. Tungekuwa na namna ya kupata viwanda tukasindika samaki, tungefika mbali. Tungeza samaki katika masoko ya dunia. Naiomba sana Serikali inayokuja kwamba hili pia litizamwe. Mazao ya misitu kama hatuwezi kama Serikali, tunaweza tukaungana na sekta binafsi na tukafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wa Dodoma wanapenda sana ujasiriamali, lakini wanashindwa kuwa wajasiriamali kutokana na kwanza dhamana katika benki zetu, lakini riba pia, wanawake wanaogopa kunyang'anywa magodoro, vitanda, viti, TV kwa sababu atakaposhindwa

kurudisha mkopo watakuja kuchukua vitu vyake na hata nyumba inaweza ikapigwa mnada. Riba ni kubwa mno! Riba katika mabanki yetu ni kubwa mno. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haiwezi kutusaidia, basi ardhi ya Tanzania ipimwe, watu wamilikishwe ardhi, wananchi katika vijiji vyetu wamilikishwe ardhi ili anayetaka kwenda kukopa basi ardhi iwe dhamana yake. Wako vijana waliomaliza Vyuo Vikuu wameamua kulima, lakini wanunua pembejeo? Hawawezi kununua kwa sababu hawana dhamana benki. Wanatamani kununua trekta, hawana namna ya kununua matrekta kwa sababu hawana dhamana. Hebu tunaposema tuwasaidie vijana waliomaliza Vyuo Vikuu, mimi ninao, wapo na ambao wameanza kulima, lakini hawana namna ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuna kampuni fulani ya vijana inaitwa Rabican, wameshanifuata mara nyingi sana wakitaka niwasaidie kupata pembejeo ya trekta, nimeshindwa kuwasaidia, kwa sababu nimewapeleka Benki na Benki wanataka dhamana. Naomba hawa ambao wanaonyesha nia ya kufanya maendeleo, basi wasaidiwe. Kama ni ardhi ipimwe basi ili mwananchi anayetaka kukopa, basi aweke dhamana yake ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwangu hapa katika Wilaya ya Dodoma Mjini tuna shida ya kuwalipa Wazabuni. Mzabuni aliyetuwekea maji amefanya mambo mengi, bado kutandaza mabomba tu ili wananchi wa Ntyuka waanze kupata maji. Sasa hivi alikuwa anatupeleka Mahakamani. Tumeshabembeleza, hatuna lugha nyingine ya kumwambia. Anadai fedha zake, hajalipwa! Naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi Wazabuni walipwe madeni yao na hasa ambao wameshafanya kazi, wamepeleka wamepata *certificate*, walipwe madeni yao. Wananchi wa Ntyuka hapa, tena ni mjini kabisa, wanateseka, kisima kimeshachimbwa, wameshaweke mashine ya maji, lakini kutandaza mabomba imeshindikana kwa sababu Mzabuni anadai. Naomba sana Serikali iwalipe Wazabuni.

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza barabara za lami nyingi! Tumejenga barabara nyingi sana za lami, lakini kama barabara hizi hatutapata namna ya kusaidiwa, barabara hizi zitaharibika kwa muda mfupi sana. Naiomba Serikali sasa ione namna ya kutengeneza reli ya kati. Jamani reli ya kati hii inawasaidia sana watu maskini, lakini pia itasaidia sana kufanya barabara zetu zidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, reli ya kati sasa itengenezwe. Waliopita zamani waliwezaje kutengeneza reli ya kati ikafanya kazi, leo sisi tunashindwa kutengeneza reli ya kati? Hebu reli ya kati itengenezwe ili

kupunguza magari ambayo yangepita kwa mizigo kwenda Mwanza, Kigoma na maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali yangu naipenda sana, lakini suala la kuendelea kujenga Ofisi za Serikali Dar es Salaam halinipi amani. Wananchi wa Dodoma hawana amani kwa Serikali kuendelea kujenga nyumba za Serikali Dar es Salaam. Hivi mliposema Dodoma ni Makao Makuu, ni Makao Makuu ya Bunge tu, siyo Makao Makuu ya Ofisi za Mawaziri? Kuna tatizo gani? Shule zipo, tumeshajenga; Shule za Sekondari, za Msingi, Vyuho Vikuu vipo; ni bahari tu! Tutachimba basi bwawa kubwa mwone kama bahari, kama bahari ndiyo inafanya Serikali isihamie Dodoma. Nawaomba tupunguze msongamano wa Dar es Salaam kwa kujenga nyumba za Serikali Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Wastaafu Dodoma, wamenifuata nyumbani jana, hawajalipwa pesa zao. Wale watu miaka yao yote wameitumikia Serikali ya nchi hii kulipa pensheni yao imekuwa taabu. Tuwahurumie jamani! Hawana nguvu za kufanya kazi, hawana nguvu ya kufanya biashara yoyote! Naomba wale watu walipwe pensheni zao. Walitaka kuandamana, nikawaambia hapana, ninyi viongozi rudini. Mimi nitalisema Bungeni na nitamwona Ndugu yangu Mheshimiwa Saada Mkuya aniambie tatizo ni nini kwa kuwalipa wastaafu? Nadhani wanasikiliza!

Mheshimiwa Spika, tangu asubuhi habari za wastaafu ambao hawajalipwa pensheni limezungumzwa sana humu ndani. Naiomba Serikali sasa wastaafu walipwe. Bora sisi tusilipwe, lakini wale hawana nguvu ya kufanya kazi yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wilaya ya Dodoma Mjini tuliingia kwenye mpango wa uboreshaji wa miji na tukapata pesa za wafadhili na pesa hizo tumejengea baadhi ya barabara za mji huu na mnazona, tuna barabara nzuri sana katika mji wetu. Kuna mambo ambayo yalikuwa yamebaki, kuna barabara ambazo zilikuwa zimebaki na kuna mambo ambavyo yalikuwa yamebaki, tukaomba fedha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kabla ya bajeti hii wafadhili watakuwa wametoa hizo fedha. Tuliambiwa kwenye Baraza la Madiwani kwamba fedha hizo zingetoka kabla ya mwezi wa nne, lakini mpaka leo ninavyozungumza, hizo fedha hazijatoka.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri, hebu fuatilia hizo fedha kwa wafadhili ili tumalizie kazi iliyobaki kwa sababu leo tutaifanya kwa gharama ndogo, lakini kadri inavyochelewa ndivyo tutakavyoifanya kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna watu wangu ambao wamejenga kandokando ya *Airport* ya Dodoma. Tangu mwaka 2007 waliambiwa wasiendeleze jengo lolote pale kando kando ya *airport* kwa sababu wanajenga barabara ya lami pale na tathimini ikafanywa. Hawajalipwa mpaka leo. Walipwe!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Said Zubeir atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Kalogeris na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, name namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kutupa afya njema jioni hii. Pili, nakushukuru wewe pia kwa kunipa hii nafasi. Pia nakupongeza kwa ujasiri wako kama walivyokupongeza wengine. Ukweli umekuwa ni kioo kwa wanawake wote kwamba mkiwezeshwa mnaweza. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tunaweza bila kuwezeshwa! Hatuwezeshwi! *(Makofi)*

**MHE. SAID M. ZUBERI:** Pili, nawashukuru wananchi Jimbo langu la Fuoni Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote hiki kugumu cha umri wa Bunge hili na niwaambie tu kwamba, hakuna hata mmoja aliyenikosea. Nawaomba wanisamehe pale nilipowakosea, ila wanachotakiwa watambue ni kwamba, mzazi kwenye nyumba anayempenda mwanawe wakati mtoto anaumwa, akimchukua kumpekela hospitali, akiambiwa na *Doctor* kwamba huyu mtoto anahitaji sindano, kwa hiyo, kinachofanyika kwa Mzee kinaonekana ni ukatili kwa mtoto. Lakini kiukweli inakuwa ndiyo utaratibu wenyewe na ndiyo mapenzi yenyewe.

Kwa hiyo, pale nilipowakwaza, lengo langu lilikuwa ni kutengeneza, haikuwa kuharibu. Nawapenda sana, wanisamehe sana, hawakunikosea. Wanitegemee tena kurudi na kupata ridhaa yao muda ukifika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Nangu kwa hotuba yake nzuri; nampongeza Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake na watendaji wote kwa bajeti nzuri iliyokidhi. Nasema imekidhi kwa sababu tuko kwenye wakati tofauti kabisa, tuna tofauti ya miaka minne iliyopita na mwaka huu wa tano ambapo kuna mambo makubwa kama uchaguzi pamoja na kazi zinazoendelea za kuandikishwa watu.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha nyingi hapa zimepotea! Maana mtu anaweza akauliza unawapongeza kwa kipi? Mbona inaonekana maendeleo ni madogo, lakini haya ni mambo ya msingi tuliyokuwa nayo sasa hivi? Walikuwa hawana jinsi kama Wizara, isipokuwa kuyakabili kwa kadri itakavyokuwa. Kwa hiyo, nawapongeza wamefanya kazi nzuri na *Inshallah* huko tutakapokwenda mambo yatazidi kuwa mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi ni lazima kila Mtanzania awe na *ID*, awe na kitambulisho. Kwa hivo, jambo hili tulilifanya; Serikali tulilipigia kelele humu waliendeleze, unajua kipindi hiki kidogo linasuasua kwa mambo hayo tuliyoeleza, lakini ni matumaini yangu kwamba tukiacha bajeti hii, tutakopokuja kwenye bajeti ijayo ya mwaka 2016/2017, ni kwamba hili litapewa kipaumbele kwa ajili ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi bila ya kuwatambua Watanzania wote kwa kazi zao, mahali pao wanapokaa na nini wanafanya, hatutaweza kukuza uchumi. Lakini kama tutawatambua vizuri tukajua wanachokifanya, basi tutaweza kukuza uchumi kupitia kodi stahiki kwa kila Mtanzania halisi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima ambalo tunalidharau, naona lina *impact* kubwa kwenye kusaidia kuiondoa Serikali hapa au nchi hapa ilipo ili kusogeza hatua, suala la kuwapa zawadi walipa kodi wadogo. Serikali huwa inajikita sana kutoa zawadi kwa walipa kodi wakubwa, lakini wanachosahau ni kwamba mlipa kodi na mlipa kodi mdogo wote ni sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivyo kwa sababu ya mitaji yao. Kwa hiyo, mwenye kumiliki Shilingi milioni tano akaifanyia biashara, akalipa kodi yake sawa sawa kwa udogo wake, basi naye vilevile alikuwa anastahili *at least* kupongezwa na ikiwezekana kuzawadiwa kama wanavyozawadiwa wale wenye biashara kubwa pale wanapofanya vizuri. Tukifanya hivi itakuwa ni *proud* kwa hawa wajasiriamali wadogo na itakuwa ni motisha kwao kuweza kulipa kodi sahihi na kwa wakati muafaka na nchi ikaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe tu kwamba, zile kodi ndogo ndogo, yaani Shilingi moja moja kwa ujumla wake ukizikusanya, kwanza inakuwa ni rahisi watu kutoa, halafu inakuwa ni fedha nyingi kuliko *bulk* ya mtaji mkubwa ya watu unaoweza ukawahesabu. Kwa hiyo, hata ulipaji kodi wao wakati mwingine unakuwa hauna nguvu.

Mheshimiwa Spika, kama tutafanya juhudi za makusudi Serikali kuweka *incentives* hizi kwa wale wajasiriamali wadogo wadogo wakatambulika, wakafahamika na wapakewa zawadi pale inapobidi, basi hili lingeweza kuinua ari kwa hawa wajasiriamali wadogo wadogo wenye mitaji ya Shilingi milioni moja, mbili, tatu na kuweza kulisaidia Taifa lao kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna suala zima la viwanda pamoja na kilimo. Siku zote ninaposimama hapa huwa napenda sana kuishauri Serikali kwamba isidharau viwanda vidogo vidogo na ikathamini viwanda vikubwa. Nchi zote zilizoendelea, kama mtafuata *history*, ziliendelea kwa kuwasaidia wajasiriamali pamoja na viwanda hivi vya kati ndipo wakaendelea kwenda na viwanda vikubwa. Tuna mfano wa kutosha, kama sasa hivi tukichukulia kwenye *Sunflowers*, ukitoka Dodoma kwenda Dar es Salaam unakuta njiani mafuta mengi. Wale ni wajasiriamali wadogo, watu wenye viwanda vidogo vidogo na wanao uwezo wa kusaidia uchumi huu uka-*generate* vizuri na tukaondoka hapa tulipo kuliko kutegemea viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba tuachane na viwanda vikubwa, ila kuwe na *category* nzuri ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia watu wa kati ambao ndio wengi katika jamii yetu au katika nchi yetu twendenao sambamba kuwapeleka huko juu, kuliko kutegemea kwamba tuwe na viwanda vichache, matokeo yake wafanye *monopolies* ambazo ndizo zinazokuja kutuangusha na kuyumbisha Serikali kwa ujumla wake. Lakini kama tutawasaidia hawa wadogo wadogo, nahisi kwamba tunaweza tukafikia mahali pazuri, tukatengeneza viwanda vingi vidogo vidogo na vikaweza kutusaidia pamoja na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, hapa kidogo kwenye suala la ukulima niondoke kidogo niwatahadharishe Watanzania hususan Wanzazibar, nimekumbuka kitu baada ya kusema wakulima wadogo wadogo. Kule kwetu Zanzibar tuna eneo dogo la kulima na hivi majuzi kuna mgombea mmoja ameshachukua Fomu ya Urais, Maalim Seif Sharif Hamad, amewadanganya Watanzania pamoja na Wazanzibari; tena alisema kwa kejeli! Mimi nasema kwa kejeli, maana yake alisema; “najua Wanzazibar mnapenda sana kula wali! Kwa hiyo, nitakachokifanya, nikiingia tu madarakani, mchele utakuwa hauna kodi, yaani utakuwa ni bure!” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kweli huyu anawadanganya watu. Katika ulimwengu huu, sayari hii tunayoishi, hakuna nchi hata moja ambayo haiendeshwi na kodi za nchi. Hakuna! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaambia Watanzania hususan Wanzazibar kwamba huyu amewadanganya mchana saa nane, jua linawaka. Wanachotakiwa ni kwamba, wakae wafikiri vizuri. Mimi nilitegema angesema labda, kwa kuwa Wanzazibar mnapenda wali, basi nitakachokifanya, nikiingia tu Ikulu, Ikulu yangu nitaihamishia Banda la Maji kile Kibokwa, Upenja, Mtwango na Cheju kunako mabonde yetu ya mpunga ili nikahakikishe tinalima mpunga mwingi tuiwezeshe hii nchi kutoa mpunga wa

kutosha na kuwalisha Wanzanzibar. Siyo kuwaambia kwamba mchele utakuwa bure. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapa anafungua mianya ya kuanza tena magendo ambayo sasa hivi hayapo kwa sababu mchele ule utaingia mwingi mwisho utakuja huku Bara. Itakuwa kazi kule kila siku hali ndiyo hiyo, lakini hakuna chochote.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza zaidi, Mwenyekiti wake Profesa, lakini Profesa naona na jina lake, Lipambavu ni Profesa kweli! Kwa sababu nilitegemea mchumi yule angemweka sawa akamwambia kwamba huko unakokwenda siko. Lakini hapa ndiyo inathibitika kwamba kule kuna watu ambao wanajiona wao ni wa Sultan, wanachosema wao ndiyo hicho hicho!

Mheshimiwa Spika, ninachowaambia Wanzanzibari, wayatafakari sana haya maneno, halafu watazame uhalisia; ukweli na uongo. Haya ni maneno yako wazi na yanadhihirisha kwamba huyu jamaa ameshachoka kufikiri na hafai hata kuwa kiongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine, kuhusiana na ripoti ya *BoT* tuliyoisoma hivi karibuni, ilituelekeza kwenye hili suala hili zima la uchumi, kwamba tunahitaji lazima tu-*export* sana na tupunguze kununua, yaani ku-*import*. Hii itasaidia hata Shilingi yetu kuwa *stable* na kuendeleza uchumi wetu. Sasa naiomba Serikali wawe wa kwanza kuhakikisha mambo ambayo hayahitajiki, hayana ulazima wa kununuliwa, basi wayapunguze ili kuisadia fedha yetu au kuusadia uchumi wetu kukua kwa haraka na wawasaidie wajasirimali wenye uwezo wa kutengeneza vitu humu humu ndani ili tuanze kuzungusha ile fedha ndani, kuliko kuitoa.

Mheshimiwa Spika, tulipata somo hivi karibuni na ninahisi kwamba ni jambo la msingi, Serikali inapaswa na ni lazima izingatie haya kupunguza manunuzi na kuongeza kuwekeza ndani ikiwemo kilimo, viwanda hususan hivyo viwanda vidogo vidogo na tuweze ku-*export* nje kwa ajili ya kulisaidia Taifa hili na kuisaidia fedha yetu iweze kuwa *stable* kwa kipindi kijacho tunachokwenda.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusu *commodityexchange*, naiomba Serikali ijitahidi sana kuwa na soko au mnada wa Kimataifa. Huu utatusaidia kipindi ambacho watu wanalima sana kwa sababu sasa hivi tunazungumzia njaa, watu walivunjika moyo kufuatana na kilimo kilicholimwa miaka miwili iliyopita na mazao kukosekana wapi pa kupeleka. Lakini kama tutakuwa tuna hii *commodity exchange*, inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Spika, hii itakwenda sambamba na wanazoziiita stakabadhi ghalani, yaani kuwa na maghala ya kuweza kuhifadhia. Kama tukichanganya mambo haya vizuri, basi yanaweza yakatufikisha pahali pazuri zaidi, kwa sababu wakulima watajua kwamba mtu akiingia tu kwenye mtandao, aliyekuwa hajui kwenye mtandao kama kutakuwa kuna utaratibu wa kuwafahamisha, soko likoje, ikiwa la mahindi, mpunga au kitu chochote huko nje; na watu wakaweza kununua, basi ni matumaini yangu kwamba tunaweza tukafikia hatua nzuri sana kuliko hapa tulipo.

La mwisho kabisa, naupongeza uongozi na Serikali kwa miaka yote hii mitano, imefanya kazi nzuri. Maneno hayo ni ya kawaida. Hakuna Mtume hata mmoja aliyekuja, akapendwa na watu wote, ila maendeleo kwa mwenye macho ameyaona. Tofauti tulikotoka na tulipo, ni vitu viwili tofauti. Ni matumaini yangu kwamba Watanzania bado wataendelea kuichagua Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Murtaza Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Kalogeris, halafu atafuatia Mheshimiwa Riziki Lulida-na Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:-** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, nakushukuru sana kwa nafasi hii niweze kuchangia kwenye hotuba ya bajeti iliyokuwepo mbele yetu leo na kwa kipindi tulichokuwanacho, leo ndiyo hotuba ya mwisho. Kwa hiyo, nianze kwanza kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, ambao wamenipa dhamana kubwa sana na kuniamini kuweza kuwawakilisha kwa kipindi hiki na wakati utakapofika, yanayofuata tutayajua hapo itakapofika.

Mheshimiwa Spika, pia nitakuwa ni mwizi wa fadhila nisipokushukuru wewe. Nakushukuru sana kwa mwongozo ulionipa na ushirikiano ambao umeonyesha kwa kipindi chote ambacho tumekuwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya matatizo na mambo ambayo yamenipa shida sana kuyafikiri na kuyaona ndani ya Bunge hili, mara nyingi huwa tunafikiri moja kati ya vitu ambavyo vinaweza vikajenga, ni Bunge hili kujadili masuala katika hali halisi iliyokuwepo. Lakini nilichokuja kugundua, ndani ya Bunge hili kuna wengine wanaingia wakiwa hawana njaa ya chakula, lakini njaa inayowasumbua ni njaa ya kufikiri. *(Makofi)*

Kwenye vitabu ambavyo niliwahi kuvisoma, kuna mwandishi na mtunzi mmoja, Shaaban Robert, yeye aliwahi kutunga kitabu na shairi akasema; “mficha kweli, ni mwizi; rada yake ni hukumu, kufungwa katika zizi; zizi la



wanyama wa wazimu, humo awe mfagizi hadi apate fahamu; hamna kitu ushenzi, kama ukweli kudhulumu." (Makofi)

Wenzetu hawa, kila siku wanakuja kudanganya na kutoa hadaa za aina mbalimbali na sasa wamekuwa na usemi, "Oktoba acha ifike." Oktoba itafika na wala haina haja ya kuimwagilia maji, itafika tu na majibu yenu mtayapata. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, yapo mengi, lakini nataka nizungumzie machache. Jana wachangiaji walikuwa wanaikosa Serikali hapa, imeleta vitabu havieleweki. Hivi hii *addendum* mliyoileta, hamjui kama Waziri wenu kiza, maana yake mimi siwezi kusema kivuli; kiza, ameleta *addendum* kufanya marekebisho ya hotuba aliyoleta! Hili nalo hamlioni! Aaah, Mungu atawaongoza katika njia iliyo sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawashauri warudi hata kwenye *dictionary* tu, hebu mwelewe nini tafsiri ya bajeti? Bajeti ni *projection* tu kwamba tutapata hiki na kile tutakachokipata, tutakitumia hivi. Mnawatia hofu wananchi hapa kwamba hili halikufanyika na hili halikufanyika! Katika nchi tano zenye uchumi imara duniani; Japan, Marekani, Uingereza, Uchina na Urusi; nchi ya kwanza inayoongoza duniani kwa kudaiwa ni Japan na ndiyo nchi tajiri na wakati mwingine tunapokea misaada kutoka kwao. Mbona wao hatuwasikii wakilaumiana deni la Taifa linakua?

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa linakua kwa sababu tunataka tujenge miundombinu, ambayo wananchi wanaiona na ndiyo wanawashangaa ninyi, kila siku mnasema hakuna kitu kilichofanyika; kila siku! Lakini barabara zinazojengwa, mnatumia! Tunataka kufanya upanuzi wa reli, mnatumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, humu ndani tunazungumzia suala la kukuza uchumi, nami nashangaa wengine wanasema, "mimi mchumi," ninyi sijui ni wachumi wa namna gani! Maana yake wachumi wako wengi. Wengine nadhani ni wachumi wa Sayansikimu, ile *homeeconomy*, labda! Kwa sababu tunawezaje kukuza hii nchi, katika fedha ambazo zimetengwa katika bajeti hii? Ni kukuza miradi ya umeme, kujenga barabara na kupanua bandari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tunawezaje kujenga uchumi bila kuweka miundombinu ya kukuza uchumi? Tuna tatizo la ajira la vijana, tuna tatizo la ukuaji wa uchumi ambao hauna uwioano kwamba wananchi wenye kipato kikubwa na wananchi wenye kipato cha chini *gap* ni kubwa. Tunaiondoaje? Ni lazima tufanye mapinduzi kwenye viwanda; na viwanda tunavyovizungumzia ni viwanda vidogo vidogo. Tunawezaje kuanzisha viwanda vidogo vidogo bila kuwekeza umeme katika maeneo ya vijijini? Njoooni tuwafundishe uchumi sisi

tunaofahamu uchumi. Maana yake sijui wenzetu ninyi mnafikiri namna gani!  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingi sana katika nchi hii ambayo hakuna haja ya kumulika tochi ili watu waweze kuiona. Miradi ni mingi! Naishukuru sana Serikali, katika kipindi ambacho nimeongoza kwa miaka cha miaka minne na nusu, tumeweza kupata miradi mikubwa ya umeme ambayo ina zaidi ya Shilingi bilioni tisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile tumepata miradi mingi ya maji, miradi mingi ya barabara kuweza kuboresha. Kwa sababu uchumi bila ya kuzalisha; baada ya kuzalisha, kufanya hicho kilichozalishwa, yaani *production, then processing*; tunazi-*process* zile bidhaa tulizozipata, *then* tunakwenda kwenye *distribution*. Tunalalamikia hapa sukari ina shida, lakini sukari hiyo utaipata vipi bila kuibadilisha kutoka kwenye mua ili ije kuwa sukari na kufika kwenye soko? Sijui kama huwa mnafikira hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye ukuaji wa uchumi, ziko tafsiri nyingi sana ambazo tunaweza tukazitumia. Inategema ni matokeo ya namna gani ambayo unataka kuyapata baada ya kufanya tathmini hiyo. Sasa sisi tunapozungumzia ukuaji wa uchumi, tunaka kuona jinsi gani ambavyo maisha ya mwananchi yanakuwa mepesi, ndiyo maana tunawekeza kwenye ujenzi wa zahati ili watu waweze kupata huduma ya afya; tunawekeza kwenye maji ili wananchi waweze kupata maji na kulinda afya zao; tunawekeza kwenye barabara ili kinachozalishwa kiweze kufika kwenye soko na wananchi vilevile waweze kuhimili zile bidhaa zinavyofika kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, leo hii hapa tumezungumza kwamba tunaagiza kwa kiasi kikubwa sana, lakini huwezi kuzuia kuagiza. Nami napingana na watu ambao wanasema sasa hivi Serikali mzuie kuagiza saruji na sukari. Saruji imeweza kusimama katika bei iliyokuwepo kwa sababu kuna saruji inayotoka nje, ndiyo maana bei imeweza kukaa hapo, vinginevyo, tukiachia viwanda vya ndani peke yake, wakitengeneza *cartel*, saruji inaweza ikafika mfuko zaidi ya Sh. 20,000/=. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima tuambizane ukweli, hivi ndivyo ambavyo uchumi unajengwa. Hatuwezi kujenga uchumi kwa kujifungia ndani kwamba vyetu ni vyetu, hatutaki kitu kingine kutoka nje. Aaah, ninyi mmesoma wapi?  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunataka kufanya mapinduzi ya uchumi, naishauri sana Serikeli, ili tuweze kukuza uchumi kwa haraka, eneo kubwa ambalo ni lazima tuliangie ni kwenye uchumi wa kukuza kilimo. Bila kuwa na *mechanized agriculture*, tukategemea mtu anatoka na jembe lake asubuhi,

kwenda kulima; mimi nasema hiyo siyo kulima ni kukuna ardhi. Lazima tujenge mazingira mazuri, tuwakopeshe wananchi, tuwape pembejeo za kutosha, waweze kulima na kile tunachokizalisha kiwe na tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuangalie katika mipango hii tuliyonayo, maana yake hii siyo bajeti peke yake, Waziri wa Mipango yuko hapa; unasikia tunayoyasema kwamba tunataka tuwe na mipango ya kufanya *transformation* ya kilimo. Lazima tubadilishe kilimo hiki. Kilimo tunachokifanya sasa, kinawaumiza sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunataka kufanya mapinduzi ya viwanda. Viwanda tulivyonavyo, hasa vya nyama, ni vichache. Tunahitaji tuwe na viwanda vya nguo. Pamba; maana yake Wasukuma ni watu ambao kwa sasa hivi wamejaliwa adhabu tu! Wana nyama nyingi, haina soko, wana pamba nyingi, nyuzi haziwezi kuzalishwa. Tunaweza tukazalisha nyuzi hapa na tukasafirisha kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika maeneo yetu tunaweza kuzalisha sana korosho, tunazalisha sana ufuta kwa sasa; viwanda vidogo vidogo vya kuweza kuboresha na kukamua mafuta; tubadilishe uchumi wa wananchi kwa kuwawezesha. Kwa nini tuagize mafuta kutoka nje kwa wingi hali ya kuwa tunaweza tukazalisha mbegu za mafuta ndani ya nchi yetu? Hayo ndiyo mambo ambayo tunatakiwa tuyazungumzie humu ndani; siyo tunakuja tu hapa kubunibuni mambo, ilimradi wewe umeambiwa ukienda useme hivi, basi unasema bila kujua hilo jambo lina athari kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukuaji wa uchumi, kama nilivyosema, ziko athari nyingi sana. Lakini jambo ambalo Serikali lazima tuliangalie kwa umakini sana, ukitaka kuangalia *effect* ya jambo mlilolifanya kichumi, mnaangalia matokeo ya mwisho au matokeo ya katikati.

Mheshimiwa Spika, sasa uchumi wetu leo hii umeruhusu sana ujenzi wa *real estates*, umeruhusu sana ujenzi wa makampuni ya mawasiliano, lakini vilevile, umeruhusu sana taasisi za fedha. Sasa inapotokea jambo kama hili, Mwaziri ninyi wote bahati nzuri ni wachumi ambao nawaamini, mnaelewa nini kinachotokea. Ni kwamba hii inaweza ikawa ndiyo sehemu ya utupaji wa fedha zile zinazokuja kutakatishwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili tumekuwa tunatoa miradi mingi sana kwa Makampuni ya kigeni. Sasa tuangalie ni namna gani ambavyo tutaweza kudhibiti, miradi tunayoiendesha ya kukuza uchumi ihusu Makampuni ya ndani ili tusiwe tuna-*export forex* zetu. Makampuni mengi ya ndani yamefanya kazi nzuri sana. Kwa mfano, ukichukulia makampuni kama ya Azam, *Mohammed Enterprises*, wamefanya kazi kubwa sana kuweza kujenga viwanda ndani ya

nchi, na hii tunalinda uchumi wetu. Sasa tuangalie, ili waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo Makampuni kama *IPP*; wamefanya jitihada kubwa sana kuweza kuajiri wazawa. *Clouds FM* wamefanya kazi kubwa sana kwa kipindi cha miaka zaidi ya mitatu kuhakikisha tunahamasisha wananchi wetu waweze kutumia bidhaa za ndani. Haya ndiyo mambo ambayo Serikali mnatakiwa muunge mkono katika kukuza uchumi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, jana kuna wachangiaji wengine walikuwa wanachangia wanasema, aah, bwana hawa wameandaa bajeti kubwa kwa ajili ya kulipana posho na mishahara. Hivi hao Walimu tunaowaajiri, Wanajeshi ambao tumewaajiri, Wahudumu wa Afya, tuwaajiri bila kuwalipa mishahara? Ndiyo fedha hizi ambazo tunatenga kwa ajili ya kuweka huko.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie, kwenye kuwekeza, unaweza ukawekeza na unaweza ukawekeza vizuri, kwenye *human capital!* Lazima tusomeshe watu, lazima tuweke huduma ya afya kwa watu wetu! Sasa ninyi wenzetu mnajifunza wapi uchumi mnaouzungumzia humu ndani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine yote, naomba niendeleo kuiunga mkono Serikali kwenye miradi yote ya uboreshaji wa uchumi, nami katika eneo la Jimbo langu, tuna miradi ya maji ambayo imeshafikia hatua nzuri. Naunga mkono bajeti hii ili wananchi wa Kipatimu, Chumo, Mingumbi, Tingi, Miteja, waweze kupata maji. Mradi wa maji umeshaanza, fedha zinahitajika na zimepangwa kwenye bajeti hii ili ziweze kukamilsiha mradi ule.

Mheshimiwa Spika, siwezi kukataa bajeti hii! Hawa wanakataa na kukataa kwao kwa kudanganya, kwa sababu baada ya kumaliza hapo, wanakuja kwenu kuwaambia mradi wangu haujafika. Mimi siwaamini, kwa sababu kwa kweli kwa hawa watu, hata akiniambia kumekuchwa, niko ndani, sikubali mpaka nitoke nje nione jua limetoka kweli! Kwa sababu huwezi kujua ni lipi ambalo analisema lina ukweli na lipi ambalo wanalisema halina ukweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanalalamikia hata kwa nini CCM imekuwa na watu wengi wanaokwenda kuchukua fomu ya kugombea Urais. Kile ni Chama cha Kidemokrasia! Mtu yeyote anaweza akaomba fomu. Kama unataka kuthibitisha, Chama chako ulichoko wewe hakuna demokrasia, kachukue fomu kesho kama hukufukuzwa! Wangapi wamefukuzwa? Tangaza kesho kwamba mimi ikifikia wakati, nitachukua fomu; kama hukufukuzwa! (*Makofi*)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kama Mheshimiwa Zitto!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU-**: Thubutu! Sasa msijitie wazimu kwenye mambo ambayo...  
(Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa kwa kumalizia dakika zangu, kuna Mgombea wa Urais mmoja upande wa Zanzibar, nimemsikia anasema, "nahamasisha watu wote waliokuwa huko Bara, wanarudi waje kupiga kura." Huku anasema, yeye akipata Urais ni lazima Muungano uvunjike. Tunachowaambia, hamasisha watu wako warudi kwanza kule nyumbani, wakafanye shughuli zao za biashara na mipango yao yote kule kwanza, halafu vunja Muungano. (Makofi)

Wewe wakati unakimbia mikono ya sheria kule, ulijificha wapi? Si ulijificha hapa Bara! Leo hii unasema Bara hapafai, kwa sababu Serikali inakuhudumia, inakupa huduma ya afya na kila kitu! Tuiseme mengi, lakini binadamu yeyote mwenye fikra timamu, lazima ukumbuke hisani! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA**: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kalogeris, Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae na baadaye Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS-**: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ambayoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kukupongeza kwa dhati Mama yangu kwa kazi kubwa ambayo umeifanya katika kuliendesha Bunge la kumi. Hakika wewe Mama ni Mama wa Chuma na mwenyezi Mungu akujalie uendelee kupata maisha mema na yenye nafaka na heri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne, anayemaliza muda wake hivi punde, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kufanikisha maendeleo yanayoendelea kupatikana katika nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii vilevile kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini kwa ushirikiano mkubwa ambao walinipatia katika kipindi changu chote cha miaka mitano ya Uongozi nikiwa kama Mbunge wao. Naamini kuna mambo mengi tumeyafanya kwa ushirikiano nao na ninaamini kwamba haya yametokana na jitihada za mimi na wao pamoja na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii vilevile kumpongeza Mama yangu Mheshimiwa Nagu, dada yangu Mheshimiwa Mkuya, Manaibu Mawaziri wa Fedha, lakini Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa katika kuiandaa Bajeti ambayo leo hii tunajadili yenye mwelekeo wa kujitegemea kama Watanzania. Bajeti hii hakika ni ya ukombozi kwa Mtanzania, hasa tunapoanza kwenda katika kujitegemea na kuondokana na wafadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ni kwamba bajeti hii tunasema ni makisio na matarajio, tunaomba katika mipango kazi itakayofanyika kwa mwaka huu angalau ifikie asilimia 80 ili angalau haya tunayojadili na kuyapitisha yawafikie Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, natumia nafasi hii vile vile kupongeza Wizara ya Fedha hasa katika suala la kuweka tozo kidogo, mimi sisemi nyingi, ni kidogo katika mafuta. Kweli itakuwa ni maumivu kwa wananchi, lakini naamini maendeleo yoyote hayawezi kuja bila kupata maumivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba upo uwezekano kwamba wapo watu wanaotaka kupotosha kuwaambia wananchi; na hili limetokea hata katika kipindi kilichokwisha tulikuwa tunahitaji mawasiliano ya simu kwa wananchi wetu vijijini, tulipitisha katika bajeti lakini walitokea wajanja wachache, waliamini kabisa kwamba hiyo itakuwa ni kete ya CCM katika uchaguzi tunaokwenda wakafanya vurugu na matokeo yake ikashindikana kupata zile fedha ambazo zingeweza kufanikisha mawasiliano kwa wote.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali katika hili; uzi ni ule ule, tukaze buti, tuhakikishe kwamba hili linapita ili tuweze kupata barabara nzuri, umeme vijijini na maendeleo yaweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu vile vile kwa Watendaji, hasa katika mamlaka za kudhibiti; Wataalam, mdogo wangu Mheshimiwa Shabiby, kaka yangu Mheshimiwa Mbunge wa Muheza wameeleza. Ukijaribu kupiga hesabu, ongezeko hili ni dogo ambalo haliwezi kuleta athari kubwa kwa wananchi.

Sasa naombe tu, mamlaka husika hasa *EWURA*, Mamlaka husika *SUMATRA*, pamoja na ongezeko hili, hebu wakakae chini wakaangalie ili isije ikatokea wafanyabiashara wachache wakatumia mwanya huu kuweza kujitajirisha na kupaka matope kwa Serikali. Mimi naamini fedha hizi zikienda kwenye barabara, maumivu tutakayoyaona sasa, faida yake ni kwamba tutakuwa na barabara nzuri ambazo zitatufanya mazao yatoke vijijini na yafike kwenye soko na hivyo kuweza kumnufaisha mkulima.

Mheshimiwa Spika, naamini vile vile barabara zikiwa nzuri, magari mengi yatafika vijijini na bei ya nauli kwa abiria itapungua. Mfano ninao tu kwenye Jimbo langu kabla barabara barabara hazikuwa nzuri, magari yalikuwa mawili ambayo yalikuwa yanafika Kisaki na kuja. Nauli ilikuwa Sh.15,000/= . Tumeboresha barabara, sasa hivi yako zaidi mabasi kumi, nauli imeshuka toka Sh. 15,000/= mpaka Sh. 8,000/= kutoka Kisaki kwenda Morogoro.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba katika bajeti mliyoipanga, hili ongezeko moja tu la tozo ya kodi kwenye mafuta, litasaidia kuleta maendeleo makubwa. Vile vile umeme ukifika vijijini tutafungua viwanda vidogo vidogo, akina mama saluni wataendesha, vijana watachomea mageti, wataengeneza milango, uchumi utakua na mafanikio yataonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nampongeza vile vile Mheshimiwa Waziri kwenye ongezeko la kodi kwenye sukari itokayo nje. Mimi natoka Morogoro, kama Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro, kuna malalamiko makubwa, ukienda Kilombero; lakini vile vile kama Halmashauri tuliweza kutembelea shamba la sukari la Kagera; Sukari inayotoka nje bila kufuata utaratibu mzuri tunaua viwanda vyetu vya ndani.

Katika ongezeko hilo, ni matumaini yangu sasa tutafanya viwanda vyetu vya ndani vijipanue na katika kujipanua kwake tutaweza kuchukua mazao ya wakulima wa miwa (*out growers*) na kuweza kuingia katika viwanda kwa sababu sukari itakuwa iko *limited* kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sukari imekuwa nyingi kutoka nje, kodi yake ndogo, ndani viwanda vinashindwa kuchukua miwa ya wakulima (*out growers*), inakumbatia miwa yake ya kiwandani, matokeo yake tunapunguza ajira kwa vijana wetu, lakini matokeo yake tunawafanya wakulima wetu wa miwa waache biashara ya mashamba ya miwa na kuingilia kwenye biashara nyingine. Lakini huko wanakokwenda naamini biashara ya miwa ukiangalia imewasaidia sana hawa *out growers*.

Vile vile itatusaidia na sisi, mfano kama kwangu kule Jimboni Morogoro Kusini, tuna mpango wa kukaribisha wawekezaji kwa ajili ya kulima mashamba ya miwa na kiwanda cha sukari itaweza kufanya huyo mwekezaji naye akawa na imani kwamba kweli Serikali inaandaa mazingira mazuri kwa uwekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, pia natumia nafasi hii kuleta ombi langu kwa Serikali. Pamoja na kuangalia kwenye viwanda vya sukari, hebu tuangalie katika viwanda vingine. Kuna Viwanda vya Nondo, Viwanda vya Mabati na Viwanda vya Cement, hebu tuangalie tunafanyaje? Angalieni katika mahesabu yenu kiutaalamu. Naamini kwamba mliangalia kwenye sukari mkaona tunapoteza.

Nawaomba kama wataalam angalieni katika Viwanda hivi vya Nondo, Mabati na Cement tuone tunaweza tukavisaidia vipi katika kuviweka sawa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie suala lingine kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwenye suala la madeni kama Hazina. Serikali ina kila sababu ya kuangalia uwezekano wa kulipa madeni ya ndani. Katika kulipa madeni ya ndani, ninaamini tutafanya wafanyabiashara wa ndani waweze kujipanua zaidi, lakini vile vile kuweza kulipa kodi kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mkandarasi, Serikali yangu inadaiwa fedha nyingi na Wakandarasi kiasi cha kufikia mahali pa kuwafanya Wakandarasi washindwe kulipa hata kodi katika kipindi tunachokwenda. Vile vile kuwafanya Wakandarasi washindwe kuaminika katika jamii wanayoishi, lakini vile vile kuwafanya Wakandarasi washindwe kutimiza majukumu yaliyoko mbele yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile hili liko sambamba na Wazabuni mbalimbali katika Serikali. Tumeshuhudia shule zikifungwa; naamini na Magereza huko tunakokwenda yatafungwa kwa sababu Wazabuni wanashindwa kulipwa fedha zao, wanashindwa kutoa huduma. Ukienda kwenye afya vile vile mahospitalini, kila mahali!

Naiomba tu Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi wakulima wa mahindi Mkoani kwangu Morogoro, kuna fedha kidogo haizidi Shilingi bilioni kumi lakini hakuna. Watu waliuza mazao yao wakiamini kwamba watakwenda mashambani wakalime, hawajalipwa fedha, wanashindwa kulima. Kwa hiyo, ni kielelezo tosha kwamba tunataka kuwatia umasikini Watanzania wenzetu wa ndani washindwe kufanya kazi yao, lakini vile vile kupata fedha za kujikimu katika maisha yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kunyanyuka, hebu atuambie Serikali ina mpango gani wa kuweza kulipa madeni ya Wazabuni wa ndani; wakulima na wakandarasi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme pamoja na kuzungumza hayo, kupita kwa bajeti hii ni maandalizi ya bajeti ijayo. Nilikuwa nina ombi kwa Serikali katika Halmashauri yangu ya Morogoro Vijijini kwenye upande wa maji hatujafanya vizuri katika kipindi chote cha miaka mitano, tumeweza kupata vijiji kumi tu kwenye ule mradi wa *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, nimeona kwamba ili kupata matokeo ya haraka kwa sasa, kuna Wilaya zimeingizwa. Naomba Wilaya yangu ya Morogoro vijijini nayo iingizwe katika mpango wa *BRN* ili tuweze kutatua tatizo la kero ya maji kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini na Wilaya ya Morogoro Vijijini.



Mheshimiwa Spika, kwenye suala la umeme Serikali imefanya vizuri sana, tumefanya mambo makubwa, vijiji vingi vimepata umeme katika Jimbo langu la Morogoro Kusini na Wilaya ya Morogoro Vijijini. Ombi langu ni kwamba katika hizi fedha ambazo zitakatwa katika tozo tunayoizungumzia sasa hivi, zikipatikana zipelekwe kwa Wakandarasi wamalize kazi umeme uwake Kisaki, umeme uwake Mngazi, Dutumi, Singisa, Kongwa, Mvuha ili wananchi waweze kufurahia matunda ya uhuru, lakini vile vile kupitia umeme huo waweze kujiongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kilimo, Mkoa wetu wa Morogoro umezungumzwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye anamaliza muda wake kuwa Ghala la Taifa la Chakula. Kwa kutaja kuwa Ghala la Taifa la chakula ni kutokana na Mkoa wetu wa Morogoro kuwa na mito 117 inayotiririka mwaka mzima. Kwa kweli ziko jitihada za Serikali ambazo zinafanywa katika kutumbukiza fedha katika kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wetu wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Morogoro Kusini tuna eneo kubwa la mradi wa Kongwa – Turo. Katika mto huo kuna mabanio mawili ambayo katika kila banio lina uwezo wa kuzalisha hekta 5,000 za umwagiliaji mpunga. Kila mara tumejaribu kuomba fedha, mara ya mwisho mwaka wa 2013 tulipata Shilingi milioni 250. Kunahitajika kama la Shilingi bilioni moja kuweza kufanikisha mradi huu. Naomba katika bajeti ijayo Serikali itusaidie kupata fedha hizo ili kusudi na sisi tuweze kusaidia katika kuzalisha chakula kwa wingi katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Kidunda. Naipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya katika kulipa fidia wananchi wa Kata ya Selembala katika kupisha ujenzi wa bwawa la Kidunda. Ombi langu, fidia imelipwa, lakini ndani ya kulipwa fidia ulionekana upungufu. Katika ule upungufu ulioonekana, naishakuru Serikali na hasa ndugu zangu wa DAWASA, walikuja wakafanya tathmini upya na tayari wameondoka na tathmini. Nimeona kuna fedha zimetengwa katika bajeti hii kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Lakini sijui na ningependa nijue kutoka Serikalini: Je, hii fidia ambayo imekuja katika kurejewa, wananchi wangu fedha hizi zipo ambazo wakilipwa ili wapishe ujenzi huo wa bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote nilikuwa nataka nijue kwa ndugu zangu wa DAWASA sisi kama Halmashauri, tuliwaambia wajenge huduma za kijamii, Shule, Zahanati na Polisi. Tuliwakabidhi kila kitu, mpaka sasa hivi hatuoni kinachoendelea. Ni nini kinachoendelea? Tungependa tujue. Wananchi hawa kwa sasa hivi tayari wameshakabidhiwa viwanja na Halmashauri pamoja na kwamba kuna tatizo, viwanja tulivyopewa ni mapori. Naamini DAWASA wanatakiwa kusafisha ili wananchi waweze kukabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka kuzungumzia Makao Makuu ya Wilaya Mvuha. Tumeendelea kila mwaka kuieleza Serikali kwamba tunataka kusogeza huduma za kijamii katikati Mvuha ili tuweze kuwatumikia wananchi wetu. Kila mwaka tunaambiwa tuombe fedha; na katika maombi maalum tumeendelea kuomba lakini hatujapewa. Naomba kupitia TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Waziri Mkuu mwaka ujao wa fedha, tupewe fedha tujenge Makao Makuu ya Wilaya yetu Mvuha tutoke Morogoro Mjini tupunguze gharama kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabla sijapigiwa kengele, namwomba Mama yangu Mheshimiwa Saada Mkuya, malipo kwa Walimu katika Halmashauri yetu. Tunadai Shilingi milioni 150 tu stahiki za Walimu katika madai yao mbalimbali. Ni fedha ndogo! Nashukuru siku nilipozungumza katika kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu, kulitokea mrejesho kule, walipigiwa simu viongozi wangu na hatimaye nadhani wamekamilisha yale ambayo nilikuwa nimeyataja. Ombi langu tu, mtupatie fedha hizo kwa ajili ya Walimu ambao wana madai mbalimbali katika Halmashauri yetu, wafike mahali na wao walipwe malipo yao wafurahie kazi kama vile inavyopasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narejea kusema tena, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu ili kusudi haya ambayo nimeyazungumza na kuyaomba yaweze kutekelezeka. Nakushukuru sana mama. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Msabaha!

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA-:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii nipate kuchangia bajeti ya Serikali ambayo iko mbele yetu. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, pumzi na kauli.

Mheshimiwa Spika, vile vile hii itakuwa ni Bajeti ya mwisho mimi kuongea katika Bunge hili. Nakishukuru sana Chama changu, Viongozi wote wa Kitaifa kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Viti Maalum kuja kuwakilisha Zanzibar. Najua nimetenda haki na Mungu akipenda tutaonana tena kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwivi wa fadhila bila kukushukuru wewe kwa yale yote mema uliyonitendea katika Bunge lako hili Tukufu, ukinipa malezi kama Mama, nikayapokea, nikashukuru na nikayafanyia kazi. Hata ukiwa Mkoani Njombe nami nikiwa Mkoani Zanzibar, tuliweza pia kuwasiliana pale tulipokuwa na matatizo ya kifamilia na ya kijamii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakutakia kila la kheri, nimesikia hutaki tena kugombea Njombe, lakini kama utakuwa nyumbani, najua wewe ni mtu wa ibada, ni mtu wa kukaa karibu na Mungu, kwa sababu tunapishana; wewe ukienda kwenye ibada mimi nakwenda kwenye mazoezi. Mungu akubariki sana na akupe wepesi wa kila jambo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi wote; Mawaziri wote kutokea Zanzibar na Chama cha Wananchi CUF ambacho kinaongozwa na UKAWA hasa Mheshimiwa Samia Suluhu. Mimi wakati sijaingia humu Bungeni; huwa nawaambia wanawake wenzangu tujifunze kwa wanawake ambao ni viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Suluhu tulipata sana kukaa ofisini yeye akiwa ni Waziri wa kule Zanzibar nami nikiwa Kitengo cha Afya kwenye NGO; Mheshimiwa Saada pia nimewahi kufanya naye kazi kwenye Wizara ya Fedha kule; kwa hiyo, nilijifunza bila kugombana na bila kuwa na itikadi za Vyama tukajenga nyumba moja, nami leo mkakuta ni Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nilipoingia humu Bungeni, Kamati yangu ya kwanza ilikuwa ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mheshimiwa Mhagama. Pia tulikaa kule bila ukada wake wa Chama, alitufahamisha mambo mengi kule kwenye Kamati na nikakaa miaka miwili na nusu nikaondoka nikaenda kwenye Kamati ya Miundombinu na nikawa hodari katika Bunge hili hata *Hansard* za Bunge zinaonesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesoma kupitia kwa viongozi na akina mama wenzangu wa CHADEMA ambao ni Walimu akiwepo Mheshimiwa Mama Kiihula, ni mlezi wangu ndani ya Chama akiwa kama Katibu wangu Mkuu, nami nikiwa kama Makamu wake kwa Zanzibar kwa Baraza la Wanawake, wakiwemo akina Mheshimiwa Susan Lyimo na akina Mama Msore popote walipo ambaye aliamia NCCR-Mageuzi.

Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu awape kila la kheri akina mama wote ambao nilijifunza kwenu na mkanipa malezi mpaka hapa nilipofika, Mungu awajaalie kila la kheri. Kama mnakwenda kugombea Majimbo, basi kama kuna mambo mazuri mmewatendea Watanzania, najua mtarudi kwenye Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo; nimewashukuru viongozi hawa lakini nawaomba Chama cha Mapinduzi, kuna matajiri ambao wanachafua Chama chenu. Hawavai sare za Chama! Pesa zao wanatumia ni silaha ya kuigawa demokrasia, kuleta chokocho za kisiasa, watu hawa mwaangalie hata kwenye kura za maoni msiwapitishie. Kama kweli ni wana-CCM kwanza wavalisheni nguo za kijani tujue ni wana-CCM, lakini wasitumie vyombo vya

Ulinzi na Usalama kugombanisha wananchi na wananchi wabomolewe maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni *message sent*; na huyo anauyefanya chokochoko hizo anajijua, sitaki kumtaja jina. Kama alishindwa kufanya kazi ya wananchi wake waliomtuma, anafanya kazi ya kutembeza pesa na kuharibu CV za watu kisiasa, mimi ndiye Msabaha, siharibiki kisiasa na ninafanya kazi na makundi yote ya kijamii. Sibagui Chama, sibagui CUF, sibagui CCM, sibagui Mkristo, sibagui Mbara; wote ninafanya nao kazi na ndiyo maana Zanzibar wananipenda. Wananienda kweli kweli, wala siyo siri! Mheshimiwa Mama Samia atakuwa shahidi! Wananienda kutokana na upendo wangu wa dhati na kutokuwa mnafiki! Mimi sio mnafiki!

Mheshimiwa Spika, yeye kama ni kada mzuri wa CCM, naomba pesa zake azitumie kujenga barabara, miundombinu na asaidie wananchi kero mbalimbali, kuanzia mambo ya jamii, hospitali, ma-school, siyo kwenda kuhangaika na *opposition* ndani ya Jimbo.

Mheshimiwa Spika, sisi tuko kidemokrasia na ndiyo maana Mwalimu Nyerere aliruhusu Mfumo wa Vyama Vingi. Kila mwananchi awe huru kuchagua Chama anachokipenda na awe huru kupigia kura Chama anachokipenda.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la Ulinzi na Usalama. Sasa hivi tunakwenda kipindi cha uchaguzi katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini nilikuwa naomba hii bajeti iangalie ni namna gani ya kudhibiti mipaka yetu. Tudhibiti mipaka, tuangalie mipaka yote ya Tanzania tudhibiti. Navipongeza vikosi vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya pia, lakini hawa mamluki ambao wanatumia vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa ajili ya kuwasafisha; kama walishindwa kufanya kazi za siasa walizotumwa na wananchi, msifanye kazi za kuwasafisha wala msiwasilize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuangalie, kuna tatizo la Bandari bubu. Tatizo hili la Bandari Bubu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, tumeliongea sana. Hizi bandari bubu zimekuwa zinapitisha magendo, madawa ya kulevya na zinahatarisha usalama wetu. Hata hivyo, wanajitahidi. Naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali iangalie hizi Bandari bubu ni namna gani ya kudhibiti ili hata kama kuna kitu chochote; biashara haramu au biashara halali zinaozingizwa, basi TRA wakusanye mapato ya Serikali. Hili ni tatizo sugu! Tunasema kodi kodi, lakini wengine wanapita kwenye njia za panya hawalipi kodi Serikalini. Hao wasiolipa kodi Serikalini, ndiyo hizo fedha zinazokuja kuwa fimbo ya kuchapa Wanasiasa ambao wanafanya kazi kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, hakuna Taifa ambalo limeendelea bila elimu. Naomba Serikali iwekekeze kwenye elimu, tuangalie ma-school yote, school za Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Zanzibar, Vyuo Vikuu, kuna Chuo Huria cha Zanzibar, Tawi lake lipo Zanzibar; pia nao waangalie Chuo kile kwa sababu wanasoma watu wengi wa Serikali. Mtenge bajeti ya Wizara ya Elimu, itawanywe bila kuipunguza na hata ikibidi tuiongeze. Kwa sababu leo mtoto wa kike tusipomjengea *foundation* nzuri ya elimu, hasa watoto wa kike; tumeona wako pembezoni; wananyanyasika!

Mheshimiwa Spika, unakuta vyoo havipo katika *standard*. Mtoto wa kike ni tofauti na mtoto wa kiume, kwa hiyo, hata mazingira yake wakati mwingine yanamfanya haendi Shule anabaki nyumbani, mwisho wa habari, anaolewa. Naomba Serikali iangalie ni namna gani ya kuwezesha Shule ambazo zipo vijijini mpeleke miundombinu na madawati watoto wasikae jamani! (*Makofi*)

Mimi leo nataka nimwambie Mheshimiwa Lukuvi, yeye ni Waziri aliyekaa siku nyingi Serikalini na amefanya kazi miaka mingi sana Serikalini. Waziri kama umefanya kazi, hata wewe Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama, kuna vitu vizuri umefanya Jimboni kwako. Mimi nimetembea kila mahali; na ndiyo maana nasema Mbunge yeyote atakayenishughulikia, nami nakwenda kumshughulikia kwenye Jimbo lake, tena mimi nina sumu kali kweli kweli!

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Lukuvi kile anachokipata ndani ya Serikali, basi awakumbuke watoto wanaosoma kwenye shule zake. Shule zile zina hali mbaya kwa kweli. Utakuta watoto wanakwenda *school* hawana hata kandambili. Tuangalie mazingira; tukijenga *foundation* nzuri ya elimu, basi tutapata wanawake wazuri wenye kujiamini na wenye kutetea kila maslahi ya Serikali. Leo hii tunajivunia tuna Spika Mwanamke. Kama huyu Mama hakujengwa kielimu na akajengwa kiuongozi, leo Kiti kile wanaume wangechukua.

Mheshimiwa Spika, siku zote nawaunga mkono akina Mama. Mahali mwanamke mwenzetu anaposimama, akathubutu, basi na wewe unamuunga mkono. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuwajengee mazingira ya kusoma watoto wa kike, wapate elimu bora ili miaka inavyokwenda basi tutakuja kupata Rais mwanamke. Watasema mwanamke hawezi lakini mimi najua kuna kipindi Rais mwanamke atatoka. Hata kwetu UKAWA ndani ya Chama chetu cha Demokrasia na Maendeleo, najua tutateua Marais wazuri lakini hata wanawake watathubutu pia watachukua fomu za Urais. Hilo linawezekana. Msiseme tu ni CCM, hata UKAWA inawezekana.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye suala la afya. Afya pia ni jambo muhimu lakini tumeangalia Wizara ya Afya, kwa kweli wanatengewa fedha kidogo sana na hii pesa hata haifiki kwa wakati muafaka. Ukienda Hospitali ya *Ocean Road*, jamani nimekaa naongea hapa na Mheshimiwa Al-Shaymaa anajua nami ni mdau; kwa kweli wagonjwa wa Saratani wanateseka sana. Mwangalie ile hospitali, japo Bakhressa anasaidia pale, basi kama kuna watu matajiri ambao wanaweza kuisaidia Serikali na wenye nia njema, basi wasaidie na ninyi Serikali kile kidogo mnachokipitisha kwenye bajeti kifike kisiishie mikononi mwa watu. Leo kila mtu atasimama hapa atasema Waziri hafai, Naibu Waziri hafai, lakini na Makatibu Wakuu ndiyo Watendaji. Mimi Wizara ya Fedha naijua uzuri, wengi ni akina Mama na wengine ni dada zangu wamo humo, lakini akina Mama mhakikishe kile ambacho kinatengwa kinafika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka wakati tunasimamia Sekta ya Viwanja tulimwita Mheshimiwa Saada akiwa Waziri na sasa hivi ile miradi alitoa fedha na kila kitu mambo yakaenda vizuri, viwanja vinakwenda vizuri sasa hivi. Hilo nakupongeza kwa kuwa tulipokuita kwenye Kamati ulisikia ushauri.

Kwa hiyo, haya mengine msiwaachie tu Watendaji wanaume, wanaume wanaweza kuchukua fedha wakatia mifuko ni wakaja wakakutia kwenye jaka la roho. Kwa hiyo, akina baba pia nao mwaangalie vizuri; atakaa pale anakutia jaka la roho, wewe saini hapa mama; na wewe kataa kama mama uonyeshe ujasiri wako kama Mheshimiwa Mama Makinda anavyoonyesha wakati mwingine ujasiri wake humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naongelea suala lingine la reli. Leo tumeona jamani tunakimbilia kwenye barabara. Barabara tunazijenga kwa muda mrefu kwa kodi za wananchi lakini zimekuwa zinaharibika kwa muda mfupi. Sasa tuangalie, uchumi hauwezi kuendelea bila kuwa na Reli ya Kati. Ukiangalia Ruvuma, Sumbawanga, Mpanda na Tabora kuna wakulima wa Mahindi, lakini umeona sasa hivi malori yanapita, mimi nasema ni miradi ya watu. Sasa hivi tuwekeze kwenye reli, kama tunataka uchumi wetu ukue.

Mheshimiwa Spika, leo Japan, Korea na Marekani wameendelea kwa kuwekeza kwenye reli na Malaysia pia wameendelea kwa kuwekeza kwenye elimu. Kwa hiyo, vyote hivi vinatakiwa vipewe kipaumbele. Elimu, Afya, Maji na Miundombinu vipewe kipaumbele. Kwa hiyo, Serikali iangalie, kuchagua ni kupanga.

Mheshimiwa Spika, tusiweke tu bajeti ya kufurahisha, lakini tuweke bajeti ya kufurahisha wananchi wetu kwa sababu ukienda kwa wapiga kura wetu, hali zao huko vijijini ni mbaya kushinda maelezo. CCM niwaambieni, Wabunge wa Majimbo msikae hapa mkashabikia, tena kwenye kura zenu za maoni

mwangalie, mfanye upembuzi yakinifu huko kwenye Majimbo. Wale ambao mnawaona hawajafanya lolote, msiwarudishe, hali ni mbaya. Safari hii CHADEMA tunachukua Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaichukua Serikali kweupee, mchana! Msije mkalia mkaja mkawa wapinzani, mimi hapa napeta. Nasema kwa UKAWA Rais bora atatoka ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo; eeh, atapitishwa na UKAWA tu, ndiyo atatoka! Kwenye Chama cha Demokrasia na Maendeleo ndipo Rais bora atatoka ambaye anajua kero za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu pia suala la maji. Maji kwa kweli yamekuwa ni kizungumkuti. Naomba Wizara ya Maji itengewe bajeti kutosha. Tunaangali leo Mkoa wa Dar es Salaam ukiangalia, EWURA wakati mwingine wanapitisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA-**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mungu akubariki.

**SPIKA**: Ahsante kwa kuongea vizuri. Msemaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia kuwa na afya njema na mimi nikaweza kuchangia katika hotuba iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa umetuongoza katika kipindi hiki tukiwa katika utulivu na amani ndani ya Bunge la Jamhuri na nimeona kabisa utulivu wako, hekima zako na busara zako ni mfano wa kuigwa na Watanzania na akina mama waliokuwa katika madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Waziri wa Fedha, kwa kweli ni mwanamke ambaye ameonyesha ujasiri kuwa anaweza. Ameonyesha kuwa sasa hivi Tanzania tunaweza kujiendesha wenyewe bila kutegemea wafadhili kutoka nje kwa asilimia kubwa. Tuendeleo kusimamia ili baadaye tujitegemeo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu anasema, mtu yeyote mwenye kusema kweli, basi ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. Mkoa wa Lindi na Mtwara tulikuwa katika hali ngumu sana kuhusu usafiri. Ilikuwa mtu unatoka Dar es Salaam kwenda Lindi au Mtwara unakaa mwezi unahangaika. Lakini kupitia Serikali ya CCM leo tunakwenda Mtwara mpaka Lindi kwa masaa manne au matano, tunasema ahsante kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwa hili limefanyika na tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi unasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza ukiwa katika lami; unasafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya mpaka Rukwa sasa inamalizika mpaka Katavi tukiwa katika lami. Tunakwenda mpaka Kigoma, tunaona hali nzuri iliyokuwepo Kigoma kwa barabara; tunaona viwanja vya ndege! Lazima tuseme kweli kama Mwenyezi Mungu tupo katika mafanikio makubwa ambayo tunaomba yaendelee. Alichokifanya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni kizuri, basi anayemwachia aendeleze hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge na kipindi hiki ni cha pili. Lakini nasema kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nimejifunza mengi sana kwa kukaa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano; kwanza busara na hekima zinatakiwa zitangulizwe mbele. Tumekaa katika Bunge hili tumeonyesha vituko vingi sana. Siyo tena viigwe katika Bunge linalokuja baadaye. Tunaomba Mwenyezi Mungu tuwalete Wabunge ambao watakuja kuleta heshima ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeonekana Bunge letu sasa hivi tumechanganya uhuni na mambo mengi ambayo unaona kabisa yanatuletea Bunge kudhalilika. Hii haikubaliki! Kama uliona Bunge ni sehemu ya kuja kufanya masihara, basi Bunge siyo sehemu ya masihara! Ni sehemu ambayo unatakiwa uonyeshe uadilifu, hekima, busara na utulivu ndani ya hekima yako ili uweze kufanya kazi katika Bunge la Jamhuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natoka katika Mkoa wa Lindi ambao ulikuwa ni Mkoa wa mwisho katika umaskini, lakini nasema Lindi sasa hivi siyo maskini tena. Baada ya miaka mitano nina imani tutakuwa katika Mikoa ambayo inaanza kupaa kama tunavyoona jirani zetu Mtwara. Mtwara walikuwa maskini kama Lindi, lakini sasa hivi Mtwara imeanza kupaa kuliko mikoa mingine ambayo ilikuwa nyuma. Hii yote ni kwa ajili ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kusimamia na kuhakikisha tunaanza kupata mafanikio tunayoyaona. Mafanikio ya gesi na kilimo, tukiyasimamia basi nina imani kwamba na sisi Lindi itafanikiwa. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, nataka nionyeshe ni maeneo gani Serikali isimamie ili Mkoa wa Lindi ufanikiwe, kwanza ni kilimo. Lindi tunalima ufuta kwa wingi sana; tunavuna korosho na tunalima vyakula vingi lakini hatuna soko. Tumelima Ufuta kwa nguvu zote kwa vile mwaka 2014 ufuta uliuzwa kwa Sh. 2,500/=. Lakini leo tumeanza kulanguliwa ufuta kwa Sh. 800/=. Tunaomba Waziri wa Kilimo, Waziri mwenye dhamana akasimamie zao la ufuta.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa Lindi maskini, unanunua ufuta kwa Sh. 800/= unategemea atafanikiwa lini? Tunahitaji kumkomboa Mtanzania maskini. Watanzania wengi walioko vijijini ndio wanahitaji wasaidiwe sasa hivi; na kitakachowasaidia Watanzania waliokuwa vijijini ni kilimo. Tukisimamia kilimo tutajikuta tumewasua wale watu ambao wako katika hali ngumu. Tutasaidiaje katika kilimo? Tukiwapelekea barabara!

Mheshimiwa Spika, Lindi kuna maeneo leo ukizungumza kuhusu barabara ni mtihani. Kwa mfano, unakwenda Nangaru kilomita 50 kutoka Lindi lakini inakuchukua kutwa hujafika Nangaru, lakini ni maeneo mazuri sana. Wakisaidiwa watu wa Nangaru watailisha Lindi na siyo Lindi tu, hata Mikoa ya jirani itapata chakula kingi kutokana na maeneo yao ni oevu lakini hawana barabara. Maeneo ya Mipingo, Matapwa na Kiwawa; tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana akaangalie barabara, wale bado wako katika hali ngumu. Tumepata barabara kubwa lakini sasa hivi tunataka barabara za vijijini zipitike ili wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, nimeiangalia Tanzania, wanaolipa kodi ni watu wachache. Tukiangalia raslimali za Tanzania na wanaolipa kodi ni vitu viwili tofauti! Hapa kuna mchanganyiko wa wakusanyaji kodi nao hawafanyi kazi vizuri na wanaolipa kodi nimeangalia zaidi ni Walimu, Manesi, Wafanyakazi wa Serikalini lakini wafanyabiashara waihurumie nchi hii walipe kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mianya katika kulipa kodi ni migumu, watu hawataki kulipa kodi. Leo tunahitaji maji, hivi bila pesa tutafanya nini? Tunahitaji Walimu wakafundishe wapate mishahara; bila kodi tutafanya nini? Madaktari wakafanye kazi, bila kodi utamlipa mshahara gani? Tujiulize kwa nini tunakuwa wagumu wa kulipa kodi? Hatulipi kodi Watanzania! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Kariakoo, unakuta mtu anahamasisha watu wasilipe kodi. Kwa kweli kama ingekuwa ni nchi nyingine, yule ni mtu wa kufungwa kabisa! Unapomwambia mtu asilipe kodi, halafu hospitali dawa zitapatikana wapi? Unamwambia mtu usitumie mashine kwa kulipia kodi halafu alipe kienyejiyenyeji, BVR asilipe halafu tunakwenda wapi? Tunarudi katika *analogy*. Sasa hivi ni ulimwengu wa *digital*, ni lazima tuhakikishe mashine zinatumiwa, watu wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, tunakuja kwenye masuala ya viwanda. Miaka ya nyuma tulisimamia sana viwanda vyetu vya ndani. Tulikuwa hatununui Khanga kutoka nje. Tulikuwa na viwanda vya ndani ya viberiti kutoka Kilimanjaro, hatukuwa tunaagiza viberiti kutoka nje. Tulikuwa na viwanda vya mafuta Ilulu lakini leo ufuta tumejaza Lindi, lakini unakaa kwa mwananchi kwa vile hatuna viwanda. Tungekuwa na viwanda tungekamua mafuta na tungeuza mafuta mazuri na watu wangepaidika na mafuta yetu. Lakini tumefunga viwanda kwa ajili ya uwekezaji ambao ni wa kubabaisha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu, wale wote waliojikuta wamechukua viwanda hawavitumii, hebu tutele azimio humu ndani tuwanyang'anye. Haiwezekani leo wananchi wa Nachingwea wana ufuta na karanga lakini viwanda vimefungwa. Unajuliza, kwa nini vile viwanda vimefungwa? Hakuna majibu! Tunauliza maswali haya kwa muda wa miaka 10, hatuna majibu, viwanda vimefungwa kwa nini? Ni kwa sababu wanataka kupeleka mazao nje kama *raw materials*. Kupeleka mazao nje kama *raw materials*, mnamfanya Mtanzania akose ajira.

Mheshimiwa Spika, ufuta ukiupeleka nje kama *raw material* wanakamua mafuta ambayo yana thamani kubwa na mashudu wanatumia keki kwa ajili ya mifugo yao. Je, sisi tunafaidika na nini na ufuta huo? Wanaununua ufuta kwa bei ya Sh. 800/=, ni bei ya kumkandamiza mwananchi. Inanisikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikienda vijijini wananiambia mama, angalia ufuta umetukalia majumbani, hauna soko. Najuliza, Idara ya Masoko na Ushirika inafanya nini? Sipati majibu! Naomba nipate majibu. Nauliza, zao la ufuta litasaidia nini kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Mtwara na Mikoa mingine wanaolima ufuta sasa hivi; hakuna soko! Lakini siyo kuwa hakuna soko, ni ubabaishaji wa wafanyabiashara kutukandamiza katika zao. Wanangojea kununua kwa Sh. 800/=, wanakwepa kodi, hawalipi ushuru ili wakauze kwa bei kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naona Tanzania tufike mahali tuwe makini tuusimamie uchumi wetu tusinyoosheane vidole. Kila mmoja awajibike kwa Utanzania wetu kuwa sisi tunaweza kama walivyoweza wenzetu.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda Malaysia, walikuwa ni watu maskini kama Watanzania. Lakini wamepata umeme wa REA asilimia 97 na sasa hivi wamejikwamua kiuchumi. Kila ukisikia Watanzania wanakawenda Indonesia au Malaysia kujifunza, kwa nini wenzetu walifanyikiwa? Walifanikiwa kwa vile waliamua kujifunga na kuhakikisha kuwa uchumi wao utakua na sisi Watanzania tunaweza kuwa kama wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumepeleka umeme, nashukuru, leo tunazungumza vijiji vya Mkoa wa Lindi karibu asilimia 80 tunataka kupata umeme. Fursa ya umeme utatusaidia ku-process Korosho kule kule Lindi. Hatutaki kupeleka Korosho nje; kila siku wanatubabaisha, mara bei imeteremka, mara imepanda, hakuna! Bado tuna uwezo wa kulisha zao la korosho kwa Watanzania nzima na bado tuna uwezo wa soko la ndani kufanya kazi. Hata yale mashudu tutakamua mafuta Lindi na tutapata ajira kwa wanalindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, mwenye dhamana naomba aingalie Lindi kwa huruma ili tupate ajira. Vijana wanahangaika, wanafukuzwa Kariakoo saa 24. Mkiwawekea mazingira mazuri, inawezekana kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa hekima na busara zako na busara zako kuhakikisha Bunge hili umeliwezesha kufikia hapa. Umekaa na watu wengine hawana nidhamu, lakini umekuwa mvumilivu. Watu wanatoa matusi ndani ya Bunge, umekuwa mvumilivu. Naomba Mwenyezi Mungu akupe nguvu, akuwezeshe hapo ukitoka, akujaalie na urudi tena usiogope. Tupo wanawake, tutakupokea na utarudi tena ndani ya jengo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana na nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa msemaji wetu wa mwisho kwa sababu tumerudia tena kwenye ratiba zile za kawaida. Wengine ambao hamkupata leo nafasi, kesho bado kuna nafasi, mtapata nafasi ya kuongea. Isipokuwa nawaomba wale wanaobakia huko wanakobakia, tafadhali wajaribu kuja hapa ndani. Wanabakia huko wanakobakia, wanaangalia kwenye TV, eeh! Jamani, mnatakiwa muwepo humu ndani. Kwa hiyo, naomba sana tuwepo humu ndani kwa sababu suala la kuzungumza bajeti ni vizuri tukawepo humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi kipindi cha Waziri Mkuu hakitakuwepo. Kwa hiyo, msije mkaamka asubuhi sana kwenda kule, hakipo kipindi. Kwa hiyo, ni sawa tu, si mnajua! (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, basi nawashukuru sana kwa jioni hii, mkapumzike. Naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 18 Juni, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*